ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe	- Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	- Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	- Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	- Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	- Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	- Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	- Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	- Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	- Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	- Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	- Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	- Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	- Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	- Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	- Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	- Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	- Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	- Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	- Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tatu – Tarehe 21 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 128

Serikali Kukubali Kuulizwa Maswali ya Papo kwa Papo Katika Vikao vya Baraza la Wawakilishi

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar imelipa Baraza la Wawakilishi mamlaka ya kuiuliza serikali masuala mbali mbali yanayohusu maslahi ya taifa na wananchi kwa ujumla, na kwa kuwa majibu ya masuala haya yanatakiwa yawe ya kweli na uhakika na sio ya kisiasa pekee, na kwa kuwa sasa wananchi wanafuatilia mijadala ya Mabunge kote ulimwenguni.

(a) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba wakati umefika wa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kujibu masuala ya papo kwa papo, ili kukidhi kiu ya wananchi na kuonesha uwajibikaji wa dhati wa serikali kwa wananchi wake?

(b) Kwa kuwa Mhe. Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anajijengea heshima zaidi serikali kwa wananchi wa Tanzania kutokana na uwezo mzuri wa kujibu masuala ya papo kwa papo. Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakichukuliaje kitendo hiki muhimu?

(c) Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ni chombo cha kukuza demokrasia nchini na chenye kuendesha shughuli zake kwa uwazi. Je, Mhe. Waziri, huoni kuwa serikali kuendelea kujibu masuala kwa njia inayotumika hivi sasa kunaficha dhana nzima ya uwazi na uwajibikaji wa serikali kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 128 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe, kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, miongoni mwa kazi za Baraza la Wawakilishi kupitia kwa Wajumbe wake ni kuiuliza serikali maswali kwa lengo la kutetea maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Shughuli za Baraza hutekelezwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni. Kwa sasa hakuna kati ya nyenzo hizo iliyoweka utaratibu wa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kujibu maswali ya papo kwa papo kwenye Baraza la Wawakilishi. Ndio maana zoezi la kujibu maswali ya papo kwa papo halifanyiki.

Hata hivyo, kama jambo hili litaonekana na Baraza lako tukufu linahitaji, basi kwanza linahitaji mazingatio makubwa kabla ya kuanza utekelezaji wake, ili utaratibu huo utakapotumika uwe na tija kwa wananchi.

Pamoja na kwamba hakuna utaratibu wa maswali ya papo kwa papo, lakini wajibu wa kikatiba wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuiuliza masuala serikali unatekelezwa ipasavyo. Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinatoa fursa ya kuwepo kipindi cha saa moja na nusu katika kila siku ya kikao cha Baraza kwa Waheshimiwa Wajumbe kupata fursa ya kuiuliza serikali maswali na Waheshimiwa Mawaziri kujibu maswali hayo.

(b) Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeweka utaratibu wake, ambao imeona unafaa utumike katika kujibu maswali ikiwemo maswali ya papo kwa papo yanayojibiwa na Waziri Mkuu.

Aidha Baraza la Wawakilishi kupitia Kanuni zake Nam. 34 – 41 limeweka utaratibu mzima kuhusiana na maswali na majibu, utaratibu huo unamtaka Waziri kujibu maswali ipasavyo, aidha unatoa fursa ya kuulizwa maswali ya nyongeza. Vile vile Mhe.

Makamo wa Pili wa Rais amekuwa akisaidia kujibu na kuyatolea kauli ya serikali maswali wizara mbali mbali yanayoulizwa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaamini kwamba, utaratibu huu uliowekwa na Baraza la Wawakilishi unaotumika sasa unatosheleza utekelezaji wa demokrasia, uwazi na uwajibikaji katika nchi yetu.

(c) Sikubaliani na Mhe. Mwakilishi kuwa utaratibu wa sasa wa serikali kujibu maswali unaficha dhana nzima ya uwazi na uwajibikaji.

Mhe. Spika, utaratibu huu uliopo sasa umewekwa na Baraza lako tukufu kupitia Kanuni zake, ambazo hivi karibuni zilipitishwa kwa kauli moja na Waheshimiwa Wajumbe, kwa kujua kwamba utaratibu huu umetumika kwa kipindi kirefu na umekuwa na ufanisi mkubwa pamoja na kuimarisha dhana ya uwazi, uwajibikaji na demokrasia.

Lengo kuu la kuiuliza maswali serikali na takriban katika nchi zote za Jumuiya ya Madola ni kutaka wajumbe wapatiwe taarifa au kuhimiza serikali kutekeleza jambo fulani. Kwa hivyo, majibu yaliyofanyiwa utafiti wa kina yanakidhi haja hiyo kuliko majibu ya papo kwa papo.

Waheshimiwa Mawaziri hufanya jitihada kadri iwezekanavyo kujibu kwa usahihi na kwa ufasaha mkubwa kutokana na kufanya utafiti, hivyo ni muhimu kwa utaratibu huu ukaendelea ili kupata majibu sahihi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).
Kwa kuwa amekiri kwamba sisi Wawakilishi tunapeleka maswali yetu wizarani na yanapata kufanyiwa utafiti wa kina kwa ajili ya kujibiwa. Maswali yanayomhusu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais moja kwa moja yatakuwa ndio papo kwa papo.

(a) Hivi haoni kwamba anaipunguzia uwajibikaji serikali, kwa sababu maswali tunayopeleka yanachukua muda mrefu mpaka yanapitiwa na muda bado hayajibiwa. Kwa hivyo, hali hii inaonesha wazi kwamba serikali haiwajibiki kikamilifu katika maswali ambayo tunapeleka?

(b) Nadhani ni vyema tukafuata utaratibu huo, ili kuamsha ari ya mawaziri kufanyakazi nzuri zaidi na hasa upande wa kushughulikia masuala ya kijamii?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi kwamba maswali ya papo kwa papo bado hayajafanyiwa utafiti wa kina na serikali ni suala la *collective responsibility*, kwa maana tunaendesha kwa pamoja. Hivyo, kufanya utafiti na tukaja na majibu yaliyosahihi na ya kina, nadhani yatasaidia sana wananchi wetu kuliko dhana ya mtu mmoja. *(Makofi)*

Pamoja na kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni mtu mwenye heshima kubwa katika nchi yetu, lakini bado ni binaadam na tumeshaona mifano katika Bunge wakati yanapotokezea matatizo ya kujibu maswali ya papo kwa papo na athari zake kwa nchi. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nakumbuka wakati tunafanya marekebisho ya Kanuni mwaka 2009 kipengele hiki cha kumuuliza wakati ule Waziri Kiongozi maswali ya papo kwa papo kilikuwemo kwenye marekebisho tuliyoyafanya, tulikubaliana kwamba utekelezaji wa kifungu kile ni baada ya Uchaguzi Mkuu ambapo tutakuwa na serikali mpya na hivyo ndivyo tulivyokubaliana. Lakini marekebisho ya mwisho tuliyoyafanya hili halikuwemo kwenye marekebisho ya Kanuni. Je, ni sababu zipi zilizofanya serikali kuondosha kifungu kile kinyemela bila ya kuliarifu Baraza hili? Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, serikali haifanyi unyemela wa aina yoyote na zile ni Kanuni za Baraza na wenyewe ni Wajumbe wa Baraza na wenye maamuzi ni Baraza la Wawakilishi na ndio mlioamua kwa kauli moja kwamba Kanuni tulizonazo sasa ni Kanuni nzuri na inafaa tuzilinde. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali kwa nia njema imeanzisha Vitengo vya Utafiti katika Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kuwa suala hili la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kujibu maswali ya papo kwa papo yatakuwa yanamjengea heshima zaidi na serikali kwa jumla na vitengo hivyo vipo.

Kwa hivyo, ni lini hasa serikali itatoa ahadi ya kwamba litafanyiwa utafiti, ili tupate kumuuliza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais maswali ya papo kwa papo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, katika swali langu la msingi nilisema hivi kama Baraza lako tukufu litaona yapo mahitaji ya kuanzisha utaratibu huo basi tutahitaji kufanya utafiti wa kina kabla ya kufanya uamuzi huo, kwa sababu inaweza kutoa athari kubwa kwa wananchi. Kwa kweli hapa inaonekana sura Wajumbe wa Baraza wana hamu ya maswali na majibu ya papo kwa papo.

Mhe. Spika, naomba suala hili tulichukue na tulifanyie utafiti na mapendekezo yetu tuyalete katika afisi yako na halafu tuone kama jambo hili linawezekana kuendelea kulifanya. *(Makofi)*

Nam. 80

Uanzishaji wa Serikali za Mitaa

Mhe. Farida Amour Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar imekuwa na muundo wa Halmashauri na Mabaraza ya Miji kwa muda mrefu.

(a) Ni lini serikali itaona umuhimu wa kuwa na Serikali za Mitaa hapa Zanzibar?

(b) Je, serikali haioni kucheleweshа kuwepo kwa Serikali za Mitaa inadumaza demokrasia katika ngazi za chini?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa kufuatilia muundo wetuu pamoja na utendaji wa Halmashauri. Kwa hivyo, naomba nitoe maelezo machache kabla ya kumjibu.

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar kifungu Nam. 128 kinaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa, ambazo uchaguzi wake, madaraka na kazi zake zitakuwa kama zitakavyoelezwa katika Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi lilitunga Sheria Nam. 3 ya mwaka 1995 na sheria Nam. 4 ya mwaka 1995, kwa ajili ya kuanzisha kazi na kuweka utaratibu

wa utendaji wa Baraza la Manispaa, Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji ya Wete, Mkoani na Chake-Chake. Mhe. Spika, hatua hii imewezesha serikali kuanzisha Serikali za Mitaa hadi katika ngazi ya Wadi. Kwa hiyo, naomba kumjuilisha Mhe. Mjumbe kwamba Serikali za Mitaa tayari zimeshaanzishwa zipo na zinafanyakazi

Sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inaelewa umuhimu kama nilivyosema wa kuanzisha hizo Serikali za Mitaa, hasa ikizingatiwa kuwa ni vyombo vya kukuza demokrasia na kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika ngazi za chini kwenye maendeleo yao. Hadi sasa Serikali za Mitaa katika ngazi ya Wadi yaani Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya zinafanya kazi nzuri.

Kwa manaa hiyo, ipo nafasi zaidi ya kuongeza ufanisi na tija pindi wakiwezeshwa vizuri zaidi na kuwa na watendaji wenye taaluma inayolingana na kazi zao pamoja na uzoefu mkubwa wa kazi zao.

(b) Serikali hivi sasa inakamilisha mchakato mzima, ambao utaweka mkakati wa kuimarisha Serikali za Mitaa kwa kutaarisha Mpango wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa (*Local Government Reform Program*), ambao pia umeainishwa katika Mpango wa Mageuzi wa Utumishi wa Umma. Aidha serikali imo katika hatua za mwisho za matayarisho ya Sera za Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, kukubalika kwa utekelezaji wa mipango hiyo, ndio itayotoa muelekeo na sura ya kama ipo haja ya kuwa na Serikali za Mitaa ya ukubwa gani chini ya ngazi ya wadi hasa ikizingatiwa eneo dogo la nchi yetu.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kusema kwamba Serikali za Mitaa zipo Zanzibar hadi ngazi ya Wadi. Lakini naamini atakubaliana na mimi kwamba katika ngazi hii ya Wadi ambapo kuna Madiwani ambao wamechaguliwa na wananchi Madiwani hao wamekuwa wapo tu na kazi zao kimsingi zimekuwa zikifanywa na Masheha, ambao hawachaguliwi na

wananchi isipokuwa ni watu wa kuteuliwa. Kwa hivyo, uwajibikaji wao kwa wananchi unakuwa mdogo kuliko wale ambao waliochaguliwa na wananchi, ambao wangewaheshimu na kuwatumikia zaidi.

(a) Kwa msingi huo swali langu ni kwamba je, lini serikali itachukua hatua za kuhakikisha kwamba madaraka yale ya msingi katika ngazi za chini yanafanywa na Madiwani ambao wamechaguliwa na wananchi na kuyaondoa kwa kiasi kikubwa kwa Masheha ambao hawachaguliwi na hivyo wanashindwa kuwajibika ipasavyo kwa wananchi wao.

(b) Katika haya Mabaraza ya Miji, Manispaa pamoja na Halmashauri inaonekana utaratibu wa Zanzibar ni wa aina ya pekee ambao haupo popote duniani, kwamba badala ya Mabaraza haya kuwa na maamuzi kupitia vikao vyao kwa Madiwani wanaochaguliwa na wananchi, zaidi inaonekana wanakutana lakini maamuzi yanayotekelezwa ni yale ya Wakurugenzi kwenye Mabaraza haya ndio wanayoyataka na kusema Wakurugenzi hawa yupo Baraza la Manispaa amechaguliwa na Rais na mwengine amechaguliwa na Waziri.

Kwa hivyo, lini serikali itaona haja ya kurejesha madaraka kwa Mabaraza yenyewe kufanya maamuzi na kuwaacha Wakurugenzi pamoja na watendaji wao kuwa watekelezaji wa maamuzi yanayofanywa na Mabaraza haya ya Miji? *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nimejitahidi kumsikiliza kwa makini Mhe. Mjumbe, lakini kwa bahati mbaya anaongea kwa haraka na *echo* bado ipo kidogo. Kwa hivyo, nitajitahidi sana kumjibu kama nilivyomsikia na kama sikukidhi haja basi anaweza kuniuliza tena.

Mhe. Spika, mgongano wa kazi na Masheha. Kwa kweli huu ni utashi wa watu wenyewe, kwa sababu kazi zimeainishwa wazi kwenye Sheria ya Kuanzishwa (*An Act To Establish the District and Towns Councils and others matters connected there is*) Sheria Nam. 4 ya mwaka 1995 na kazi zimeainishwa kwa uwazi kabisa.

Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo kwa lugha ya Kiingereza kazi moja kama hivi. ifuatavyo:-

"*Every District Council shall perform in relation to its area of jurisdiction the following functions:-*

Mhe. Spika, zipo kazi kwenye sheria kama nne nazo ni:-

(i) *To formulate, coordinate, supervise the implementation of plans for the economic, commercial, industrial and social development;*

(ii) *To insure the collection and proper realization on the revenue of the Council;*

(iii) *To make by laws applicable through out the areas of jurisdiction and*

(iv) *To consider regulate and coordinate development plans projects and programs of villages and township Council within the areas of jurisdiction.*

Mhe. Spika, hizi ni kazi wa Waheshimiwa Wadiwani. Sasa kama masheha wanachukua kazi zao basi hiyo si sahihi, nadhani Sheha yeye ni mtawala katika ngazi ya chini na dhana zake pia zimewekwa na hapa sina. Kwa hivyo, hii migongano ni kama nilivyosema ni utashi tu wa watu wenyewe, lakini mambo yako wazi kabisa na hivi sasa tunajitahidi kuwapa *seminars* Madiwani, ili wajue wajibu wao na Masheha pia, kwa lengo la kujua wajibu wao na kuepusha mgongano.

Swali la pili sikulisikia vizuri, lakini nadhani Mhe. Mjumbe alitaka kujua hizi kazi pamoja na *benefits* zao. Mhe. Spika, naomba areje tena kidogo kwa sababu sikumsikia vizuri tena kwa taratibu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ameuliza kwamba Wakurugenzi pamoja na Makatibu wa Halmashauri wale imekuwa kama ndio wanaoongoza hizo Halmashauri. Kwa hivyo, anachokitaka ni lini hasa Wakurugenzi pamoja na Makatibu hao watakuwa wanatekeleza maamuzi ya Manispaa pamoja na Halmashauri hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Kwa mujibu wa hii sheria Katibu wa Halmashauri ndiye Mtendaji Mkuu wa Halmashauri na hiyo imewekwa wazi kabisa, sasa kama yeye ndiye Mtendaji Mkuu na anawajibika kwa Waheshimiwa Madiwani. Mhe. Spika, kama haifanyiki hivyo basi hilo ni tatizo na inabidi tuliweke sawa.

Vile vile kwa huyu Mkurugenzi naye nafasi yake pia inabidi awajibike kwa serikali yake pale. Hali hii ni ku-*share* madaraka tu kama anafanya anavyotaka yeye bila ya kuwasikiliza wenzake nafikiri hiyo sio sahihi. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza ya swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja lenye vifungu viwili kama ifuatavyo:-

Amesema kwamba Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Miji yameanzishwa kwa Sheria Nam. 4 na 5 ya mwaka 1995 na hivi sasa wizara imo kwenye mikakati ya kufanya *reform*.

(a) Kwa kweli kilio kikubwa cha Madiwani ni mshahara. Je, kwenye *reform* hiyo imezingatiwa?

(b) Hivi sasa serikali imeanzisha Mfuko wa *CDF* kwa ajili ya majimbo. Lakini wenzetu Bara Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe kwenye Halmashauri zile na sisi sheria haikutuweka. Je, kwenye marekebisho hayo na sisi tutakuwemo kwenye sheria hiyo ya Mabaraza kwa ajili ya kutetea mfuko wetu? *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Waheshimiwa Madiwani wameleta maombi serikalini ya kupatiwa mshahara. Kwa kweli hilo tumekuwa tukilizingatia na niseme kwa kushirikiana na Serikali Kuu hili bado tunalizingatia na hasa tukitilia maanani kwamba wenyewe wanazalisha. Sasa kama wanazalisha basi hilo ni la kuzingatiwa na kufanya utaratibu kuona vipi tunalifanikisha hilo.

Mhe. Spika, ni kweli kwa sababu ya utendaji wao pamoja na wanavyofanya, lakini nadhani Mhe. Mjumbe anafahamu kwamba hawaondoki patupu, wanao utaratibu wao wenyewe wa kupata posho ambazo zinawasaidia kidogo.

(b) Kuhusu *CDF* ni kweli kwa utaratibu uliopo *CDF* Waheshimiwa Madiwani wawili wanaingia kwenye kikao hicho cha kupanga hizo *programs* kama sikosei na sisi Wawakilishi hatumo. Mhe. Spika, nakumbuka suala hili mara nyingi Mhe. Mjumbe amekuwa akituuliza.

Kwa hivyo, ni vyema kama serikali suala hili tulichukue na tukae na kwa sababu sisi tunayo mipango ya kuanzisha Sheria yetu ya *CDF* ya Zanzibar. Kwa maana hiyo, hilo tutalitia maanani na tuoni vipi tutalifanikisha.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa utendaji wa Serikali za Mitaa ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi. Vile vile Serikali za Mitaa katika Zanzibar hazina ufanisi kwa muda mrefu na kwamba serikali imeandaa mpango huuu wa *reform*, lakini *reform* hii sasa ni muda mrefu tunaisikia inatajwa tuu na Waheshimiwa Wawakilishi wamekuwa wakidai kwa muda mrefu sana iharakishwe.

Sasa Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja ya kutwambia ni lini *reform* hiyo italetwa hapa Barazani?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, tatizo hili limekuwa la muda mrefu na hii niseme kwamba hili suala sio rahisi lazima tukiri na sisi Serikalini tumeona uzito wake, kwa hivyo tunaichukua kadri ya kujifunza kwa wenzetu lakini pia tunapojifunza tunaona zile juhidi zake hapa kwetu zitafanyika vipi, nakupa mfano Mhe. Abdalla Juma wewe unatokea Wilaya ya Mkoani pale pana halmashauri na Baraza la jiji hiyo Chake-Cheke tu sasa tizama migongano iliyopo, wanagongana maeneo, wanagongana *revenue* wanagombania hata kazi hiyo Chake- Chake tu.

Sasa haya mambo yote inshaalla yatafanikiwa.

Nam. 11

Kasma ya Fungu la Vijana

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:

Hivi sasa Zanzibar inao vijana wengi wanaozururа ovyo bila ya kufanya kazi. Vijana hao wanapokwenda Wizara ya Vijana kutafuta msaada wa kuwezeshwa hujibiwa kwamba Kasma ya Fungu lao la Vijana ni dogo na fedha hizo kidogo haziingizwi kwa wakati.

(a) Mhe. Waziri nakuomba ulieleze Baraza letu Tukufu ni kwa nini fungu linakuwa dogo kiasi cha kushindwa kusaidia vijana hao.

(b) Kwa sababu Wizara inayohusika na vijana haipewi fedha ya kutosha kushughulikia vijana wetu naomba kujua Serikali imetayarisha mpango gani KItaifa kuwasaidia vijana wetu.

(c) Kwa kuwa Maofisa wa vijana hawapewi fedha za kutendea kazi huoni kwamba Serikali imetekeleza nguvu kazi kubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, jukumu la kupanga vipaumbele vya matumizi kwa taasisi mbali mbali za serikali si la Wizara ya Fedha bali ni la taasisi husika baada ya kupokea kiwango cha ukomo wa matumizi *(ceiling).* Aidha, mgao wa matumizi unapofanyika kwa kila mwezi kwa vifungu mbali mbali vya Wizara kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopanga na Wizara husika. Hata hivyo, ni vyema kwa Wizara inayoshughulikia masuala ya vijana kutoa kipaumbele katika fungu hilo la vijana ili vijana wengi zaidi waweze kuwezeshwa.

(b) Mhe. Spika, kisera Wizara ya Vijana Maendeleo ya wanawake na Watoto ndio iliyopewa dhamana ya kusimamia vijana, lakini Serikali imeandaa *program* mbali mbali ambazo zinalenga katika kuwasadia vijana na serikali imepanga kuzitumia katika mipango ya kitaifa ifuatayo ambayo inawasaidia vijana wetu.

i) Kuwafundisha vijana elimu ya ufundi ili waweze kujiajiri na kuajiriwa kulingana na mahitaji ya soko la ajira.
ii) Kuwapatia mikopo ya kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kushirikiana na benki mbali mbali .

(c) Mhe. Spika, kama nilivyosema awali fedha za kuwasaidia vijana ziko katika programu mbali mbali, kinachohitajika ni kwa Wizara husika kutoa kipaumbele katika matumizi hasa katika programu za vijana. Hata hivyo, vijana ndio nguvu kazi inayotegemewa na Serikali na jamii kwa ujumla, kwa msingi huu haiwezi kutekelezwa bali Serikali itaendelea kuimarisha nguvu kazi hii ili iweze kuleta tija kwa vijana wenyewe na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wa maafisa wa vijana ni imani yangu kuwa wanayo majukumu mengi ya kufanya ikiwa ni pamoja na kuratibu mambo yote yanayohusu vijana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Naomba nimuulize Mhe. Waziri yuko tayari kushirikiana na hizo Wizara ili vijana na wao waweze kupatiwa fungu lao la kasma.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Wizara yangu kama jina linavyosema Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo nataka kumthibitishia Mhe. Viwe, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Wizara hizo nilizozitaja ili tuweze kuandaa program zaidi za vijana na hatimae kuweza kuweka fedha zaidi kwa ajili ya vijana wetu.

Nam. 17

Leseni za Udereva

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:

Pamoja na jitihada za Wizara za kuweka mazingira mazuri kwa vijana wetu kujiajriri katika fani ya udereva wa magari kwa kuruhusu vyuo vya mafunzo ya udereva vya watu binafsi, vijana wanaochukua mafunzo hayo wamekuwa wakipatiwa leseni za magari ya Private, yaani daraja la B1 badala ya leseni za gari za abiria ambazo zingewawezesha kujipaltia ajira.

(a) Ni sababu zipi zinazosababisha vijana hao kupewa leseni za madaraja mengine ambazo haziwasaidii sana katika kujitafutia maisha.

(b) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kitendo hicho kinawavunja moyo vijana hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza ninatoa shukurani kwa Mhe. Mwakilishi kwa kuziona jitihada za Wizara yangu za kuweka mazingira mazuri kwa vijana wetu kujiajiri katika fani ya udereva na kuruhusu vyuo vya mafunzo ya udereva vya watu binafsi.

(a) Kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 na Kanuni ya mwaka 2003, ya usalama barabarani inaelekeza kuwa dereva yeyote aliyemaliza mafunzo yake hatopatiwa leseni ya kuendesha magari ya abiria hadi pale atakapopata uzoefu wa kuendesha magari mengine kwa kipindi kisichopungua miaka miwili. Sababu hii hupelekea kuwajengea uzoefu madereva wetu sambamba na suala la umri wa madereva hao.

(b) Kitendo hicho hakiwavunji moyo vijana wetu ila kinawapa uzoefu na umakini kwa madereva wote wanaotaka kuendesha magari ya abiria.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa wanafunzi wanapotoka chuoni huenda kwa mkaguzi kwenda kupewa leseni au huenda kwa Silva kufanyiwa matayarisho mengine ili ya kuonekana kwamba dereva huyu kafanyakazi vizuri na kupewa leseni ile. Je, Mhe. Waziri hawa madereva wanaopewa leseni hizi za D na C1na D1 huwa wanapewa na nani?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Katika majibu yangu mama nimeeleza kwamba madereva wa gari za abiria kwa mujibu wa sheria Nam. 7 mwaka 2003 inaeleza kwamba, ili uweze kupewa leseni ya udereva wa gari za abiria unahitajika upate uzoefu wa leseni za daraja nyengine za leseni kwa kipindi kisichopungua miaka miwili, baada ya kupata uzoefu huo wa miaka miwili kupewa na leseni za daraja jengine ndipo utapandishwa daraja na kupewa leseni za gari ya abiria.

Mhe. Mbarouk Mussa Wadi (Mtando) Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Vyuo vya madereva hivi vingi naona viko kwenye *private sector*, serikali ina mpango gani wa kuanzisha vyuo hivi ili na wananchi kule vijijini vyuo vikajengwa kwenye mikoa yao ili wakaweza kwenda kujifunza, kwa sababu hivi vyuo vyote vinaonekana viko mjini. Mwananchi anayetaka kujifunza kutoka kijijini lazima aje mjini apige kambi kwanza ya kuja kujifunza. Je, ni lini serikali itaanzisha vyuo hivi katika Mikoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, utaratibu wa kupata leseni ni kwamba unatakiwa kwenda katika vyuo vya udereva, vyuo hivi ni vya watu binafsi sheria haikukataza kuanzishwa popote ndani ya Zanzibar. Hivyo naomba kutoa wito kwa wenzetu walioko Mikoani wahamasike na wao waanzishe vyuo hivi ili kupunguza hiyo kadhia ya kuja mjini.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, hawa wanaosoma hawa udereva tunataka Mhe. Waziri atwambie wanaanzia miaka mingapi, kwa sababu tunakuta watoto wadogo wadogo wanaoendesha magari, sasa atwambia kuanzia miaka mingapi watoto kupewa magari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Kwa mujibu wa sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 imeeleza madaraja ya leseni kwa msingi huo, kuanzia umri wa miaka kumi na sita hadi umri wa miaka ishirini na tano ndipo panapomfumo wa watu wanaoendesha. Kwa mujibu wa daraja hizi kuna daraja (A) ambao ni vipando vya pikipiki, kuna daraja (B) ambayo ni gari ndogo, kuna (B1) gari za Tax, kuna (C) gari za mizigo chini ya tani tatu na nusu, kuna (C1) tani tatu na nusu, (C) ni zaidi ya tani tatu na nusu, kuna (D) na (D1) kuna (G) kuna (M).

Mhe. Spika, kwa mtu ambae atakuwa na umri wa miaka kumi na sita anaruhusika kuendesha piki piki, kwa mtu ambae atakuwa na umri wa miaka ishirini na moja anaruhusika kuendesha magari madogo madogo yasiyo magari ya abiria, ana umri wa miaka ishirini na tano akikubaliana na utaratibu wa sheria anaruhusika kuendesha gari ya abiria.

Mhe. Spika, inawezekana ikawa kuna mtu ana umri wa miaka ishirini na moja au ishirini na mbili huyo anaruhusika kuendesha gari lakini sio tu ile ya abiria.

Nam. 189

Kupanda kwa Bei za Bidhaa na Uwezo Mdogo wa Wananchi

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza:

Katika kukabiliana na kupanda kwa hali ya maisha na kupanda kwa bei za bidhaa, Serikali huchukua hatua ya kupandisha mshahara kwa wafanyakazi wake.

(a) Kwa mwaka ujao wa fedha 2011/2012 Serikali imewaongezea kiasi gani wafanyakazi wake.

(b) Nyongeza hizo zimewekwa kwa utaratibu gani ili kila mfanyakazi afaidike bila ya kuwepo tafauti kubwa baina ya wafanyakazi wa Serikali.

(c) Serikali imewafikiriaje walimu ambao ndio wenye maisha duni zaidi kutokana na maslahi madogo wanayopata.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora) - Alijibu:

Mhe.Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lako Nam. 189 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kukubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mjumbe kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huchukuwa hatua ya kupandisha mshahara kwa wafanyakazi wake kila baada ya muda hali ya kifedha inaporuhusu ili waweze kukabiliana na kupanda hali ya maisha.

(a) Kuhusu kima cha Mshahara ambacho Serikali itaongeza wafanyakazi wake katika mwaka wa fedha 2011/2012, kwa sasa haitakuwa vyema kukitaja naomba tukafanya ustahamilivu hadi wakati wa mjadala wa Bajeti ya Serikali na Bajeti ya Wizara yangu utakapoanza ambapo tutaweza kutaja kima cha mshahara ambacho Serikali inatarajia kuongeza kwa wafanyakazi wake.

(b) Serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kuongeza nyongeza za mshahara ili kila mfanyakazi afaidike na kuepusha mpishano mkubwa baina ya wafanyakazi wa Serikali. Aidha, utaratibu huu kuzingatia elimu pamoja na uzoefu wa muda wa utumishi wa kila mfanyakazi takriban Wizara zote zimekamilisha *scheme of service* zao na uzoefu wao kwa kila mfanyakazi.

(c) Katika mwezi wa April, 2010 Serikali imewafikiria walimu kwa kuwapangia mshahara kwa mujibu wa ujuzi na uzoefu wao kazini pamoja na kuwarejeshea asilimia 25% ya posho la ufundishaji ambalo lilikuwa limesita tangu 2007 wakati wa marekebisho ya mshahara. Hata hivyo, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Mwakilishi kuwa maisha duni si kwa mwalimu tu bali hata kwa wafanyakazi wa kada nyengine, sambamba na maelezo hayo, napenda kumuhakikishia kwamba Serikali imo katika kufanya jitihada ya kuyanyanyua mishahara ya wafanyakazi wote hivi sasa kutegemea na hali ya fedha na itakaporuhusu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Serikali imesema wazi wazi kwamba imeamua kurekebisha na kupitia mishahara ya watendaji wake wote na itazingatia vigezo vya muda pamoja na elimu, lakini zipo taarifa kwamba mishahara hiyo haikuhusishwa wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi.

a) Naomba kujua hilo ni kweli?
b) Kama ndivyo wafanyakazi hao hawakupewa watalipwa malimbikizo yao ya miezi mitatu ya *arrears*.
c) Kwa sababu wanaofanya vigezo hivyo ni wataalam wa Wizara ya Fedha na nchi hii ina wafanyakazi katika kila taasisi, huoni kwamba kuna kila dalili ya kujipendelea wale wafanyakazi ambao ndio wanaandaa ile nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Kwanza wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi hawamo kuna utaratibu maalum kwa wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi, wao wanafuata utaratibu gani.

Kuhusu wafanyakazi wengine walioko serikalini wana utaratibu gani wao wanazingatiwa kwa huo utaratibu uliopo hawatoachwa hilo namhakikishia Mhe. Hija Hassan Hija kwamba hawatoachwa, tutafuatilia na kusimamia katika hii faraja inayokuja.

Suali la lini wataanza kama ni mwezi wa October basi ni October tunasema tunaanza kulipa kuanzia tarehe Fulani, kwa hivyo hapo ndipo inapoanza nafikiri hiyo iko wazi kabisa.

Jibu la tatu Wizara ya Fedha na Uchumi kwamba labda maofisa wale ndio wanaopanga watapendelea, nataka nimfahamishe kwamba hii kazi siyo ya Wizara ya Fedha na Uchumi ni ya Wizara maalum ambayo serikali imeamua kuiunda haya mambo yote ya *scheme of service* na utumishi kwa ujumla huku ndio kwahali kwake, hii serikali imefanya kwa makusudi baada ya kuona kwamba kuna matatizo mengi sana ya utumishi yanakwama ndio maana ikaunda Wizara hii.

Wizara ya Fedha na Uchumi kazi yake ni kutoa fedha tu kwa hivyo Mhe. Hija Hassan Hija una maoni yoyote au mapendekezo yoyote tafadhali njoo tuonane tutarekebisha.

Nam. 95

SUZA Kutumia Udahili wa *TCU:*

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:

Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar *(SUZA*) kimejiunga na mfumo wa udahili kupitia *Tanzania Commission of University – TCU*.

(a) Je, Mhe Waziri huoni kwamba suala hili litapelekea kupunguza nafasi kwa Wazanzibari katika fani ya ualimu ambao kwa sasa wanaofundishwa kutoka Zanzibar ni asilimia 90%.

(b) Je, huoni kwamba mpango huo utaisababishia SUZA kuchukuwa wanafunzi wengi kutoka nje ya Zanzibar na ambao wakimaliza hawatoinufaisha Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Spika , kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake Namba 95 lenye sehemu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Mhe.Spika, mfumo wa udahili unaotumiwa na Tanzania *Commission for Universities* unaoitwa " *Central Admission System* " *(CAS)* ni mfumo ambao unawadahili waombaji wote wanaotaka kwenda kusoma Vyuo Vikuu vya Tanzania kupitia mfumo mmoja.

Mfumo huu umesaidia sana katika kuwatambua waombaji wenye kutumia vyeti vya kughushi na kuwapatia nafasi za kujiunga na vyuo waombaji wenye sifa zilikubaliwa. Pia mfumo huo huwapanga waombaji katika chuo kimoja tu badala ya utaratibu wa mwombaji kuwasilisha maombi yake moja kwa moja vyuoni ambapo mwombaji anaweza kukubaliwa na zaidi ya Chuo Kikuu kimoja.

Utaratibu huu umesaidia katika kupunguza usumbufu kwa Vyuo Vikuu kwa sababu mwombaji anakubaliwa kujiunga na Chuo Kikuu kimoja tu. Utaratibu huu wa udahili unatumika kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo Vikuu moja kwa moja kutoka Skuli za Sekondari na huwahusu waombaji wanaojiunga na vyuo Vikuu kutoka Makazini.

Ni kweli kuwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilijiunga na Mfumo wa udahili wa Wanafunzi kupitia " *Central Admission System* " kwa majaribio .

Mfumo huu umesaidia Chuo Kikuu cha Taifa kupata wanafunzi wengi zaidi kutoka sehemu tofauti kwani tokea kujiunga na mfumo huu miaka miwili iliyopita idadi ya wanafunzi imeongezeka sana. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a). Utaratibu huu haupunguzi nafasi za wanafunzi wa Zanzibar kujiunga na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar pindipo kama wanatimiza sifa za Kielimu na wameainisha kutaka kujiunga nma chuo hicho katika fomu zao za maombi. Utaratibu huu pia unatumika katika kuwadahili wanafunzi kutoka Zanzibar wanaojiunga na vyuo Vikuu mbali mbali vilivyoko Tanzania bara kikiwemo Chuo Kiikuu cha Dar es Salaam. Utaratibu huu umesaidia sana katika kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaotoka katika Skuli za Sekondari za Tanzania bara kujiunga na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar jambo ambalo limesaidia sana kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi katika Chuo Kikuu chetu na kuongezeka kwa mapato ya Chuo ambayo yamesaidia katika shughuli za uendeshaji.

b). Kama nilivyotangulia kusema utaratibu huu unatokana nafasi sawa kwa waombaji wote wenye sifa za Kielimu kuchaguliwa kujiunga na Chuo bila ya upendeleo. Kwa vile udahili wa Wanafunzi kwa kutumia mfumo wa CAS ni wa hiari. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar , kiliamua kujitoa rasmi katika mfumo huu kuanzia tarehe 23 Machi 2011. Hivyo waombaji wote wanaotaka kujiunga na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuanzia mwaka huu wamepitisha maombi yao moja kwa moja Chuoni badala ya kupitia kwa CAS. Hata hivyo napenda ieleweke kuwa pamoja na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kujitoa katika utaratibu huu, kigezo cha sifa za Kielimu kitaendelea kutumika katika udahili wa wanafunzi wanaojinga na chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar bila ya kuwepo upendeleo wa aina yoyote.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri wanafunzi pindi tu wakimaliza elimu zao katika chuo kikuu cha Taifa SUZA.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Pamoja na matatizo yote tuliyokuwa nayo ya kuajiri lakini wao wanapata upendeleo wa kwanza kwa hivyo tunaendelea na utaratibu huo kila anayemaliza Chuo Kikuu kwa shahata ya kwanza au ya pili tutawaajiri kwa sababu tunawahitaji katika fani maalum.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali mola la nyongeza kama ifutavyo. Kwa kuwa tunaingia katika jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kuwa vyuo vyetu vinaanza sasa na vinaanza kujitoa katika jumuiya kama *TCU* kuna athari gani SUZA ilivyojitoa katika *TCU* na ushirikiano na vyuo vyengine.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Kama nilivyosema katika suala langu mama kwamba suala la kujiunga kwa utaratibu wa kasi ni wa hiyari, na kwa sababu hata ukijitoa katika utaratibu huu hakuna kitu ambacho utakikosa na vile vile kwa sababu chuo chetu cha SUZA kina sifa zinazotambuliwa kwa hivyo bado ni sawa sawa na Vyuo vikuu vyengine.

Nam. 108

Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar Kutambuliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar mwaka 2010 na miongoni mwa mambo muhimu yaliyoingizwa ni kitambua Zanzibar kuwa ni nchi moja miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungao wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna busara gani iliyotumika ya kufanya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar na zaidi ya yale yanayohitaji marekebisho ya Katiba kabla Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanyiwa marekebisho hayo.

(b) Je, ni lazima Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iyatambue marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar na kuna athari gani iwapo Bunge halitayatambua marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Marekebisho ya 10 yalifanywa kwa kuzingatia mabadiliko ya mfumo wa Serikali na uendeshaji wake. Fursa hiyo ilitumika pia kufanya marekebisho ya kasoro zilizokuwepo katika Katiba yetu kwa kuzingatia kuimarika kwa utawala bora na haki za raia.

Mhe. Spika, Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar hayakuwa na nia ya kufuta au kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano bali marekebisho hayo yamedhihirisha tu kuwa Katiba hiyo ya Muungano ina kasoro kadhaa za msingi ambazo zinahitaji marekebisho. Miongoni mwa eneo lenye kasoro ni lile linalohusu masuala ya Muungano na hasa uhusiano wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Spika**,** mfano mzuri wa kasoro hizo ni lile la kutoeleza hadhi ya Zanzibar ndani ya Muungano wakati takribani nchi zote zenye Muungano zinaeleza hadhi ya Washirika wa Muungano ndani ya Muungano huo.

Mhe. Spika, mfano wa pili ni ule wa Katiba ya Muungano na hata Katiba ya Zanzibar kabla ya Marekebisho ya 10 kutaka Rais wa Zanzibar ashauriane na Rais wa Muungano katika kuigawa Zanzibar katika Mikoa na katika uteuzi wa wakuu wa Mikoa. Ni dhahiri kuwa sharti hili linapingana na Katiba yenyewe ya Muungano kwa vile Tawala za Mikoa na uteuzi wenyewe wa Wakuu wa Mikoa si suala la Muungano. Pili sharti hilo lilitokana na historia ya mfumo wa chama kimoja ambapo Katibu wa Mkoa wa Chama alikuwa pia ndiye Mkuu wa Mkoa. Mfumo huo uliwekwa bayana ndani ya Katiba, chini ya kifungu cha 17 cha Katiba ya Zanzibar ya 1979 ambacho kilieleza:-

“Mtu yeyote aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Chama kuwa Katibu wa Chama wa Mkoa chini ya kifungu cha 56(1) cha Katiba ya Chama atakuwa vile vile Mkuu wa Mkoa huo katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar”

Aidha ugawaji wa Mikoa masharti yake yalielezwa chini ya kifungu cha 2(2) cha Katiba hiyo ambayo kilimpa Mamlaka Rais wa Zanzibar kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa au kukubaliwa na Chama husika kwa wakati huo.

Mhe. Spika, kwa sababu nilizozieleza hapo juu ni wazi kuwa suala hilo lilikuwa la kisiasa kwa kufuata mfumo wa Chama uliokuwepo na kamwe si suala wala halijawahi kuwa suala la Muungano.

Mhe. Spika, kasoro hiyo iliwahi kuondolewa kufuatia marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya 1979 yaliyofanywa na Sheria Nam. 9 ya 1982 kwa kurekebisha kifungu cha 17 cha Katiba hiyo. Hata hivyo, kwa

bahati mbaya wakati wa kutunga Katiba ya Zanzibar ya 1984, marekebisho hayo hayakuzingatiwa.

Mhe. Spika, kwa sababu nilizozieleza hapo awali, marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar yalikuwa ndani ya Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi na hayakuhitaji ridhaa, idhini wala Baraka ya chombo chochote nje ya Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar hazijaweka sharti la marekebisho ya Katiba au Sheria yoyote yaliyo chini ya Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi kutambuliwa kwanza na Bunge ndipo yawe na nguvu za kisheria. Hivyo si lazima marekebisho ya 10 kutambuliwa na Bunge bali ni wajibu wa Bunge, Wabunge na raia wa Jamhuri ya Muungano kuheshimu Katiba ya Zanzibar na kuilinda kwa vile ni moja ya nguzo za Muungano wetu, na kwamba ni Nchi ambayo iliungana na Nchi nyengine kufanya Jamhuri ya Muungano. Aidha, ni wajibu wa Bunge kufanya marekebisho ya Katiba ya Muungano ambayo ni wazi kuwa ina kasoro kadhaa zinazohitaji kusawazishwa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali lifuatalo.

Kwa kuwa Zanzibar hivi sas imefanya marekebisho yake ya 10 katika mwaka 2010 na tunategemea Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya marekebisho ya Katiba yake karibuni.

Je, Mhe. Waziri kuna athari gani za kisheria hapa endapo yale marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar hayatozingatiwa katika mchakato mzima wa kutengeneza katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu lielewe kwamba Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni Katiba mbili zilizo sawa sawa. Haihitaji kwamba katiba ya Jamhuri ya iitambue katika ya Zanzibar. Kwa sababu katika ya Zanzibar ni ya nchi ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni Katiba ya inayohusiana na Muungano ya nchi mbili.

Kwa hivyo hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano haitozingatia matatizo yale ambayo yamo katika Katiba ya Zanzibar bado katiba ya Zanzibar itakuwa ni Katiba sahihi na itakuwa ni Katiba yenye nguvu kwa upande wa Zanzibar. Kitakachodhihirika hapa ni kwamba bado kutakuwa na mizozo na migogoro

baina ya Katiba hizi mbili ambazo lazima tuyatatue. Hayo yatakuwa ni katika masuala ya kero za Muungano ambayo ndio madhumuni hasa ya kufanya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili kero hizi za muungano ziweze kuondoka.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja kama ifuatavyo. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano juu ya madaraka ya kutunga sheria ya Bunge ibara ya 64(5) naomba kunukuu.

> "Bila ya kuathiri kutumika kwa Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii kuhusu mambo yote ya Tanzania Zanzibar yasiyo mambo ya Muungano, Katiba hii itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano na endapo sheria nyengine yoyote itakayokiuka masharti yaliyokuwemo katika Katiba hii, Katiba ndiyo itakayokuwa na nguvu na sheria hiyo nyengine kwa kiasi inachokiuka Katiba itakuwa ni batili"

Swali langu liko hapa Mhe. Spika, je, kifungu hiki Mhe. Waziri kinakusudia nini?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza nina furaha kwamba hiki kifungu amekisoma na Katiba anayo. Katiba inasema kwamba bila ya kuathiri kutumika kwa Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii kuhusu mambo yote ya Tanzania, yasiyo mambo ya Muungano. Kwa hiyo hapa ni kwamba yale mambo ambayo sio ya muungano, mambo ambayo ya muungano ndio Katiba ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na nguvu lakini mambo si ya muungano Katiba haina nguvu kwa Zanzibar. Kwa sababu Zanzibar ni nchi peke yake na inaendeshwa na Katiba yake ya Zanzibar.

Nam. 49

Kupandishwa Kwa Bei ya Umeme, Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:

Hivi karibuni, '*TANESCO'* imetoa mapendekezo kwa '*EWURA'* ya kupandisha bei ya umeme kwa zaidi ya asilimia 35 (35%), lakini kutokana na sababu za msingi *EWURA* imetoa idhini kwa *TANESCO* ya kupandisha bei hiyo kwa asilimia 18.5 (18.5%) tu. Hata hivyo, imeongeza hofu na wasi wasi mkubwa kwa watumiaji na zaidi hofu ya kupanda kwa gharama za maisha.

(a) Kwa kuwa bei ya umeme ilipopandishwa kwa asilimia 169 (169%) ilileta matatizo makubwa kwa Zanzibar, Je. Mhe. Waziri kutokana na bei hi mpya ya *EWURA*, watumiaji umeme wa Zanzibar wataathirika vipi.

(b) Ili kujiepusha na matatizo haya ya kupandishwa kwa bei ya umeme kunakoiathiri sana Zanzibar, Wizara haioni haja ya kutafuta chanzo chengine cha nishati ya umeme kwa lengo la kuinasua Zanzibar ya kubebeshwa gharama kubwa za umeme.

(c) Kwa kuwa Zanzibar nimteja mkubwa wa *TANESCO* na kwa kuwa suala la ushirikishwaji katika maamuzi ya kupandishwa kwa bei ya umeme kuna umuhimu wake. Je, Zanzibar inashirikishwaje katika maamuzi hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 49 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kama ongezeko la asilimia 168 la bei ya umeme lingekubaliwa na *ZECO*, athari yake kwamba mtumiaji wa umeme wa Zanzibar angelazimika kulipia umeme kwa Shs. 240 kwa uniti moja badala ya shs. 120 kwa uniti
zinazolipwa sasa.

(b) Mhe. Spika, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kuwa Wizara yangu imeweka msisitizo wa kutaka iheshimiwe kwa mkataba wa kuuziana umeme baina ya TANESCO na *ZECO (PPA*) ambao ndio ulioweka vigezo vya kuuzia umeme, kuwa na umeme mbadala haitopelekea kuwa na umeme wa bei nafuu kwa muda mchache.

(c) Mhe. Spika, kutokana na Sheria zilizopo Tanzania Bara maamuzi ya kupandishwa kwa bei za umeme ni lazima yaidhinishwe na Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji *(EWURA).*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika kutatua tatizo la umeme Zanzibar, serikali imeamua kuchukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kulaza umeme mwengine kutoka Ras Kilomoni hadi Fumba, lakini pia imeamua kwa msaada wa nchi wafadhili kuangalia

vianzio vyengine vya umeme kama vile upepo na jua, lakini hasa katika maeneo ya Unguja. Kwa kuwa Zanzibar ni Unguja na Pemba. Na kwa kuwa tunategemea umeme huko huko kutoka Tanzania Bara.

Je, vyanzo hivi mbadala kwa nini vibakie Unguja tu na visipelekwe na kule Pemba ili kutatua suala zima la umeme katika visiwa vyetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kufahamu kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inalengo la kuondoa tatizo la umeme Zanzibar.

Isitoshe kuhusu suala la tatizo la umeme Pemba nahisi kwamba suala hili sasa hivi lipo katika hatua nzuri baada ya kuweka laini zetu kutoka Tanga kuja Pemba, kwa hiyo watumiaji wa umeme wa Pemba wanapata umeme wa kutosha kabisa. Kuhusu Unguja tunategemea kipindi kijacho cha mwaka wa 2012 mwanzoni mwa mwaka huu tutaweka laini mpya na kuliondoa tatizo hili la umeme Zanzibar.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza zaidi.

Mhe. Spika, waswahili wana misemo mingi ya Kiswahili ambayo kwetu ni fundisho. Kuna msemo wa kwanza wa Kiswahili unasema **"**Mtumaini cha ndugu hufa masikini". Kuna muimbaji mwengine alisema "Babu mkongwe miujiza wachakuwa chanja huliweza, wachukua gogo wajilemeza"

Mhe. Spika, maana yake kusema msemo huu ni ukweli usiofichika kwamba sasa hivi wananchi wa Pemba wanaumeme kutoka Tanga na tunafaidika sana. Lakini kwa sababu ya kusema misemo hiyo ni kwamba hivi sasa kuna tatizo ya kupandishiwa bei ya umeme iliyokithiri Zanzibar, ni ndugu zetu ambao kila jitihada zinafanywa kuitoa bei ile ya kupandisha kiholela hawakubali. Sasa tunaunga tena umeme mwengine kutoka Dar-es-Salaam kuja tena Zanzibar. Hivi sasa anatwambia kwamba Pemba katika Umeme huu wa mbadala hautowekwa kwa sababu tunapata umeme kutoka Tanga.

Je, endapo wale ndugu zetu kutokana na hili deni tulilonalo wakitukatia umeme tutaelekea wapi. Naomba majibu kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza katika jibu mama nimesema kwamba ongezeko la kupandishwa bei ya umeme Zanzibar hatukulikubali au hatujakubaliana nalo.

Mhe. Spika, katika kulifuatilia suala hili mimi mwenyewe tarehe 26 mwezi wa 5 nilitembelea katika kituo cha umeme Ubungo na nikakaa na Bodi ya Wakurugenzi kwa kulizungumzia suala hili. Makubaliano ni kwamba Shirika la Umeme Tanzania *TANESCO* litaonana na Shirika la Umeme Zanzibar *ZECO* pamoja na Eura kulijadili suala hili na kulipatia ufumbuzi utakaofaa. Katika ufumbuzi utakaopatikana katika mjadala huo ni kwamba kupunguzwa kwa bei ya umeme si kupandishwa kwa bei ya Umeme. Hili likimalizika basi *Inshallah* nategemea tutakuwa katika hali nzuri bila ya mvutano wa *ZEC* pamoja na *TANESCO*.

Nam. 37

Matunzo ya Madaktari Wanaorudi Kutoa Huduma Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kuna madaktari wazalendo wa Zanzibar ambao walikuwa wanafanya kazi nje ya nchi na kuamua kurudi kwa lengo la kusaidia katika kuimarisha huduma za afya hapa nyumbani.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuwaenzi wataalamu wetu hao wazalendo.

(b) Je, Serikali inajua matatizo ya kiutendaji ambayo madaktari hawa wanayo hivi sasa hapa nyumbani.

(c) Je, Serikali ipo tayari kuwasikiliza na kuwasaida kwa lengo la kuhakikisha kuwa majukumu yao yanatekelezeka vyema.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 37 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo kuhusiana na uzalendo aliouzungumzia Mhe. Mwakilishi. Daktari mzalendo ni yule ambaye amehitimu masomo yake na kurudi kuendelea kufanya kazi katika nchi yetu na kustahamili matatizo na mazingira magumu yaliopo hapa kwetu.

(a) Serikali tayari ina mpango wa kuboresha maslahi ya madaktari wote pamoja na kada nyengine za afya ili wale waliopo waendelee kubaki na wale walioko nje ya nchi yetu waweze kurudi na kuja kushirikiana na wenzao katika kutoa huduma kwa wananchi.

(b) Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mwakilishi kwamba serikali inayajua matatizo yote ya kiutendaji ambayo madaktari wetu wanakabiliana nayo, likiwemo la mishahara midogo, ukosefu wa vitendea kazi, usafiri, sare, nyumba za kuishi pamoja na marupurupu mengine.

(c) Serikali siku zote imekuwa ikiwasikiliza wafanyakazi wake wakiwemo madaktari. Aidha utatuzi wa baadhi ya matatizo unashindikana kutekelezwa kwa wakati kutokana na ufinyu wa "budget" uliosababishwa na hali ya uchumi wa nchi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa muhimu wa suali hili tulikuwa tunatarajia tusikie yale majibu lakini hatukusikia lolote isipokuwa manunguniko. Kwa hivyo tunaomba lielezwe vizuri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa sauti yako inasemekana haisikiki vizuri, wajumbe wanalalamika kwamba hawasikii vyema.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, leo asubuhi nimepata taarifa kwamba Bara letu la Afrika linapoteza madaktari zaidi ya 78,000 kwa mwaka kwenda ng'ambo kwa ajili ya kufanya kazi na kufata maslahi bora zaidi.

(a) Naomba nimuulize Mhe. Waziri hapa Zanzibar sasa hivi tuna madaktari wangapi na kila daktari mmoja anawahudumia wagonjwa wangapi.

(b) Katika mkumbo huo wa madaktari wanaokilimbilia ng'ambo Zanzibar huwa tunachangia madaktari wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hiyo taarifa imetoka leo asubuhi kama unavyosema. Madaktari wa Unguja hawakuanza kuondoka leo, wapo wengi waliondoka na wengine hata kurudi hawarudi. Madaktari wetu wapo karibu kila idara, inategemea ma fild iliyopo. Hata hivyo sio wengi wa kutosha.

Kwa mfano Idara ya Wanawake Uzazi tuna madaktari kama wanne. Tukenda kwenye Idara ya Upasuaji kuna madaktari pia wanne wawili ni madaktari na

wawili ni wasaidizi wa madaktari. Ukienda kwenye sehemu ya matibabu ya kawaida inategemea seksheni waliopo, kuna madaktari wanaofikia wanane lakini wapo katika *field* tofauti, kwenye masikio, kisukari na wale ambao wanatibu maradhi ya kawaida na wengineo wasaidizi wa madaktari. Hao ndio madaktari tulionao katika hospitali ya mnazi mmoja. Kuna madaktari wengine katika hospitali tofauti za Chake-Chake kama sikusei kuna madaktari watatu, Wete kuna daktari mmoja, Kivunge, Makunduchi sehemu zilizobakia zinawasaidizi madaktari. Hao ndio madaktari tulionao.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa kutoa maelezo ya ziada kuhusu idadi ya madaktari.

Mhe. Mwakilishi amesema kwamba kuna matatizo kama kiasi madaktari 78,000 wanatoka nchi za Afrika kwenda Ulaya kama nimesikia vizuri. Hilo ni suala la kawaida si Afrika tu, dunia nzima kuna tabia hiyo ya madaktari kuondoka nchini kwao kufuata maslahi mazuri. Hata huko Uingereza moja katika watu wenye matatizo ya kupata manasi. Matokeo yake manasi ya nchi za Afrika wanakwenda huko wanaajiri wa bei kubwa sana. Hata hapa Zanzibar kwa sababu ya maslahi wengine huwa wanakwenda Tanzania Bara kufuata maslahi.

Mhe. Naibu wangu amesema kuna tatizo la suala la uzalendo. Wale madaktari tulionao hapa kwa mujibu wa suala alilouliza amesema madaktari lakini mwenzangu amesema kuna. madaktari *specialist* na kuna madaktari wasaidizi. Sasa kama wote hao ni madaktari suala alilioliuliza hatuwezi kumpa kwa pamoja hivi sasa tutalieleza kwa maandishi kumueleza ufafanuzi zaidi.

Pili kwa miaka kumi iliyopita tumepoteza madaktari 19 waliondoka kwenda nchi mbali mbali na tumepoteza manasi 63. Sasa wanapotaka kurudi hatuwezi kuwapa maslahi bora kuliko wale waliokaa hapa miaka kumi wakapata tabu hapa. Hasa kwa sababu na wao ni Wazanzibari.

Madaktari wanaopewa maslahi tofauti ni wale tunaokubaliana kwa kuwaazima kutoka nchi za nje kama vile Misri, Uingereza au China hao huwa wanakuja kwa masharti maalum. Kwa hivyo, anapokuja Mzanzibari aloshindwa kustahamili au aliyepatwa na matatizo akaenda nje anapoamua kurudi huwa tunashukuru kama karudi, lakini huwa amerudi kwao. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu swali la msingi alitoa takwimu ya madaktari waliopo hapa Unguja. Mhe. Spika, kwa mahesabu ya haraka haraka inaonekana ni madaktari

zaidi ya 12 wapo hapa Unguja, lakini Pemba alitaja kuna 2 wako Chake-Chake na kuna1 yuko Wete na Mkoani sijui ni 1. Lakini baada ya utafiti wa kina inaonekana pale Mkoani ukiacha wale madaktari wa Kichina ni *Assistance Medical Officer* mmoja ambaye ndiye daktari dhamana wa ile Hospitali ya Mkoani na wakati Machina takriban wameshamaliza muda wao na wanaondoka. Vile vile katika Hospitali ya Chake-Chake kuna *Assistance Medical Officer* sijui huyu wa Wete kama ni daktari au vipi.

a) Je, daktari mmoja anatakiwa ahudumie wagonjwa wangapi.
b) Je, isingekuwa vyema kwa hawa madaktari waliopo Unguja wakafanya maarifa ya kupelekwa kule Pemba ili kusaidia angalau pale Mkoani kwa sababu wale madaktari wa Kichina wameshamaliza muda wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tukichukua *ratio* ya daktari mmoja ni kwamba tunazungumza daktari naomba mnielewe, tunapozungumza daktari ni yule aliyesoma kwa miaka 5-7 hao wengine wote hao ni wasaidizi tu. Kwa hivyo, ukitaka kuchukua *ratio* yake kwa siku anatakiwa angalau kama unataka mgonjwa atizamwe vizuri basi wasizidi wagonjwa 20. Kwa hivyo, fanya 20 mara 360 utapata kwa mwaka anahitaji kuona wagonjwa wangapi.

Mhe. Spika, pia amezungumzia suala la madaktari katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee. Mhe. Spika, Hospitali ya Abdalla Mzee kuna timu tosha ya madaktari wa Kichina ambayo ina kila mtaalamu na kila fani, na daktari mzalendo anakuwepo pale kwa sababu ya kusimamia wale waliopo kwani hawawezi wakakaa wageni bila ya kuwa na wenyeji. Pia Hospitali ya Mnazi Mmoja ukumbuke kwamba ni ya rufaa, kwa hiyo wataalamu wazalendo wengi watatakiwa wawepo pale ili hao wengine wanaotoka sehemu nyengine wakija pale wakutane na madaktari wanaostahiki.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011-2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na mijadala wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar leo tumebahatika kuwa na wageni ambao ni vijana wenu Waheshimiwa Wajumbe wapo wanafunzi 29 pamoja na mwalimu wao kutoka Skuli ya Mwembeladu naomba wasimame ili kuwasalimia Wajumbe. Hawa wamekuja kuona wazee wao shughuli wanazofanya katika kupitisha Bajeti ya Serikali. Karibuni sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha tukafika hapa wote tukiwa tuko katika hali ya usalama. Pia nakushukuru na wewe kuwa na afya njema ukaweza kuendelea katika kikao chetu hiki.

Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote katika hotuba yake ya bajeti aliyotusomea hapo juzi. Mhe. Spika, kitabu hiki kina malengo makuu yanayofuata katika ustawi wa nchi hii, mimi nawapongeza sana watendaji wa fedha na uchumi. Vile vile nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwani bajeti yetu ya mwaka huu imepangika na kueleza mambo yote yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, mimi nitaanzia kuhusu vijana, wanawake na watoto. Hapa katika vijana, wanawake na watoto ni kwamba tuna matatizo makubwa yaliyotukumba katika nchi. Mhe. Spika, nchi yetu tunaifanya ni njema atakae aje na tayari watu wanakuja.

Mhe. Spika, watoto wetu siku hizi wanapotea hivyo naieleza serikali ijue kuwa tuna matatizo ya kupotea kwa watoto wetu. Mhe. Spika, ni mzazi gani awezae kustahamili watoto wawili au watatu kwa siku moja ukiambiwa wamepotea na tena huwa hawarudi tena. Hivyo, mtoto azaliwe Mji Mkongwe afike miaka 15 au miaka 6 au 7 ndio kweli atoke asijue kurudi kwao, lakini ni kwamba kuna watu wapo hapa wanatufanyia udhalilishaji wa kuwakimbiza watoto wetu jinsi ya kutudhalilisha watu wa kisiwa cha Zanzibar.

Mhe. Spika, ni kwamba vijana wetu tunaiomba serikali iwatizame sana kwani kundi la vijana ndio kundi mahususi litakalokuja kutujadili badala ya hatima zetu sisi. Mhe. Spika, siku hizi watoto wanaingia katika makundi mbali mbali kama vile ya ulevi, wizi, ubakaji na kila kitu. Hivyo, tunaiomba serikali iyaone mambo haya ili waweze kuwaondoa watoto hawa ili wasiwe tegemezi na wale waliokuwa tayari wameshaweza kufanya kazi basi waziri wetu awezeshwe kuwadhibiti watoto hawa na kuweza kuwapa misaada mbali mbali ili kujua hatima zao za baadaye. .

Mhe. Spika, kitabu hiki kinatueleza kuhusu ukulima ni kwamba Chuo cha Kilimo pamoja na hawa watu wa ufiti watakaopewa kazi hii tunaomba waweze kufika katika vijiji ili waweze kutoa taaluma.

Kwanza tunataka tujue hii mbegu inayoweza kustahamili ukame na kuweza kupata mazao kuondoa umasikini katika nchi yetu, ni kwamba kuna udhalilishaji mkubwa sana sasa hivi wa kuweza kupanda vipando vikifika kati kati vipando hivi vikatoweka bila ya mavuno. Kwa mfano, Mheshimiwa tukija katika kilimo cha mpunga tunaambiwa kuna mbegu nzuri inayoitwa “nerika”.

Mhe. Spika, kwanza tunataka tujue tutaweza kupata wapi mbegu hii na itatosheleza Zanzibar mbegu hii kwa wananchi wote na tujue tukiitaka twende kwa nani ili tuweze kukidhi mahitaji yetu.

Mhe. Spika, zamani tukilima mbegu zetu za kutegemea mvua na tukivuna, lakini kwa sasa hivi haikubali tena na tunafikiria kuwa ardhi imechoka. Kwa hivyo, hawa watafiti katika Chuo cha Kilimo ni kuwa wafanye utafiti kuanzia mbegu mpaka ardhi wenyewe na kujua kitu gani kinaturejesha nyuma katika kilimo chetu.

Mhe. Spika, kitabu hiki hapa kina mbegu za muhogo, mbegu hizi wakulima wengi wanangukia katika kulima kilimo cha muhogo, lakini hizi mbegu kuna zile zinazoanzia miezi 3 mpaka miezi 6. Lakini nasema mbegu hizi zitakuwa hazikidhi haja kwa sababu muhogo utakaoupanda wa miezi 3 na miezi 6 ikiwa hujautumia muhogo huu ndio unaoharibika ikawa hauliki. Kwa hivyo, tunaomba mbegu hizi tukishafanyiwa utafiti basi tuweze kupata na mbegu zitakazokidhi kujivuta mpaka miezi 9.

Mhe. Spika, vile vile nije na hawa wanawake watakaofanyiwa vikundi katika utafiti wa mazao. Mhe. Spika, kweli tulikwenda katika ziara yetu tukakiona kituo kinachojengwa Skuli ya Kizimbani. Tunaiomba wizara inayohusika pamoja na bajeti ya serikali itakapokamilika watu hawa waweze kushajiishwa vikundi mbali mbali kuanzia vijana, wanawake na wanaojiweza. Hata hivyo, kupatiwa ajira kwenye kiwanda kile na ule utafiti na wao wawepo wakati wanapofanyiwa utafiti wa mazao yao watakayokwenda kuuza pale kujipatia ili kujiondolea matatizo yanayowakumba siku hadi siku.

Mhe. Spika, halafu matatizo ya mazingira mama yangu hapa jana alisema, mazingira yana upeo mpana sana. Mimi naiambia serikali bila ya kujipanga na kuwa na umadhubuti mzuri sana na ikaweka pahala pazuri watu wakaweza kwenda kuchimba mchanga. Mhe. Spika, ni kwamba uchimbaji wa mchanga utaathiri nchi hii.

Mhe. Spika, kila unapopita unakuta madimbwi na mashimo makubwa sana yanayochimbwa mchanga hujui penye mji wala hujui vijijini, wewe unaona tu mashaka yanaingia. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri hili serikali ilione kwa sababu sasa hivi tuna wimbi kubwa sana la mashimo makubwa sana katika nchi hii, hivyo serikali iweze kuweka mahala maalum watu waweze kuingia kwa kibali na sheria zitakazopangwa ili waweze kwenda kuchukua mchanga wasijichimbie tu mchanga kiholela.

Mhe. Spika, hapa tulipomaliza Baraza letu lilopita hapa sisi tuliomba kujengewa mabwawa yakuweza kuzalisha maji ya mvua. Mimi nataka nijue

serikali imefikia wapi, kwa sababu sasa hivi maji hayatoshi, maji yaliokuwepo yanamwagiwa kwenye kilimo, maji hayo hayo tunataka tutumie, humo tunamokaa maji ni matatizo. Kwa hivyo, tunataka tujue uvunaji wa maji ya mvua umefikilia wapi au ndio basi?

Mhe. Spika, tukija katika zao la nchi sarafu ya hapa ni karafuu, lakini mikarafuu inakufa siku hadi siku na hatujapata kitu mbadala cha kuweza kukidhi haja ya mikarafuu. Mhe. Spika, kuhusu mikarafuu tuweze kupewa nyenzo kwa sababu tunakwenda pale tunapewa mikarafuu kuinunua ukenda kuipanda mia basi unapona mmoja. Mhe. Spika, mimi nawaomba watafiti wafanye kazi zao na kuweza kuteremka kwa wakulima ili waweze kuwashajiisha kupanda zao la mikarafuu ili tuweze kuibuka na wimbi la umasikini.

Mhe. Spika, sisi tunasikitika sana minazi yetu inatoweka tunanunua nazi kutoka Tanga moja ni shilingi elfu moja. Hivyo jamani nchi hii nazi zilizokuwepo zimekwenda wapi mpaka tusipate nazi, ni kuwa minazi inakatwa ovyo ovyo ikipasuliwa mbao. Mimi naiomba serikali wale wote walioekeza viwanda vya kupasua mbao za minazi iwe ni marufuku, isipokuwa kilimo wenyewe wende ikiwa minazi imeshachoka ndio waweze kusema huu uondolewe na huu uondolewe kwa kibali maalum na hapo ukishang'olewa ukapandwe mwengine. Mhe. Spika, huo ni mtihani tena Unguja na Pemba minazi inahama tena kwa kasi zaidi.

Mhe. Spika, mimi nasikitika sana bajeti yetu imejikunjua kikweli kweli wala hatutaki tuichangie sana sisi tunataka tumboreshe tu Mhe. Waziri na kumpongeza tunangoja hivyo vitabu kimoja kimoja, isipokuwa tunatoa yale maelezo yetu ajue kuwa hapa hiki kitabu na sisi tunacho.

Mhe. Spika, tukija katika mafuta tulipitisha katika Baraza letu hivyo tunasema tena tusiwe tegemezi mafuta ya nchi hii Mhe. Waziri usimame kidete kwani ndio yatakayotuinua sisi kiuchumi. Mhe. Spika, tunaomba tutetewe kwanza tunasema mapato ya ndani ya Zanzibar wakusanye wenyewe Wazanzibari, umasikini huu unaotukumba ni kwamba fedha yote inayokusanywa hatujui inakwenda wapi.

Mhe. Spika, mimi siamini kuambiwa inaingia kwenye benki hii ikisha ikaingia benki hii halafu ikatoka tukaletewa sisi, mimi siamini lazima pesa itakapoingia itakuwa na mchujo. Mhe. Spika, ni vizuri haya mapato ya ndani tuyakusanye wenyewe ili tuweze kukidhi haja katika serikali yetu.

Mhe. Spika, halafu nasikitika sana kitabu nimekisoma mna, vijana mna watoto na sekta mbali mbali. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametusahau walemavu kwani

ni watu wa nchi hii lakini humu naona sijawaona . Kwa hivyo, tunaomba walemavu wana mambo kamili kama watu wengine tunataka elimu, afya na mambo mengine lakini Mhe. Waziri ametusahau tunaomba serikali ituone sisi kwani tuna udhalilishaji mkubwa sana.

Mhe. Spika, la mwisho ninalolisisitiza mimi nasema katika Baraza hili tumesimama hapa kuweza kuchangia kitabu hiki, lakini nawaomba wenzangu bajeti hii ni bajeti ya wananchi wa Zanzibar basi tuweze kuichangia na kuweza kuipitisha. Mhe. Spika, na wenzetu wote watakaopitisha bajeti zao basi tuweze kuwachangia na kuwaboresha.

Mhe. Spika, badala ya hayo mimi nakushukuru sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi hii yakuweza kueleza machache na kutia nyalio katika Bajeti ya Serikali kwa sababu mengi yamesemwa na sisi tunaendelea kutia nyalio.

Mhe. Spika, mimi kwanza nianze sekta ya elimu kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kuweza kutuletea bajeti hii ambapo kweli wamejitahidi. Mhe. Spika, mimi namfahamu Mhe. Waziri ni mtu mwenye uweze na Katibu Mkuu wake wamejitahidi kututayarishia kitu kizuri. Aidha, nataka nimpongeze tena Waziri kwa lugha ambayo ameiwasilisha hapa hata sisi ambao hatujui lolote kuhusu uchumi basi tumefahamu sana. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze katika kitabu hiki kwenye ukurasa wa 34 Mhe. Waziri amezungumzia changamoto ambazo wamezipata katika kutayarisha MKUZA hapo katika Sekta ya Elimu kwamba ni pamoja na lugha ya Kiingereza ni tatizo kwa wanafunzi wetu pamoja na walimu.

Mhe. Spika, hili nashukuru kwamba walimu karibu 700 wanaendelea kuwapa mafunzo ya lugha za Kiingereza, aidha tunaishukuru serikali kwamba wana mpango maalum wa kuwashajiisha wanafunzi wa kike ili waweze kupenda masomo haya ya sayansi na hesabati. Mhe. Spika, jambo hili vile vile nadhani ni mkakati mzuri wa serikali, lakini uutekeleze kwa matendo kwa sababu maneno huwa ni mazuri lakini mara nyingi huwa tunafeli katika matendo. Mhe. Spika, siku zote lazima serikali wajue kwamba kuna uhondo kuyataka matendo, wasipofanya matendo siku zote tutaendelea kula uvundo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika sekta hii ya elimu na kuwashajiisha wanafunzi wa kike mimi nadhani wangelikwenda katika ziara nadhani pamoja na kujenga hizi skuli kumi na tano ambazo ametueleza Mhe. Waziri pamoja na kupatiwa mafunzo ya walimu, kuwashajiisha wanafunzi kupenda sayansi, nadhani

wangefanya kitu cha ziada. Mhe. Spika, masomo ya sayansi sasa hivi kwa hapa Zanzibar wanafunzi wengi hawayapendi na hususan hawa wasichana. Mimi nafikiri tungefanya kitu cha ziada cha kuwashajiisha, wakati Mhe. Haroun Ali Suleiman alipokuwa Waziri wa Elimu nilifurahi sana yeye alitangaza dau hasa kama mwanafunzi akipata *division one* ya somo hili la sayansi aliahidi kutoa hata laki mbili kwa kila mwanafunzi.

Kwa hivyo, kuna mpango wa kuingia katika *E Government* wakati tunataka kuingia basi lazima tuweke msingi na kuweka msingi ni kuwa na watu wa sayansi hasa mambo haya ya kompyuta. Mhe. Spika, Wizara ya Fedha ingekuwa na kasma maalum itakayowekwa kwa ajili ya kuwapa motisha wanafunzi watakaofanya vyema katika mitihani yao ya sayansi.

Mimi naona wangeweka dau hasa kwamba mwanafunzi wa Zanzibar atakayepata "A" tuseme kama ya *Physics* tutampa pesa na mwanamke tutamzidishia atayepasi sayansi ili na wao wasichana waweze kupenda haya masomo ya sayansi.

Mhe. Spika, hapo hapo kwenye elimu sasa niende moja kwa moja katika hii elimu mbadala na mafunzo ya amali. Mhe. Spika, serikali yetu imeanzisha kitu kizuri kwa sababu haya mafunzo ya amali yanawasaidia wanafunzi wetu wanapomaliza vijana wetu hujiajiri wenyewe. Napenda nilishukuru Baraza hili kwa kuweza kupitisha sheria ile iliyoweka *Vocational Training Authority* ambayo ilipitishwa hapa hapa Barazani mwaka 2006.

Mhe. Spika, authority hii inaweza kutusaidia sana kwa kuweza kuwafanya wanafunzi wetu wa mafunzo ya amali kufanya vizuri. Mhe. Spika, katika sheria ile nadhani kila muajiri kwa taarifa tulizonazo alitakiwa alipe *five percent* ya mshahara ya muajiri wake kuchangia katika hii *Vocational Training Authority* taasi hii ya elimu ya amali anatakiwa kila muajiri aweze kuchangia *five percent* ya mshahara wake ili waajiriwa waweze kupata mafunzo.

Mhe. Spika, la kusikitisha sheria hii ilipitishwa mwaka 2006 lakini ilianza kutumika mwaka 2009, hapa pana mapungufu makubwa kwamba sheria karibu miaka 3 imetungwa lakini imeanza kutumika mwaka 2009.

Mhe. Spika, kwa taarifa nilizonazo ni kwamba michango inayoahirishwa hapa ni kwamba imetakiwa mara moja tu. Kwa hivyo, ningeomba kama taarifa hizi ni kweli au si kweli Mhe. Waziri atueleze kwa sababu nilidhani nilipoangalia katika kitabu hiki nimeona kwamba mafunzo ya amali yametengewa shilingi milioni mia tatu tu kwa ajili ya maendeleo. Lakini sijui hizi ni katika hiyo michango inayowasilisha yote ni mia tano au pesa hizi ziko wapi, kwa sababu

kama kila muajiri anachangia mambo manne hivyo hawa wangekuwa na pesa nyingi hawa *vocational training*.

Mhe. Spika, lakusikitisha tunayo skuli iliyopo Vitongoji ya Mafunzo ya Amali hizo shilingi milioni mia tatu walizopelekewa hizi wanahitaji *principle* kwani mali zinaharibika sana, lakini milioni mia tatu ziweze kuje *fence* skuli iliyopo Kaskazini Unguja. Mhe. Spika, ni kwamba zote zinahitaji *fence* skuli hizi kwa sababu wanyama wanaingia wanaharibu mazingira ya skuli, wizi pia upo mwingi. Mhe. Spika, nilidhani haya mafunzo ya amali yangepewa umuhimu sana ili wanafunzi wetu wanapomaliza pale waweze kujiajiri wenyewe na kuipunguzia mzigo serikali.

Mhe. Spika, nadhani serikali ingeipa kipaumbele mafunzo haya kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati inayoshughulikia haya mambo ya wanawake na ustawi wa jamii, hivyo tulikwenda kule skuli ya mafunzo ya amali iliyopo Vitongoji tukaangalia pale kuna baadhi ya vitengo hawajavifungua pale kwa sababu hawana pesa. Mhe. Spika, tumekwenda katika maeneo mengine vifaa ni kidogo sana, nafikiri Wizara ya Fedha labda wangewapangia kasma Wizara ya Elimu katika eneo hili wakaweza kuimarisha haya mafunzo ya amali ili vijana wetu wakaweza kujiajiri wenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake vile vile amezungumzia kwamba serikali ina mpango wa kuanzisha *E Government* ni mpango mzuri sana Mhe. Spika. Nadhani mpango huu unaweza kuisaidia serikali kuwa na mawasiliano mazuri baina ya taasisi za kiserikali pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, hii ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetofautiana sana na serikali nyengine zilizopo hasa hizi zilizokuwa Kusini mwa Jangwa la Sahara haikupatikana hivi kimaneno maneno. Ni serikali iliyopatikana kimabavu na ina historia kubwa katika kupatikana kwake. Kwa hivyo, inahitaji udhibiti wa hali ya juu. Sasa tunaingia katika mfumo huu wa hii *E Government*, huu ni mfumo ambao *transparence* itakuwa kubwa, serikali inaweka mitandao kwa wananchi ndani ya nchi na hata nje ya nchi. Kwa hivyo, zile taarifa za kiserikali ikiwa hatukuwa makini basi tunaweza kukuta kwamba kunakuwa na *linkage* ya taarifa za kiserikali. Kwa hivyo sasa, naomba niishauri serikali mambo yafuatayo Mhe. Spika.

Kabla ya kuingia katika hii *E Government* lazima tupate kitu kinachoitwa *surver*. Hii ni *internet service provider*. Hii itasaidia sana kuweza kuzi-*centralize* zile *website* zote, serikali inaweza kuzi-*centralize website*, kwa hivyo zile taarifa unapotaka kuzichuja unaweza ukazichuja, zinazotaka kupelekwa kwa watu ikazipeleka, lakini bila ya kujitayarisha kwa kuendelea kutumia hii *ZANZINET* basi taarifa za serikali zitapenya. Kwa hivyo, ni vyema kabla ya

mfumo huu wa *Internet Service Provider* ili tuweze kudhibiti hizo taarifa zetu za siri. Kuna taarifa za kiusalama ni lazima tuwe tunazidhibiti.

Vile vile Mhe. Spika, ni vyema kabla hatujaingia huko tukawa na *regulatory system of internet* tukazi-*regulate* hizi *internet system* kusudi mambo yetu yakawa hakuna kule kuvuja, zisivuje taarifa zetu ambazo tunataka zibaki katika mawizara, katika taasisi ili wenzetu wasije wakaziweka nje ya mji. Hilo ni jengine kwamba tunapotaka kuingia katika hii *E Government* umakini huo unahitajika sana.

Kwa hivyo, tusijiingize tu kichwa kichwa ni lazima tujitayarishe, ni lazima tuwasomeshe vijana wetu. Kwa sababu ikiwa unataka kuingia ujue ni wangapi wanamiliki kompyuta, ni wangapi wanajua kompyuta, kwa hivyo, kabla hatujaingia tuhakikishe kwamba taaluma hii ya *computer system* tunaipeleka kwa wananchi wetu kusudi na wao waweze kuwa na *access* katika kuchukua taarifa serikalini.

Hivi ninavyosema hata humu ndani ya Baraza tukishaanzisha itakuwa ni tatizo kubwa kwa sababu kuna watu hawajui hata *a, b, c,* kuhusiana na kompyuta. Aidha hivi sasa humu ndani ya Baraza kama mnataka kuingia katika mfumo huo hakuna *system* ya kompyuta angalau kila mwakilishi anakuwa na kompyuta yake hapa anaweza ku-*function*. Sasa tunataka kwenda huko hata sisi huku hatujui, tuwe makini sana katika hilo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, twende katika vyanzo ambavyo Mhe. Waziri amevizungumzia pale kwenye vyanzo vya mapato. Alipozungumzia kwenye vyanzo hivyo akazungumzia karafuu. Nafikiri kuna vyanzo ambavyo hawakuvi *exhaust* baadhi ya vyanzo.

Mimi nakuhakikishia Mhe. Spika, kwanza kuhusiana na mafuta amezungumzia mafuta tu katika vyanzo vipya ambavyo wanatarajia. Kuhusu mafuta hata Mhe. Raya Suleiman kasema hapa kwamba, si *issue* tena, mimi nilifikiria kuhusu mafuta hapa tutaambiwa tayari kuna kasma hii ambayo imetengwa kwa ajili ya kuendeleza utafiti na uchimbaji sio katika kusua sua tena. Wananchi wanalipa kodi kuitisha Baraza hili, Baraza hili limeitwa limeshapitisha maamuzi kwamba mafuta ni mali ya Zanzibar, sasa yachimbwe tu hakuna *discussion* tena, kufanya vyovyote vile ni kupoteza za pesa za walipa kodi ambazo tumawalipisha wananchi kuitisha Baraza kuwa lifanye maamuzi yale.

Kwa hivyo, mimi nategemea kwamba sidhani kuwa katika bajeti hii hamna fungu, ni matarajio yangu kwenye mwezi wa Novemba tunaweza kuona nini bajeti itakayozungumzia suala zima la kuendeleza utafiti na uchimbaji wa mafuta. Mimi kwa timu ninayoiona huku katika *back benchers* Mhe. Spika,

wala tusifikirie serikali kwamba tulioko huku hatuna uwezo wa kuendesha serikali, na laiti serikali ingelikuwa ni kama koti mtu anaweza kuvaa na kuvua basi ningeomba ituazime hiyo serikali wiki tatu tu, mungeona mwelekeo wa Zanzibar katika uchimbaji wa mafuta halafu tungewarudishia serikali yenu. Hebu tuazimeni jamani muone, lakini ndio serikali sio kama koti hatuwezi kuazimwa. Kwa hivyo, sisi lazima tuwalazimishe nyinyi msimamie mambo haya.

Mhe. Spika, sasa chengine kipya cha mafuta ambapo Mhe. Waziri sidhani kama hakukiona, lakini labda amesahau. Wakati Mhe. Rais anafungua Baraza hili Dkt. Ali Mohammed Shein alizungumzia kwamba anataka lianzishwe dawati la *DIASPORA*. Alizungumza na mimi nilifurahi sana kwamba sasa tumeshaona pahala. Mheshimiwa kama kuna nchi Zanzibar ni nchi moja ambayo ina Wazanzibari wengi wanaoishi nje ya Zanzibar, na katika nchi nyingi kabisa hata hizi nchi zilizoko katika Jangwa la Sahara wanawatumia hawa *DIASPORA* kuleta maendeleo katika nchi yao ukiachia Somalia basi na sisi tumeenea sana huko nje ya nchi. Tunaweza tukawa hatumo katika *single number*, lakini hatujaitumia hazina hii.

Naamini kama dawati hilo litatumiwa vizuri basi nakuhakikishia Mhe. Spika, tija itapatikana kupitia *DIASPORA*. Mimi huwa nasikia Mhe. Rais kama anapokwenda nje ya nchi anazungumza na Wazanzibari wanaoishi Sweden, Uingereza, sasa muombe wataalamu watusaidie, vipi serikali inaweza kuvuna mapato kupitia *DIASPORA*. Serikali nyingi zimefanya hivyo.

Sasa Mhe. Spika, mimi nafanya utafiti na nitakapoukamilisha naweza nikauwasilisha kwako jinsi ya baadhi ya nchi zinavyofaidika na *DIASPORA*. Nimeshaona kwamba kuna nchi nyingi zinanufaika na *DIASPORA* na wala si kwamba labda tutanufaika kwa *financial contribution* tu, lakini hata *technical contribution* au *technical advice*. Ninavyokwambia hivi sasa wakati huku sisi tunataka kuanzisha *E Government*, kuna wataalamu waliobobea Wazanzibari katika fani hiyo ya kompyuta ambao wako nje ya nchi huko wananufaisha nchi nyengine. Sasa ingelikuwa tunawatumia vizuri wale wangetusaidia *finance contribution* pamoja na hizo *technical issues* kama hizi lakini tumewadharau.

Mhe. Spika, kuna wengine hivi sasa wana *old force* kubwa katika serikali za nchi nyengine. Watu wa Fuoni tu, hapo wengine wanatoka Kuu Kuu Kangani huko wana *old force* za kiserikali. Sasa kwa nini tuwaache. Mimi naamini serikali ikiwa itajipanga vyema basi naamini tutapata mapato ya ziada, kwa nchi hii yenye watu milioni moja na laki mbili *DIASPORA* watatusaidia sana. Wengine hivi sasa ni *Rotating Ambassador* wa nchi kadhaa, muulizeni Mhe. Ismail Jussa Ladhu anawajua wengine ni *Mayatullah* ni watu wa hapa hapa maeneo ya Kuu Kuu Kangani au Fuoni na Mwera wanaongoza taasisi za kidini,

naamini kwamba tukiwatumia vizuri *DIASPORA* na wako willing lakini serikali tu inawazembea zembea. Ndio nikasema kama mnatuazima sisi huku *back benchers* hiyo serikali kwa muda wa miezi mitatu mtaona vitu vyetu, nina timu yenye uwezo sana hapa, nimezungukwa na pande zote na timu yenye uwezo, tuazimeni muone miezi mitatu tu.

Mhe. Spika, nimalizie kwenye umeme mbadala, kwa sababu mambo mengi yamezungumzwa mimi natia nyalio tu kidogo. Umeme mbadala tumeambiwa utaanzishwa katika maeneo kadhaa lakini yote yamezungumziwa hapa Unguja kama kuna eneo lenye upepo mwingi basi ni Mashariki ya Pemba. Ningeomba ufanywe utafiti wa kina kama ile bahari ya mashariki ya Pemba itafanyiwa utafiti basi pale umeme utakaovunwa kutokana na upepo utakuwa ni mkubwa sana.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nasema kama waziri atanijibu kwenye hili suala langu la *contribution* inayotolewa ambayo wanakusanya *TRA* kwa muajiri kupeleka katika ile *authority ya vocational trading*, akinijibu vizuri na akinionesha mapato hayo ni kiasi gani pamoja na watakavyoitumia *DIASPORA*, pale ambapo wataweza kutuletea *mini budget* ndogo kwa ajili ya kuchimba mafuta sio mjadala mwengine, basi nitaunga mkono hoja hii. Ahsante sana Mhe. Spika.*(Kicheko).*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Lakini kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana asubuhi hii ya leo katika Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kujadili hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na wasaidizi wake kama Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Manaibu Katibu lakini pia bila ya kumsahau Katibu wa Mipango katika wizara hii pamoja na maafisa wote wa Wizara ya Fedha. Pia na wale wote ambao wameweza kufanikisha kwa namna moja au nyengine bajeti hii nzuri, bajeti ya serikali ya mwaka 2011/2012. Kwa kweli Mhe. Spika, bajeti hii ni bajeti nzuri, imepangika, imegusa katika kila maeneo na Mhe. Waziri anastahiki pongezi.

Nataka pia nimpongeze na kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa muda mfupi tu kuweza kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ambapo tabaan sasa hivi tunaona imeanza kwa kazi na kwa vitendo. Kwa hivyo tunawatakia kila la heri katika kufanikisha maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake hii ameelezea mipango yake na ame-*quote* kwamba mipango yote hii ya bajeti ya mwaka huu ya maendeleo ameipanga kutokana na ule mwelekeo wa serikali wa mipango ya maendeleo ya Dira 2020, lakini pia imejumuisha mikakati ile ya kupunguza umasikini (MKUZA) lakini pia imezingatia katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa kweli Mhe. Spika, bajeti hii tokea Mhe. Waziri alipoisoma hapa katika Baraza lako nimekuwa nikiipitia pitia kila wakati, lakini kila ninapozunguka naona tayari amesha-*cover*, ilikuwa nimekaribia kukosa hata namna ya kuchangia, kwa kweli bajeti ni nzuri inastahili pongezi.

Mhe. Spika, bajeti hii Mhe. Waziri safari hii hakuiita jina, hakuibatiza jina lakini mimi nataka kusema kwamba bajeti hii ni bajeti ya watu. Mhe. Waziri bajeti yako ni bajeti ya watu. Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Spika? Kwa sababu imegusa maeneo makubwa matatu ambayo maeneo hayo yote yamegusa maisha ya watu. Kwanza imezungumzia juu ya nia ya kuimarisha kilimo.

Sekta ya Kilimo ikiwemo pamoja na Mifugo na Uvuvi. Sekta hii ya kilimo kwa kiasi fulani inabeba asilimia 42 ya wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, karibu nusu ya wananchi wa Zanzibar imewazungumzia maslahi yao na mambo yao na katika sekta hii imekusudia kupunguza bei ya mbolea, pembejeo za kilimo lakini pia imekusudia kuimarisha mambo chungunzima ambayo kwa kiasi fulani kama yatatekelezwa vizuri basi suala la kilimo litaimarika zaidi. Kwa hivyo, tutegemee asilimia 42 ya wananchi wa Zanzibar watafaidika na bajeti hii.

Lakini pia bajeti hii inakusudia kurekebisha maslahi ya watumishi wa umma, inakusudia kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Kwa maana hiyo, wale watumishi wa umma ambao ni sehemu ya jamii nao watafaidika katika bajeti hii ya serikali ambapo mishahara ya watumishi itarekebishwa, maslahi yao yatarekebishwa na mifumo mizima juu ya utumishi ambapo ni jambo ambalo lilikuwa likilalamikiwa kila wakati nalo litaweza kurekebishwa. Kwa hivyo, hii ni bajeti ya watu.

Jengine ambalo maana ya kusema kwamba ni bajeti ya watu kwamba serikali au Mhe. Waziri amekusudia kutopandisha kodi ya aina yoyote. Kwa maana hiyo, ikiwa kodi haitopandishwa basi hata bidhaa nazo hazitopanda bei kiholela. Hapa Mhe. Waziri tunakuomba uwe makini sana na wafanyabiashara wetu na kwa sababu wafanyabiashara wetu kila wakati wanakuwa wao wanataka kutengeneza faida lakini kodi hukupandisha kwa maana unazuia ile *inflation* ambayo inaweza ikakua. Kwa hivyo, vile visingizio vya

wafanyabiashara kwamba kodi imepanda katika kipindi hiki cha mwaka huu itakuwa hakipo. Kwa hivyo, bajeti hii ni bajeti ya watu, imewagusa watu katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametuelezea katika bajeti hii namna ya uchumi unavyokua, ambapo pato halisi la Zanzibar limekua kwa asilimia 6.5 kwa kufikia shilingi 385 bilioni mwaka 2010, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 kwa mwaka 2009. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hii ni taarifa nzuri, pamoja na kwamba huu ukuaji wa uchumi unakwenda taratibu mno lakini hali ya uchumi inaonekana inaendelea kukua kwa asilimia hizi ambazo Mhe. Waziri ametueleza. Lakini hata pato la mtu binafsi kwa mwaka 2010 liliongezeka kwa asilimia 7.6 kutoka shilingi 728,000 mwaka 2009 hadi kufikia shilingi 783,370 mwaka 2010. Kwa hivyo, hii ni taarifa njema Mhe. Spika, kwamba uchumi wa nchi unaongezeka, pato la mtu linaongezeka, tabaan mambo yanaonekana yanakwenda mbele.

Lakini Mhe. Spika, mara nyingi tumekuwa tukipata masuala kutoka kwa wananchi wa kule mitaani pale wanaposikia kwamba uchumi umeongezeka, pato la mtu kwa mtu limeongezeka, wanakuwa wanajiuliza na kwa sababu wao kila wakati wanakuwa hawana fedha mfukoni wanasikia kwamba serikali imetangaza kuwa uchumi umekua, pato la mtu limekua lakini wakijiangalia kila ukicha fedha mfukoni hakuna.

Mhe. Spika, ni lazima tubadilike katika namna ya kukuza uchumi wetu. Sisi sio wataalamu wa uchumi lakini mara zote huwa tunapata kutoka kwa wataalamu wa uchumi. Kwa mujibu wa wataalamu wa uchumi wa *BOT* wanasema kwamba, ili uchumi uweze kumfikia kila mtu katika nchi ni lazima uchumi huo ukue kwa zaidi ya asilimia 10. Hiyo ni takwimu ya wana uchumi wa *BOT* na sasa hivi tupo kwenye asilimia 6.7 tabaan kwamba itakuwa si rahisi kwa sasa hivi wananchi wetu wa kawaida kuona wana hali ya ukuaji wa uchumi wetu.

Lakini jengine ambalo Mhe. Spika, nalo tumelipata kutoka kwa wana uchumi, taarifa tulizozipata zinasema kwamba uchumi wetu unakua lakini unakua kulingana na sekta za huduma kikiwemo kilimo na utalii. Sasa uchumi unapokua katika utaratibu huu au katika sekta hii, tabaan unakuwa unaongezeka kidogo kidogo. Kwa hivyo, inakuwa si rahisi uchumi ule kumfikia kila mtu, isipokuwa pale uchumi utakapoongezeka katika maeneo ya viwanda basi uchumi ule unakuwa unaongezeka kwa kasi na kila mmoja unamfikia.

Mhe. Spika, nilikuwa naangalia suala la vipaumbele. Katika kufikia hali hii ya ukuaji wa uchumi ulio imara ambao kila mmoja wetu utamgusa, ni vipi serikali imeweka kipaumbele katika kuimarisha sekta ya viwanda? Nimeangalia

vipaumbele ambavyo Mhe. Waziri ameviweka ni vizuri, lakini vinaonekana kwamba vimekosa kulenga katika lile eneo ambalo linaweza likabadilisha namna ya ukuaji wetu wa uchumi.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba tunahitaji kubadilika, njia zetu za kuimarisha uchumi ni lazima zibadilike ili uchumi huu tunapouzungumzia kukua kwake kila mtu ahisi kwamba kweli uchumi umeongezeka na pato la mtu kwa mtu limeongezeka. Tunahitaji kuimarisha namna ya uwekezaji, uwekezaji katika maeneo ya viwanda na ili tuweze kuwekeza katika maeneo ya viwanda ni lazima tuimarishe maeneo huru ya uchumi kwa sababu ni maeneo ambayo tayari yameshatayarishwa, maeneo ya kujenga viwanda pamoja na kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko nayo imetuelezea namna wanavyokusudia kuimarisha maeneo haya na kuifanya Zanzibar kuwa ni eneo huru la kiuchumi. Lakini ni lazima kipaumbele kiwekwe katika eneo hili la viwanda.

Lakini pia tunahitaji kubadilika katika mfumo wa uimarishaji wa uchumi wetu. Ni lazima tufanye utaratibu wa kuwekeza katika maeneo yetu ya bandari, maeneo ya Uwanja wa Ndege, maeneo Huru kama nilivyotangulia kusema. Maeneo haya kama tutakuwa tunayafanyia kazi na kuachana na ule utaratibu tuliokuwa nao sasa hivi basi nchi yetu inaweza kupiga hatua.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo ningehitaji kulizungumzia ambalo na Mhe. Waziri amelizungumzia ni suala la kuimarisha mapato yetu huku tukipanga mipango ya matumizi ya fedha na mipango ya maendeleo tunahitaji kuimarisha mapato. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyojipanga katika kuimarisha mapato yetu ya Zanzibar. Amesema kwamba serikali imekusudia kuimarisha zaidi usimamizi na ukusanyaji wa mapato kwa vianzio vilivyopo na kuziba mianya inayotumika katika kuepuka kupunguza kukwepa kulipa kodi pamoja na kuendelea kufuatilia matumizi mabaya ya misamaha ya kodi nchini. Hii ni njia muhimu sana na kwa sababu bila ya kuwa na mapato ya uhakika basi mipango yetu ya maendeleo haiwezi ikafanikiwa.

Kwa kweli Mhe. Spika, bado mapato yanayokusanywa hapa kwetu naweza kuthubutu kusema labda ni aslimia 50, kuna zaidi ya asilimia 50 ya mapato yanavuja kutokana na watu wajanja. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tufanye kila linalowezekana kuona kwamba tukusanye karibu ya kodi zote zile ambazo zinastahiki, kodi zinazotokana na biashara hazijakusanywa vizuri.

Mhe. Spika, utashangaa leo mtu anakwenda dukani kununua kitu hapewi risiti. Hilo ni jambo ambalo limezoweleka hapa visiwani hakuna risiti, hakuna chochote unakwenda unanunua bidhaa tena ya thamani kubwa lakini hakuna hata risiti unayopewa. Sasa hebu tujiulize, ni vigezo gani vinavyotumika kwa

wenzetu wa *ZRB* kwa mtu yule ambaye anakwenda kulipa ile kodi ya ongezeko la thamani wakati yeye biashara zake anazoziendesha pale hatoi risiti wala kitu chochote, ni tabaan kwamba mapato yanaonekana katika eneo lile yanavuja na tunahitaji kuyasimamia na kuona kwamba Zanzibar inakusanya mapato yake halisi kutokana na sekta ya biashara.

Lakini hata katika sekta ya utalii, inaonekana kwamba kuna mapato mengi yanavuja katika sekta hiyo. Kwa hivyo, tumuombe sana Mhe. Waziri ili aweze kutekeleza vizuri bajeti yake hii basi ni vyema akasimamia zaidi uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato na kujaribu kuziba mianya ile ambayo wafanyabiashara wanaitumia ya kukwepa kulipa kodi.

Mhe. Spika, mimi hivi karibuni nilifanya safari kwenda Kenya. Wenzetu wa Kenya walichoweza kufanikiwa ni juu ya wafanyabiashara kulazimika kutoa risiti, kito chochote unachokinunua Kenya utapewa risiti. Mfanyabiashara hakupi kitu hata ukinunua *pair* ya kanga lazima umeshapeleka pesa anakupa risiti ndio anakupa bidhaa. Kwa hivyo, tukajifunze kutoka kwa wenzetu wa Kenya wamefanya juhudi gani, wamewezaje mpaka wafanyabiashara wameshajihisha na kufanya jambo hili.

Mhe. Spika, juzi kamati yangu ilipokuwa ikizungumza na watu wa *ZRB* nilizungumzia hili, lakini hoja iliyojengeka kutoka kwa wakusanyaji mapato hawa wa *ZRB* wanasema kwamba wameomba fedha serikalini kwa ajili ya kuimarisha hili lakini kwa bahati mbaya sana fedha hadi leo
Hawajapatiwa. Wamejipanga vizuri wameanzisha mradi ili kuona kwamba jambo hili linafanikiwa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri unapotaka kumkama maziwa mengi ng'ombe ni lazima umpe majani.

Namuomba Mhe. Waziri awapatie nyenzo watendaji wetu wa *ZRB* ili hivi sasa wasipate sababu ile ya kusema kwamba tumeomba fedha kwa ajili hii na ndio maana inakuwa hivi na hivi zile hoja nyingi ziweze kuondoka. Wapatiwe fedha katika mipango yao ili tuone kwamba makusanyo haya ya kodi yanakusanywa *at least* kwa asilimia 90. Mimi ninaamini Zanzibar mapato yapo mengi sana na kama tutayakusanya ipasavyo basi tutaweza kufanikiwa. Kwa hivyo, pamoja na juhudi hizi zinazofanywa ni lazima usimamizi wa jambo hili uwepo na watendaji waweze kusaidia.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amezungumzia suala zima la kuimarisha Muungano. Suala la kuimarisha Muungano ni suala muhimu na kwa sababu Muungano umetusaidia mambo mengi. Lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa makini ili tuweze kuongeza uchumi wetu. Kuna eneo hili ambalo tuna matumaini kwamba kama litasimamiwa vizuri na humu Mhe. Waziri amelizungumzia suala la ripoti ya *Joint Financial Commission (JFC).*

Mhe. Spika, suala hili ni eneo muhimu sana na sisi tumejaribu kuzungumza nao wale watu wa *commission* wanasema kwamba mapato yanayotokana na kodi za Muungano yanaweza yakaendesha shughuli za Muungano na fedha bakaa kubwa itabakia itaweza kugaiwa kwa serikali zetu mbili zote.

Lakini sisi tunajiuliza kwa nini ripoti hii imewasilishwa serikalini katika serikali zote mbili tokea mwezi wa Agosti, 2006 na hadi leo ripoti ile haijafanyiwa kazi. Juzi Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake ametueleza kwamba ripoti hii tayari imeshawasilishwa lakini uwasilishwaji huu unaonekana ni wa mara ya pili lakini mara ya kwanza imewasilishwa haikufanyiwa kazi na kwa kweli imeshachukua muda mwingi ndio maana imerejeshwa tena serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Kwa hivyo, jambo hili tunamuomba sana Mhe. Waziri ashirikiane na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha ripoti ile inafanyiwa kazi na unaanzishwa mfuko maalum kwa mujibu wa katiba. Kwa sababu kutokana na kutokuwa na mfuko ule maana yake ni ukiukwaji dhahiri wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano tokea mwaka 1977.

Mhe. Spika, ili Mhe. Waziri alisimamie jambo hili na tunaomba sana afanye kila linalowezekana na kama hakuna uwezekano wa nguvu zake basi tunaomba Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza hili ikutane na Kamati ya Fedha ya Bunge kuzungumzia jambo hili na mustakbali wake uweze kupatikana kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri pia ametuzungumzia juu ya suala la mafuta. Suala la uchimbaji na utafutaji wa mafuta kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar au Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala hili ni la Muungano. Lakini Mhe. Spika, Baraza lako tukufu lililopita suala hili lilichukua nafasi kubwa, tumeweza kujadili kwa kina, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetuletea waraka tukaujadili na tukafikia pahala juu ya jambo hili.

Kwa hivyo, mimi nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na serikali bado kuna haja ya kusimamia jambo hili. Huku tukitafuta namna ya kupata vianzio vyengine vya mapato basi suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta ni jambo muhimu. Rasilimali hii ni ya Wazanzibari wenyewe na ni lazima itumike.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu mara zote anapokupa kilema anakupa na mwendo. Kabla ya suala hili la utafutaji wa uchimbaji wa mafuta Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa inategemea pato lake kutokana na karafuu. Lakini sote ni mashahidi hapa kwamba sasa uzalishaji wa zao la karafuu unashuka siku hadi siku, sasa hivi kwa msimu mzima wa mwaka basi hata zile tani elfu tano za karafuu hazitimii na hili linatokana na uzalishaji.

Mhe. Spika, jana Mhe. Ali Abdalla Ali amesema hapa amepanda mikarafuu 20 amepata mikarafuu miwili, akapanda tena mikarafuu 10 akapata mkarafuu mmoja. Hii inaonesha dhahiri kwamba zile nguvu au kasi za ardhi kwa wakati ule kwa zao hili zimeanza kupungua.

Mhe. Spika, baada ya zao la karafuu tukabuni tena njia nyengine tukaanzisha sekta ya utalii ikawa imechukua nafasi kubwa kwa uchumi wa Zanzibar lakini nayo inaonekana bado ni tete inalega lega. Kwa hivyo, ni dhahiri sasa kuna haja ya kulishughulikia jambo hili la utafutaji na uchimbaji wa mafuta ili wananchi wa Zanzibar waweze kufaidika na rasilimali hii ya mafuta.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri humu pia amezungumzia suala la maji kwamba katika bajeti hii serikali itatilia mkazo sana upatikanaji wa maji safi na salama. Sisi tunakubaliana na hoja hii na kwa sababu wananchi wetu kwa kweli wana matatizo makubwa sana ya maji. Lakini hili nitakuja kulizungumza zaidi wakati wa bajeti ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Lakini kwa kuwa humu Mhe. Waziri ameligusia na ni suala muhimu basi ni vyema na sisi tukalizungumzia ili wananchi wetu wajue kwamba suala la matatizo ya maji ni suala muhimu katika nchi yetu na sisi wawakilishi wao waliotuchagua tunalizungumzia. Lakini pia tunaridhika na mipango ya serikali juu ya kuondosha tatizo la maji ambapo Mhe. Waziri ametueleza kwamba jumla ya dola za Kimarekani milioni 123 zinahitajika kuondosha matatizo ya maji kwa Zanzibar ambapo visima zaidi ya 52 vitachimbwa.

Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa maji linahitaji kusimamiwa vizuri. Nakumbuka Mhe. Spika, katika Mkoa wetu huu wa Mjini/Magharibi kulikuwa na mradi ule wa Wajapan ambapo walifanya *study* katika mkoa huu. Lakini hatimaye wakatueleza kwamba zitakapopatikana fedha kiasi cha shilingi bilioni 30 basi tatizo la upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi litakuwa tena ni historia. Kwa bahati nzuri ndugu zetu wa Japan wakatusaidia fedha hizo na kuanzia mradi wa awamu ya mwanzo na awamu ya pili yote imetengenezwa lakini bado tuna matatizo ya maji.

Kwa hivyo, suala hili la upatikanaji wa maji mbali ya upatikanaji wa fedha linahitaji kusimamiwa kwa karibu sana. Vyenginevyo tunaweza tukazipata hizi fedha milioni 123 ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* tayari imeshaonesha nia ya kusaidia katika sehemu ya fedha hizi lakini bado matatizo ya maji yakaendelea kuwepo. Kwa hivyo, suala la kusimamia miradi hii inayoshughulikia masuala ya maji ni muhimu sana.

Mhe. Spika, bajeti hii Mhe. Waziri ameweka vipaumbele kama 6 na tunampongeza kwa vipaumbele alivyoviweka. Kipengele kimoja

alichokizungumzia ambacho kinazungumzwa sana hapa ni namna ya kuimarisha huduma ya afya ambapo msisitizo zaidi ulilenga katika ununuzi wa vifaa vya hospitali, dawa muhimu pamoja na kuimarisha huduma zinazotolewa na vituo vya afya vya wilaya na mikoa. Hichi ni kipaumbele muhimu.

Mhe. Spika, unapoweka kipaumbele juu ya jambo pamoja na hali yetu ngumu ya kifedha lakini ni lazima uoneshe ni namna gani unapoongeza bajeti katika eneo lile. Eneo hili linahitaji kupewa msukumo unaostahiki ili kuona kwamba afya za watu wetu, huduma za dawa pamoja na masuala mengine yanayohusiana na afya yanatekelezwa kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, uzoefu unaonesha kwamba hata zile *ceiling* zetu tunazowawekea mawizara basi ule utekelezaji wake kidogo unakuwa haufikii katika ile asilimia ambayo imekusudiwa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri sekta ya afya ni muhimu, wakati unapowaingizia fedha kwa ajili ya miradi na mambo mengine kwa ajili ya utendaji wa kazi, basi hicho kiwango kidogo ambacho wamepangiwa waweze kukipata kwa asilimia mia moja. Hili ni eneo muhimu ambalo linahitaji kuangaliwa kwa makini na kwa sababu ndipo panapogusa maisha ya watu.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Mhe. Waziri ameliwekea kipaumbele ni masuala ya elimu. Suala la elimu ni muhimu na tunaishukuru sana serikali kwamba katika bajeti hii tayari wametenga ziada ya karibu shilingi bilioni moja ukilinganisha na bajeti iliyopita kwa ajili ya kuwalipia ada watoto wetu hawa ambao wanasoma elimu ya juu waliokuwa nje na ndani. Mhe. Spika, kiwango hichi kwa kweli ni kidogo lakini serikali imejitahidi kuweka ziada ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya watoto wetu.

Mhe. Spika, kwa kweli wazee wa watoto hawa wanaosoma elimu ya juu wanakuwa katika wakati mgumu sana. Mtoto anasoma vizuri, anafaulu vizuri lakini kwa bahati mbaya anapofaulu katika kuendelea na masomo ya juu basi wakati mwengine wanashindwa kupata ile ada asilimia ambayo imewekwa. Kwa hivyo, eneo hili nalo Mhe. Waziri basi aliangalie kwa jicho la huruma kile kiwango walichowekewa basi kiweze kupatikana kikamilifu ili watoto wetu hawa waweze kupata elimu ya juu. Wanapopata elimu ya juu ndio wataalam wetu hawa wataweza kuja kutusaidia hapa katika kuendesha elimu.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wangu umemalizika kwa hivyo sina la ziada isipokuwa zaidi nitakuja kuchangia wakati wa bajeti zile za mawizara ambapo tutaweza kutoa michango zaidi katika yale maeneo ambayo yameelekezwa na wizara husika. Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono bajeti hii ya watu na wananchi wa Zanzibar wasiwe na wasi wasi na bajeti hii kubwa zaidi ni kusimamia utekelezaji.

Mhe. Spika, hapo ndipo kwenye tatizo, kama Mhe. Waziri bajeti hii hataisimamia basi mwakani atakuja kuwa hana maneno. Lakini bajeti hii kama utaisimamia na ikaweza kutekelezwa angalau kwa asilimia 90 tu basi nchi yetu itabadilika, kilimo kitabadilika, afya itabadilika, sekta ya elimu itabadilika, barabara na mambo mengine. Lakini kubwa iweze kusimamiwa pia utekelezaji wa bajeti hii uweze kwenda vizuri.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hotuba hii juu ya Mpango wa Maendeleo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutufikisha hapa. Mhe. Spika, mimi kwanza nipo katika kilimo kwa sababu mimi mwenyewe ni mkulima lakini kinachoturudisha nyuma ni wanyama waharibifu. Hapo zamani tulipokuwa tukilima ilikuwa kila baada ya mwezi kule kwetu shamba tunaletewa wasasi wanasaka wanauwa nguruwe. Lakini hivi sasa wanyama waharibifu, wadudu wamejaa kwenye makonde yetu watu wanarudi nyuma kwa kilimo.

Mhe. Spika, mazao kama mihogo, migomba utaiona meusi na hakuna utafiti wowote ambao umefanywa wala hatujui ni kitu gani kinachosababisha vile. Mhe. Spika, ningewaomba mabwanashamba wawe na karibu na wakulima kuwapitia wananchi wao watazame kuna nini kwenye mashamba yao.

Mhe. Spika, pili kuhusu uvuvi. Mhe. Spika, kule kwetu ni baharini lakini utagundua hatuli samaki kwa sababu hatuna nyenzo. Mhe. Spika, ningeiomba serikali itupatie nyenzo za uvuvi ili tuweze kuboresha kazi ile ya uvuvi. Mhe. Spika, tunakula samaki wanapokuja watu ambao wana nyenzo, wanakuja Wakojani kutoka Pemba wanavua pale tunakula samaki Jambiani nzima ikisha tunapeleka mjini kwa kuuza.

Mhe. Spika, kwa upande wa wanawake kule kwetu kuna bahari wanavua, wanapanda mwani. Mhe. Spika, mwani ni zao kubwa kule kwetu na asilimia kubwa ya wenye kupanda mwani ni wanawake lakini zao lile halipewi kipaumbele. Mhe. Spika, kilo moja inauzwa kwa shilingi mia mbili hamsini mpaka mia tatu halina faida yoyote, kipande cha sabuni bado hujapata, robo ya sukari bado hujaipata. Mhe. Spika, ningeiomba serikali iwafahamishe wale wenye makampuni kwamba angalau wanunue kilo moja shilingi elfu moja na mia tano wafaidike wananchi. Wananchi wanateketea na zao hili wenyewe wanawake lakini lina shida.

Mhe. Spika, nakuja kwa upande wa walimu. Mhe. Spika, walimu ni watu wa kupewa kipaumbele maana yake mawizara yote wanaanzia kusomeshwa na

walimu mpaka kufikia polisi, jeshi au kazi yoyote ile lakini walimu mshahara wao mdogo. Mhe. Spika, ningeomba wizara hii wapewe kipaumbele waongezewe mishahara yao kwa sababu wanapata shida.

Mhe. Spika, zamani tuliposoma sisi ilikuwa darasa moja watoto 25 au 30 sasa utagundua darasa moja watoto 70 mpaka 80 tunawapoteza wanafunzi. Tutasema walimu hawasomeshi lakini wanasomesha isipokuwa nguvu zao zinakuwa kidogo wanafunzi wanawazidi sana kipimo. Mhe. Spika, ingawa walisema kwamba kuna mabanda tayari yanatarajiwa kujengwa basi ningeiomba serikali itilie mkazo kuhusu suala hili.

Mhe. Spika, suala la mafuta kila siku nalisikia lakini sijatia saini kama yapo au hayapo. Mhe. Spika, ningeomba nifahamishwe kwamba kweli haya mafuta yapo na kampuni gani imeshahakikisha kwamba mafuta yapo na yapo wapi katika visiwa vyetu viwili hivi. Ikiwa yapo tuambiwe yatachimbwa tarehe ngapi, mwaka gani. Ikiwa tayari yapo tuhakikishiwe kwamba wananchi sote tunabeba masururu na mapauro twende tukachimbe mafuta hayo.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii mia kwa mia na wananchi wangu wa Wilaya ya Kusini.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hotuba hii. Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe, pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Spika, nianze kwa kusema kwamba bajeti hii kiujumla imeleta matumaini, pia inaonesha ukuaji wa bajeti hii kutoka shilingi bilioni 444 ya mwaka jana mpaka kufikia shilingi bilioni 613 ambayo imechanganya mambo mbali mbali ikiwemo kazi za kawaida na za maendeleo.

Mhe. Spika, pili ni jambo linalotia moyo zaidi serikali kuona kwamba imetenga shilingi bilioni 234 kwa matumizi ya kawaida ambayo humu imejikita zaidi katika kuongeza mishahara ya wafanyakazi na kwa kweli hilo ni jambo la faraja.

Mhe. Spika, niseme tu hapa kwamba ile mishahara nimuombe Mhe. Waziri husika atakapokuja hapa ikidhi ile haja. Kwa sababu tunaona kwamba mishahara mpaka sasa hivi kutokana na ongezeko la hali ngumu ya kiuchumi na hali ngumu ya watu wetu. Kwa hivyo, angalau ikija ikitamkwa hiyo mpaka sasa hivi ipo kwenye mabano lakini niseme kwamba itazamwe kwa undani zaidi ili angalau ipunguze ule ukali wa maisha.

Mhe. Spika, jambo la tatu nizungumzie miradi. Mhe. Spika, miradi kwa kiasi fulani Mhe. Waziri ametenga fedha ambazo ni shilingi bilioni 378 humu zitakuwemo fedha zetu sisi wenyewe na fedha za wafadhili. Hata hivyo, watu walipiga kelele hapa kwamba hii bajeti ni tegemezi, lakini nikisema kwamba ni tegemezi ni lazima sisi wenyewe tuoneshe nguvu yetu japo ni ile ndogo. Kwani Mhe. Spika, watu wamesema ni vibaya kuiba, lakini kama tutakopa na tutakubaliwa ili tufanikishe mambo yetu katika bajeti zetu si vibaya. Mhe. Spika, tunaweza tukakosa na kile ambacho chetu kidogo tukajumlisha pamoja.

Mhe. Spika, jambo la msingi ni kwamba ile mikopo ambayo tutaichukua ni mikopo nafuu na halafu tuirejeshe. Mhe. Spika, hizi kazi za maendeleo mpaka sasa hivi kwa upande wangu mimi nasema kwa sababu tumechangia na tutawapa moyo wale *donors* ambao wanatusaidia.

Mhe. Spika, bajeti hii imeonesha ukuaji katika sekta zote ikiwemo mama na mtoto, elimu, ufugaji na kadhalika, pia kutoa kipaumbele kwa MKUZA namba mbili.

Mhe. Spika, mchango wangu katika bajeti hii ili iwe *effective* kuna mambo ningependa kushauri. Ni kuwa na watu ambao watakuwa ni watekelezaji, uongozi bora, mipango makini iliyo wazi, utaalam na usimamizi mzuri wa bajeti hii. Yote haya yakikusanywa tutahakikisha mafanikio na malengo yetu.

Mhe. Spika, naipongeza serikali ya awamu ya saba inayoongozwa kwa ilani ya Chama cha Mapinduzi chini ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sina mengi isipokuwa niseme mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono hoja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru lakini hali yangu naona sio nzuri tokea jana, lakini nitajitahidi au sijui utaniruhusu kwamba nikae au niendelee hivyo hivyo.

Mhe. Spika: Kama hujisikii unaweza ukakaa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, mimi zaidi nitakuja kwenye ajira. Mhe. Spika, ajira ni tatizo la taifa na serikali bado imejitoa katika kuajiri watu. Mhe. Spika, sekta binafsi ndio iliyoziba pengo la kuajiri watu ambapo bado sasa hivi haijajiandaa katika kuajiri watu. Mhe. Spika, ningeiomba serikali ikawajengea mazingira mazuri ili sekta hizi ziweze kujitayarisha na kuandaa ajira.

Mhe. Spika, nije katika suala la kilimo. Mhe. Spika, kilimo ni sekta mama ambayo inategemewa na wengi na hususan sisi wenyewe tuliomo humu. Kwa sababu Mhe. Spika, ikiwa si kilimo sisi sote humu pesa haitufai chochote ni lazima kilimo ndio kinachotuongoza.

Kwa hivyo, ningeomba sekta ya kilimo iunganishwe na sekta ya viwanda ili iweze kuzalisha zaidi kwa sababu wakulima ni wengi na mazao ni mengi yanayozalishwa Zanzibar lakini wakulima hawajui mazao yale wayauze wapi. Hatimaye mazao yale Mhe. Spika, yanabakia kuoza na kuvamiwa na mafunza.

Kwa sababu sasa hivi tukiangalia hasa suala la embe linavamiwa na mafunza, laiti ingekuwa suala hili la kilimo limeunganishwa na suala la viwanda ingekuwa wananchi wanapovuna mazao yao wanapeleka viwandani kuuza ili kupata mafanikio yao. Lakini Mhe. Spika, tatizo hili limekuwa gumu. Kwa hivyo, mimi nadhani faida itakayopatikana kwenye kilimo ndio faida itakayotuwezesha sisi hapa Wazanzibari kwa sababu wananchi wengi mazao yao wangepeleka kwenye viwanda na hata na sisi tungepunguza kuagiza mazao kutoka nje au tungepunguza kuagizia matunda yanayotoka nchi za nje.

Mhe. Spika, nikija kwenye suala la uvuvi wa bahari kuu, suala hili ni la Muungano lilivyosemwa hapa kwenye ukurasa wa 26. Mhe. Spika, linasema kuwa suala la uvuvi wa bahari kuu ni suala la Muungano. Lakini naomba ninukuu kidogo kwenye hiki kifungu kinasema kwamba

> “Aidha, serikali ilitoa leseni 16 kwa wavuvi wanaovua bahari kuu, leseni 5 zilitolewa kwa mashirika ya uvuvi kutoka Sychelles, na leseni 11 zimetolewa katika mashirika ya uvuvi kutoka Spain”.

Mhe. Spika, hapa nimuulize Mhe. Waziri bado sijapafahamu, hizi leseni zilizotolewa zimetolewa katika serikali gani hii ya Zanzibar au Serikali ya Muungano.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 73 kuhusu uvuvi. Sekta ya uvuvi ni sekta mama tukiacha sekta ya kilimo, lakini sekta ya uvuvi nayo ni sekta inayoongoza hapa Zanzibar. Mhe. Spika, ukiangalia hapa katika vipaumbele vipo 6 tu hapa katika ukurasa wa 73 uliopewa vipaumbele, lakini uvuvi haukupewa kipaumbele ambapo sasa hivi uvuvi ndio sekta ya pili baada ya sekta ya kilimo. Kwa sababu sekta hii ya uvuvi ndio inayoongoza katika taifa letu.

Tunao wavuvi wengi tu hapa kwetu na sekta hii ya uvuvi haikupewa kipaumbele. Kwa hivyo, wale wavuvi wetu wanatusikiliza na sekta yao hii haijapewa kipaumbele nao bado wako katika kujishughulisha na uvuvi.

Ukiwaangalia wavuvi Mhe. Spika, hawana zana za kuvulia, vyombo vya kufikia kina kirefu cha maji, hawana hata nyenzo nyengine za kutumia. Je, Mhe. Spika, hii sekta ya uvuvi ambayo hatukuiimarisha hapa itatufikisha wapi na wavuvi wetu.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la karafuu. Baada ya miaka kadhaa mbele basi mikarafuu Pemba itaanza kutoweka. Hivi sasa mikarafuu inaanza kutoweka kwa hali ya juu. Kwanza ni kutokana na bei, ingawa serikali inasema kila siku itapandisha bei, kila siku inapandisha bei, lakini bado Mhe. Spika, bei ya zao la karafuu bado na wakulima wetu bado wana tatizo hili la kupanda mikarafuu. Kila mmoja sasa hivi hahisi hasa kama kuna zao la karafuu, kwa sababu haoni manufaa ya zao la karafuu na ukiangalia kila siku serikali inapiga kelele kwamba watapandisha bei ya zao la karafuu. Mhe. Spika, suala hili naomba lionekane.

Kwanza naomba Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri katika hii michango ya AK na JK hao wakulima wa karafuu wamepewa mikopo hii, au huu mchango wa AK na JK Mhe. Spika, kaondoka nao mwenyewe, kwa sababu tukiangalia huu mfuko wa AK na JK ni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi na kuwasaidia wakulima wadogo wadogo. Lakini hawa wakulima wa karafuu sehemu zote tu sijui kama mchango huu unawafikia. Mhe. Spika, naiomba serikali isiongeze nguvu katika vikosi tu, lakini bado iongeze nguvu katika zao hili la karafuu na kuwapa mikopo wakulima wetu ili waweze kuliimarisha zao hili.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la uchimbaji wa mafuta. Suala hili la uchimbaji wa mafuta tumelipigia kelele sana toka kwenye Baraza lililopita na tukawa na imani kubwa sana wananchi. Lakini hadi hii leo Mhe. Spika, likizungumzwa suala la uchimbaji wa mafuta basi Mhe. Waziri katika hotuba yake hii anasema Serikali ya awamu ya Saba itaendelea. sio kwamba tayari huu uchimbaji wa mafuta sasa hivi uko tayari, tegemeo letu Mhe. Waziri akisimama hapa atatuambia kwamba uchimbaji wa mafuta wakati wowote utachimbwa. Lakini hapa anasema kwamba serikali itaendelea kulipatia ufumbuzi, pamoja na kulitoa suala la mafuta katika orodha ya Muungano.

Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Waziri atakaposimama hapa atueleze hasa kakusudia nini katika suala hili la mafuta. Wananchi wetu tunalitegemea suala hili liwe tayari limeshaanza kuchimbwa, lakini kila kukicha tunaambiwa serikali itaendelea kulishughulikia, mpaka lini Mhe. Spika, suala hili litaendelea tu. Isipokuwa tupewe ukweli au serikali imeshindwa. Ikiwa serikali imeshindwa basi itueleze tu ili tujuwe moja wapo. Mimi nadhani kwa hapa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi).*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia mchana huu tukiwa katika hali ya uzima na afya.

Pili, nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi ambaye umenipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia angalau kidogo katika bajeti yetu hii.

Tatu, Mhe. Spika, nisiwe mwizi wa fadhila nimshukuru sana na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye kwa kusema kweli nimpongeze kijana huyu kwa umahiri alionao, ni kijana mzalendo ambaye anaitakia nchi yake maendeleo mazuri na kwa haraka sana. Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa bajeti yake hii nzuri ambapo kila mheshimiwa ambaye amefika hapa basi ameweza kumpongeza kwa asilimia mia bajeti hii.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, basi nichukuwe fursa hii kuiunga mkono hotuba hii ya bajeti kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo Mhe. Spika, pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dk Shein na yeye kwa ushupavu na ukakamavu wake ambaye akiwa ndiye kiongozi wetu mkuu na kwa muda mfupi sana ametuonesha njia nzuri tu ya kufikia maendeleo, pale alipokuwa akiagiza na mwenyewe kuweza kufuatilia kwa haraka sana, namshukuru na nampongeza sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mimi nianze kama wenzangu walivyoizungumza sekta ya kilimo. Ni kweli kilimo ndio uti wa mgongo wetu, ni kweli wenzetu Bara wamesema kilimo kwanza na mimi naendelea kusema kwa sababu hapa hapawezi kufanyika lolote bila ya chakula, kwanza tule hata ukienda hospitali kwa daktari basi hakuchomi sindano kabla ya kukuuliza pengine umepata angalau kikombe cha chai. Kwa hivyo, wizara hii kama ilivyojionesha katika hiki kitabu, mimi msisitizo wangu haya yote ambayo yamepangwa humu, basi tuweze kumwezesha waziri wetu wa kilimo, ambaye ni kijana mahiri anaweza kuyasimamia haya vizuri na tuweze kufikia lengo la kupata chakula, tena kile ambacho ametuletea mswada wake hivi karibuni chakula cha ziada ndani yake ili tuweze kujiwekea akiba.

Mhe. Spika, kusema kweli tukimuwezesha Waziri huyu wa Kilimo na Maliasili, basi tunaweza tukafikia maendeleo kwa muda mfupi sana hasa tukizingatia ukulima huu wa umwagiliaji maji ambao unaweza kusababisha

mavuno mengi. Tukipata mbolea na utaalamu kwa wataalamu wetu tunaweza tukavuna vizuri na tukawa kweli tuna chakula cha kujiwekea akiba.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye sekta ya utalii, ambapo katika utalii sekta hii Mhe. Spika, nia ya serikali kukaribisha utalii ni kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Kiuchumi ni pale ambapo hoteli zinapoingiza wageni basi wanalipia kodi mbali mbali za serikali. Lakini katika maendeleo ya jamii huwa tunawataka wawekezaji hawa kutoa ajira kwa wananchi wanaoishi karibu na miradi yao. Vile vile wanatakiwa kutumia mali ghafi zinazopatikana kama vile mboga mboga, samaki na matunda mbali mbali.

Mhe. Spika, kitu kinachoshangaza ukipita katika mahoteli mbali mbali, wenzetu hawa kwanza wameajiri wageni wengi kutoka Kenya na Tanzania Bara, ambapo sisi tulikuwa tukijua Wazanzibari wanaweza wakafaidika sana na utalii katika nchi yao. Vile vile mali ghafi hizo zinasafirishwa kutoka huko badala ya kuwa sisi Wazanzibari tungelikuwa tunapeleka sisi kule mahoteli basi tungeweza kufaidika sana na utalii huu.

Halikadhalika Mhe. Spika, niseme kuhusu wafanyakazi hasa wa Zanzibar, basi huwa wana matatizo makubwa katika mahoteli. Kwanza mikataba yao haiko vizuri, wanapata usumbufu wa kufukuzwa kazi mara kwa mara. Basi suala hili nimuombe Mhe. Waziri aliangalie kwa mtazamo mzuri ili wafanyakazi wetu waweze kufaidika na huu utalii ambao tumekusudia uwe unaingiza pato serikalini, lakini na kwa wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Spika, pia sekta hii pamoja na kuwa inatupatia mambo mengi ya kiuchumi, lakini bado upande wa pili kuna mtazamo nao tuutazame ili tuweze kujipanga vizuri katika sekta hii kuona tunapata faida kubwa na sio hasara kubwa.

Mhe. Spika, huu utalii hatukuuangalia katika mtazamo wa hasara zake, tuliangalia katika mtazamo wa faida zake tu. Kuna hasara pia zinapatikana. Katika ukanda huu wa utalii watoto wengi wanakosa kusoma, wanatoroka vyuoni, wanatoroka maskuli na kujihusisha katika mabiashara ya kitalii kwenda kuuza uza pembezoni mle mwa fukwe.

Pia utalii huu unaonekana kuzagaa sana mambo ya ukahaba katika mahoteli, ambayo haya yanasababisha sana maambukizi ya ukimwi ambalo ni janga kwa taifa letu. Mhe. Spika, lazima tunapokaa kupanga miradi yetu hii basi tuweze kupanga na kujua athari zinazopatikana ili tuweze kuzipatia ufumbuzi mapema, lakini tusiangalie faida peke yake.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hilo la sekta ya utalii, niende katika afya. Kwanza nashukuru sana na naipongeza sana serikali kwa juhudi zake ilizochukua kutujengea vituo vya afya mbali mbali na nyumba za daktari, lakini inaonekana kuna upungufu mkubwa wa madaktari. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili linabainika wazi hasa Mhe. Rais alipokuwa akifanya ziara katika mikoa yetu, basi katika Mkoa wa Kaskazini aliliona hili na alitoa maagizo kwa Mhe. Waziri kuweza kutuongezea wafanyakazi pale. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri ikifika wakati wa bajeti yake basi na yeye aweze kutukubalia hili kwa sababu tunasumbuka sana.

Mhe. Spika, nije katika utawala. Katika utawala pale kuna ujenzi wa maofisi hasa ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri aipe kipaumbele ofisi ile na kuweza kuiingizia fedha za kutosha ili waweze kuondokana na lile jengo la zamani ambalo ni bovu na lina hatari. Wakati wa msimu wa mvua wafanyakazi wanashindwa kuamini kukaa juu kule na baadae hushuka kwa kuhofu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aweze kutusaidia juu ya suala hili, tuondokane na jengo lile na tuweze kupata jengo lililokuwa la kisasa na la maendeleo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika sekta ya uvuvi, ambapo waheshimiwa wenzangu wameshazungumza mengi juu ya uvuvi, lakini na mimi kwa upande wangu nilitaka niwatetee wavuvi wadogo wadogo hasa kina mama wa Mkoa wa Kaskazini. Kina mama wa Mkoa wa Kaskazini na wao wanajishughulisha sana na kazi za kutanda dagaa, ni wanawake wajasiri na wanajituma kweli kweli, ningeiomba serikali iweze kuthamini michango yao hii na kuweza kuwapatia nyenzo.

Mhe. Spika, kuna wanawake wanatanda dagaa, lakini kuna wanawake pia wananunua dagaa wakachemsha wakaanika. Mhe. Spika, siku zinazokuwa za mvua wanawake hawa huwa wanahangaika sana na tatizo lile. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kuweza kuwajengea wanawake hawa au wananchi wote wa Mkoa wa Kaskazini ambao wanajishughulisha na biashara hizi kiwanda cha kuweza kukaushia madagaa yale, hasa siku zinapokuwa ni msimu wa mvua.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kuwa bajeti hii ni nzuri na imejikita kila pahali. Juzi tu kabla ya kuja hapa tulikuwa pale *Ocean View Hotel* tukipata semina ya kuja hapa. Nimpongeze Katibu wetu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alisisitiza sana kuhusu viwanda. Suala hili mimi nalipongeza na waheshimiwa wote waliosimama kulizungumza hili. Viwanda ni kweli vinaweza vikatupatia mafanikio kwa muda mfupi sana, tunaweza tukapata faida kubwa iwapo tutawekeza katika viwanda.

Mhe. Spika, nalisema hili kwa ushahidi kwa sababu mimi natokea Mkoa wa Kaskazini na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ilijaalia Kaskazini ile kukaweza kujengwa Kiwanda cha Sukari. Kwa hivyo, nalisema kwa ushahidi wakati kiwanda kile kilikuwa kikijiendesha vizuri wakati ule wa Mchina kwa hivyo niliona maendeleo yaliweza kupatikana kwa muda mdogo, yakaweza kutunufaisha watu wa Mahonda.

Mahonda ilikuwa iking'ara na sio Mahonda peke yake, kwa sababu wafanyakazi wengine walikuwa wakitoka mjini nikiwaona kwa macho yangu na wakija kule. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tuliweza kufaidika wananchi hasa wa Zanzibar, kwa sababu pale Mahonda hawapo watu wa Mahonda tu peke yao, wapo watu kutoka sehemu mbali mbali wanaishi pale. Kwa hivyo, tuliweza kufaidika na maendeleo ya kiwanda kile wakati ule kiwanda kinafanyakazi.

Tulipata faida hata wale wafanyabiashara ndogo ndogo basi waliweza kufanya biashara zao vizuri na kuwa na uhakika wa soko la kuuza. Wafanyakazi wakienda zao mashambani basi wakirudi walikuwa wanavamia biashara zao pale, waliweza kujipatia kipato cha kujiendesha kwa muda mfupi. Hata wauza maduka, maduka yao yalikuwa yakienda vizuri kwa sababu wafanyakazi walikuwa wakiyatumia maduka yake kwa kukopa au kununua bidhaa zao, baada ya kupata mishahara yao tu walikuwa wakiingia madukani, hivyo Mahonda iliweza kuonekana kuwa na maendeleo mazuri kwa muda mfupi.

La kusikitisha Mhe. Spika, kiwanda kile kipo na tunaambiwa kina mwekezaji. Hili ndio la kusikitisha sana, kiwanda kinamwekezaji lakini hatuoni anachozalisha. Tuna masikitiko kwa sababu pale sisi tunasema hatuingizi faida bali tunaingi hasara. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kulisimamia au kulifuatilia kwa umakini suala hili ili tuweze kupata ufumbuzi juu ya hili, kwa sababu kiwanda kile kikifanya kazi wananchi wetu wa sehemu mbali mbali wataweza kufaidika na ajira pale na kuweza kuipunguzia mzigo serikali kuona wananchi wake wanazubaa zubaa tu hawana kazi za kufanya.

Mhe. Spika, la masikitiko zaidi mwekezaji huyu baada ya kuzalishia sukari basi anazalisha *spirit*. *Spirit* Mhe. Spika, mimi ningesema haitupendezi au hatuitaki kwa sababu tunajua ukishalewa basi matokeo mbali mbali yanaweza kutokea, kwa sababu wanasema pombe ni mama wa maasi.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Spika, mwekezaji huyu kama kiwanda anakiweza azalishe sukari ili tupate sukari tupate na ajira, lakini kama hakiwezi ni vizuri aturejeshee wenyewe ili tutafute mwekezaji mwengine tuweze kupata maendeleo ambayo tuliyoyakusudia.

Mhe. Spika, mimi niendelee na mchango wangu kwa vijana, wanawake na watoto. Mhe. Spika, ningeomba sana vijana waweze kupata mafunzo maalum ili wapatiwe ile mifuko waweze kujiendesha na hatimaye waweze kujiajiri wao wenyewe bila ya kutegemea ajira ya serikali.

Mhe. Spika, nikija kwenye watoto, napinga sana ukatili wanaofanyiwa watoto wa kubakwa ovyo ovyo na kuwaharibia maisha yao na kuwapotezea kila kilichochao kwa huu ubakaji ambao unaonekana hivi sasa imekuwa ni tatizo kubwa sana kwetu.

Mhe. Spika, itakapofika hotuba ya Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto tutaichangia sana kwa sababu inatuuma sana hii.

Mhe. Spika, mchango wangu kwa leo hii unaishia hapa. Nampongeza tu Mhe. Waziri na namuombea *Inshaallah* kwa Mwenyezi Mungu, amjaalie kila la kheri ili bajeti hii iweze kupita. Ninavyojua kwa umahiri wake ni msimamizi mzuri, lakini hatokuwa msimamizi mzuri bali pia atakuwa mtekelezaji mzuri. Sisi tuko hapa kama wawakilishi basi kazi yetu ni kumsindikiza yeye kuona tunayasimamia vizuri yale yote ambayo tumeyapitisha hapa na tunafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, mimi na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Panya Ali Abdalla na mimi nakushukuru, hasa kwa kutetea ujenzi wa ofisi za mkoa. Lakini hasa hasa Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja. Tunaendelea. Sasa ni zamu yake Mhe. Hija Hassan Hija na baadae Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai kwa pamoja ambao tuko hapa kwa ajili ya kuchangia jambo muhimu hili kwa maslahi ya wananchi wetu na nchi yetu.

Aidha, Mhe. Spika, nikupongeze kwa kunipatia muda huu wa kuongea kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar. Napenda nitowe pongezi maalum kabisa kwa Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Omar Yussuf Mzee. Mimi namuelewa kwamba ni mtaalamu anayekubali kuelekezwa na kukosolewa. Nimelithibitisha hilo pale juzi alipoamua kutufanyia semina kwa ajili ya kuitambua bajeti nzuri na bajeti mbaya. Huu ni ujasiri, kwa sababu kwenye miaka yangu yote niliyokuwepo hapa Barazani

sijaona semina kama ile ya kuambiwa hiki ni kibaya na hiki ni kizuri. Kwa hivyo, ni ujasiri wa Mhe. Waziri na hii inatokana na utaalamu wake. Kwa hivyo, alichaguliwa na Mhe. Rais kwa kweli limesibu maana.

Mhe. Spika, nimeamua kuchangia bajeti hii kwa sababu ya kusukumwa na mambo manne muhimu kabisa.

1. Nasukumwa namaslahi ya wananchi.
2. Nasukumwa na maslahi ya nchi yangu.
3. Nasukumwa na maslahi ya Jimbo langu. na
4. Lakini kama mwanadamu nasukumwa na maslahi yangu binafsi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa msingi huo ni lazima niseme kwa kuzingatia katiba, kanuni, muongozo wa Rais na uwazi katika kufikia malengo hayo.

Mhe. Spika, nianze kabisa mchango wangu kwenye mwelekeo wa bajeti, Mhe. Waziri ametueleza kwamba mapato ya ndani kwa bajeti hii tunayozungumza itafikia bilioni 221.24 ambapo TRA watakusanya bilioni 100.58, ZRB bilioni 120.66 na ni ongezeko la asilimia 20.2 kwa bajeti hii.

Mhe. Spika, matumizi ya ndani ya bajeti hii ni bilioni 234.18 ambayo hii ni nakisi ya bilioni 12.9 au bilioni 13 ni mapungufu ya matumizi ya ndani.

Mhe. Spika, mapato mengine ambayo Mhe. Waziri ametuonesha ni hati fungate. Mwaka 2010/2011 ilikuwa bilioni 3.0 na mwaka huu ni bilioni 15.0 sawa sawa na asilimia 400. Mhe. Spika, hapa najenga wasi wasi kwamba tumeacha kukopa kwenye mabenki yetu, tumeamua kuelekeza nguvu kwa watu binafsi kwa kiasi cha asilimia 400. Maana yake ni kwamba faida itakayopatikana moja kwa moja itakwenda kwa wafanyabiashara waliokopesha. Kinyume chake kama tungekopa mabenki maana yake faida hii ingeingia ndani ya mikono ya wananchi wenyewe.

Sasa Mhe. Spika, ili kuwajibika na kuweka uongozi bora na uwazi, namuomba Mhe. Waziri angalau angetuambia basi ni wafadhili gani wa ndani waliotukopesha bilioni 15 kwa asilimia 400, ili tuwajuwe tukiwa kama wawakilishi wa wananchi. Tukishawajua Mhe. Spika, itaondosha ile dhana kuwa labda kuna watu wanatukopesha, lakini ndio hao hao ambao kuwa wanatupa ile *monopoly* ya biashara au masuala mengine.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ili kuweka uwazi kabisa, namuomba mtaalamu wetu Mhe. Waziri angalau atuambie hawa wasaidizi wetu ambao wametoa bilioni 15 za kifungate ni nani na faida yao itakuwa ni kiasi gani.

Jengine ambalo ningetaka kujua mwaka 2010/2011 kulikuwa hakuna bakaa, lakini bajeti hii Mhe. Waziri anatuambia kwamba kutakuwa na bakaa iliyoletwa ya bilioni 4. Atuambie sasa Mhe. Waziri bakaa hii ni kutoka wapi, wakati miradi ya mwaka jana ya maendeleo haikutekelezwa kwa sababu ya uchache wa fedha, lakini bajeti hii inatuambia marejesho ya bakaa ni bilioni 4 ambazo zimerejeshwa.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningezungumza ni kuhusu misaada ya kibajeti DBS ambayo ni bilioni 30.28, hii ni nakisi ya asilimia 15.2 ya matarajio ambayo ilikuwa tupate bilioni 55.24.

Mhe. Spika, nataka nirejee kwenye bajeti ya Tanzania ya mwaka huu. Tanzania bajeti yao ni trilioni 13.53 ambapo asilimia 53 ni fedha ya ndani na asilimia 47 ni mikopo na misaada kutoka nje. Sasa Mhe. Waziri atuambie bilioni 30 *GBS* ni kutokana na fungu gani la fedha kutoka nje. Kwa kweli ukipiga hesabu ni fedha ambayo ni asilimia 47 ni *trillion* karibu 7 na wala haiji kwenye asilimia hii ambayo tumeipata. Sasa labda atwambie mtaalamu fedha hii ambayo tumeipata ni kiasi gani mapato yameingia kwenye Mfuko Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Wazanzibari wakapata bilioni 30.28 ya *GBS*.

Mhe. Spika, naomba kujua pia ni nani hasa anayesimamia mapato haya, Wazanzibari wanaletewa tu au kuna kuwa na vikao gani kwa ajili ya kuratibu masuala haya ya misaada kutoka nje. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, matakwa ya kifungu cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 133 yatekelezwe.

Kwa kweli wenzangu wamesema hapa kwamba SMZ na SMT wanaendelea kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutokuundwa Mfuko wa Tume ya Pamoja wa Fedha za Nje na kufungua *account* ya fedha za nje.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba wataalamu wa fedha wanasema kwamba. "*Four percent of trillion is get billions, but ninety percent of nothing you get nothing*". Kwa hivyo, inaelekea Wazanzibari wanachukua asilimia 90 ya hapana kitu na wanapa hapana kitu na wala hawachukui ile asilimia nne ya trillion na kupata mabilioni.

Kwa manaa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili alizingatie sana na vyenginevyo itakuwa ni wimbo tu ambao tunaimba.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mapato yanapungua. Katika hili njia moja ya kupata mapato ni kupunguza safari za nje najua hili nitaeleweka vibaya pengine lakini ndio uwazi wenyewe. Kwa kweli hatuwezi kuwa na Mawaziri, Makatibu

Wakuu pamoja na Wakurugenzi ambao kazi kubwa ni kwenda nje, kwa hiyo lazima waende nje kwa ajili ya kuleta faida. *(Makofi)*

Kwa mfano, nimejaribu kufanya utafiti mdogo tu, nimeona kwamba Mhe. Rais amekwenda Turkey wakati aliporudi amezungumza na waandishi wa habari nini alikipata Turkey. Vile vile Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar alikwenda Oman na Norway na wakati aliporejea alizungumza na waandishi wa habari na ametueleza nini amekipata. Mhe. Spika, pia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alikwenda Iran na wakati aliporejea alituambia nini ambacho amekipata. Sasa iweje Mhe. Spika, Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi waende kimya kimya bila ya kutoa ripoti.

Ushauri wangu Mhe. Spika, ikiwa viongozi wakubwa wa nchi hii wanaeleza faida ya safari zao. Sasa ni wakati wa viongozi wetu wa chini kueleza pia faida ya safari zao, vyenginevyo Mhe. Spika, safari ambazo si za lazima basi ni vyema kupunguzwa.

Kwa utafiti wa haraka haraka kwa Waziri ambaye bado hajaondoka Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, nashukuru sana kwa kweli alibakia kwenye wizara yake na kufanyakazi za kuwaletea watu lishe bora ya nchi hii. Kwa hivyo, hatuwezi kuona Waheshimiwa Mawaziri wanasafiri usiku na mchana bila ya kujua safari wanayokwendea na faida yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linaongeza mapato ni kudhibiti matumizi holela. Kwa kweli wenzangu wameshasema na Ripoti ya Mkaguzi Mkuu na Mdhabiti wa Hesabu za Serikali imeelekeza ipasavyo kwamba kama serikali itapunguza matumizi holela basi mapato yataimarika.

Jambo jengine ambalo nataka kushauri ni kupunguza manunuzi ya magari ya fahari kama ambavyo Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Wenyeviti) alivyozungumza.

Vile vile kuhusu suala la kudhibiti watendaji ambao si waaminifu. Mhe. Spika, hivi sisi Wazanzibari tuna usafi wa aina gani, maana yake hakuna habari ya kusema kwamba kuna mtendaji fulani ameharibu mali za umma.

Kwa mfano, leo asubuhi nimesikia redioni kuna kiongozi mmoja alikuwa Rais leo amefikishwa Mahakamani kwa rushwa. Sasa ikiwa rais anafikishwa Mahakamani kwa rushwa, lakini Zanzibar hakuna mtu ambaye ameonekana ameharibu mali ya umma na hizi Mahakama zetu zinashughulikia waiba ndizi na nazi kule Mwera.

Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba watendaji ambao si waaminifu wadhibitiwe. Kwa kweli wapo watu ambao waamini kwamba Zanzibar baadhi ya watendaji wa serikali ni matajiri zaidi kuliko wafanyabiashara na hii ni hatari kubwa. Tunapofika hatua ya kuwa mtendaji ni tajiri kuliko mfanyabiashara ni hatari kubwa Mhe. Spika na lazima kama tuko *serious* katika kuwasaidia wananchi wetu, basi ni lazima mambo haya tuyachunguze na tuyadhibiti ili tuweze kufikia ufanisi mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo linaweza kuongeza mapato ni mafuta na gesi na hapa sitaki kuzungumzia mafuta, kwa sababu mimi kwa upande wangu sioni busara kwamba Mhe. Waziri atie kwenye hotuba yake, kwani hayo ni maamuzi ambayo Baraza limeamua na wala hayahitaji tena *story*. Kwa kweli maamuzi haya yamepita ndani ya Baraza hili Mhe. Spika na wala sio jambo la kuzungumzwa au kuandikwa kwa ajili ya kupoteza wakati wake Mhe. Waziri, isipokuwa ni maamuzi sahihi ya Wazanzibari. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninachomuomba hapa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi mwaka juzi ulitupeleka Songosongo. Kwa kweli tulikwenda na tuliviona visima vimechimbwa vya gesi na mafuta na tuliambiwa kwamba gesi ile imeanza kuuzwa miaka kumi nyuma.

Mhe. Spika, hili ni jambo la Muungano, sasa namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kuhusu mapato kutokana na gesi miaka kumi ni kiasi gani na Zanzibar imepata kiasi gani. Kwa kweli najua hii si bajeti ya kuzuia fungu, lakini natahadharisha kwamba itakapofika Wizara ya Fedha kama sijapata jibu basi sitokuwa na uwezo wa kupitisha bajeti hiyo. Kwa maana hiyo, lazima aniambie kwamba gesi kwa Tanzania tunapata kiasi gani na Zanzibar tunapata kiasi gani na hapo ndipo nitakapokuwa na kuwezo wa kumsaidia kupitisha Bajeti yake ya Wizara ya Fedha. . *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine niseme tu kwamba miradi ya maendeleo nimefanya utafiti wa bajeti tatu za nyuma. Kwa mfano, Bajeti ya mwaka 2009/2010 fedha za wahisani zilikuwa ni asilimia 13, kwa hivyo tegemezo ilikuwa ni asilimia 17, mwaka 2010/2011 wahisani walikuwa 84 Zanzibar, yaani SMZ walikuwa ni asilimia 16. Lakini bajeti hii ambayo mimi sisemi kama ni nzuri au mbaya wafadhili ni asilimia 90 na Zanzibar ni asilimia 10, sasa kama nzuri au mbaya itaonekana kwenye *calculation*.

Kwa kweli hii ni hatari kubwa kwamba tunataka kujenga miundombinu tena ya kilimo, usafiri, mawasiliano kwa asilimia kumi ya Mfuko wa ndani ni hatari kubwa. Hii tafsiri yake nini, kwa maana hiyo hakuna mradi utakaobadilika

tena. Kwa mfano, mwaka jana Mhe. Spika, barabara ya Mgagadu/Kiwani ilitengewa shilingi milioni 350 hata shilingi haikupatikana na mara hii kwa mategemeo makubwa zaidi imetengewa shilingi milioni 350, tafsiri yake hakuna shilingi itakayoingizwa. Sasa ni bajeti ambayo kwa kweli kwa mtazamo wangu haitaongeza chochote kwenye miradi ya maendeleo, kwa sababu ya wafadhili kutuwekea asilimia kubwa.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu gani, tumeelezwa mwaka jana kwamba mfadhili Wizara ya Afya aliahidi kutoa chanjo na bahati nzuri alikuwa ni mwanamke. Lakini wakati anaahidi kutoa chanjo alikuwa ni mjamzito, sasa alipojifungua tu akasema hivi sasa siwezi kutoa fedha Wizara ya Afya nalea mwanangu.

Kutokana na hali hiyo, tumeathirika Mhe. Spika kwa sababu mfadhili amejifungua, sasa wafadhili wangapi watakuwa ni wajawazito. Mhe. Spika, kwa kweli bajeti hii ni tegemezi sana na kwa hivyo lazima serikali ikae itafute vyanzo vya fedha na si kutafuta ni maamuzi tu.

Kwa kweli ninahakika tukiamua leo kwamba tupige hesabu za mapato ya gesi, basi Zanzibar itapata *trillion*s *and trillions* za mapato yake, yaani ni maamuzi tu ya kisiasa bado hatujaamua. Mhe. Spika, suala hili si jambo la kutafuta wataalamu kama ikabidi Wizara ya Fedha wakae kitako, isipokuwa ni jambo la kuamua tu. Kwa mfano, mimi na Mhe. Ismail Jussa Ladhu tukae kitako tupige hesabu za mapato ya gesi tupate fedha, yaani ni jambo la ujasiri kuamua. *(Makofi)*

Lakini tatizo lipo hapa Mhe. Spika, ni ndoa za mke ndugu ukimuoa mke ndugu Mhe. Spika si hasha kukosa mtoto na wala huwezi kushtaki kwa baba mzazi, mtoto wa Ami yangu nikimshtaki nitapata nini, basi ni maudhi hayo tu, lakini hesabu iko wazi mtoto wa darasa la pili anaijua.

Kwa mfano, Mhe. Spika, na wala si hesabu ya *TIGO* kwamba 2 X 1 = 4, yaani ni hesabu iliyo wazi wazi kwamba tukae kitako Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake tufanye hesabu za gesi kwa kipindi cha miaka kumi ni kiasi gani watupe fedha zetu na wala si jambo la kutafuta maneno Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama hilo hatuwezi Ilani hiyo nzuri ya rangi ya kijani haitotekelezeka au ile Ilani nzuri ya rangi nyekundu ya CUF haitotekelezeka na itakuwa ni hadith tu. Kwa kweli mimi namuamini Mhe. Waziri kwa sababu alikuwa Mbunge na anajua masuala ya fedha na alikuwa *TRA* na leo Waziri wa Fedha, atueleze tatizo nini Mhe. Spika. Hivi kuna mtu anaogopwa atatupiga au atatufunga. Nadhani ni jambo la kuamua tu leo na wala si kesho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze hapo ni kuhusu maslahi ya wafanyakazi wetu. Kwa kweli nimejenga hofu kwamba kwa mujibu wa marekebisho ya Katiba mpya maslahi ya wafanyakazi sasa yatashughulikiwa na Tume ya Utumishi wa Umma, hata ile Tume ya Mahakama, Vikosi na ile ya Baraza la Wawakilishi wanapeleka mashauri yao kwenye Tume ya Utumishi wa Umma.

Taarifa ambazo ninazo hadi hii leo watumishi wa Baraza la Wawakilishi hawajazingatiwa maslahi yao na asubuhi Mhe. Waziri aliniambia kwamba watazingatiwa, sasa lini. Mhe. Spika, ikiwa mimi leo napitisha Bajeti ya Serikali nasikia tayari imetajwa kwamba hii ndio *figure* ya mshahara watazingatiwa lini Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba suala hili tupatiwe ufafanuzi wakati atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho, ili tusiwe tunazungumza maslahi mengine na tukawaacha watendaji wetu muhimu ambao ndio wanaoturahisishia sisi kufanyakazi.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye hotuba hii Mhe. Waziri amezungumza kuhusu suala la kuanguka kwa bei ya karafuu. Mhe. Spika, nimefanya utafiti mdogo hapa nilipo kwenye mtandao hadi dakika hii ninayozungumza bei ya karafuu kwa Soko la Dunia ni dola elfu 8 hadi 8500.

Kwa maana hiyo, kwa kilo ni dola 8 na nusu kwa Tanzania shilingi ni elfu 19 kwa pichi. Sasa hivi ni kweli mlamagendo akubali shilingi 5,000/= za SMZ au akubali 12,000/= za Kenya na hesabu hiyo haina matatizo Katibu Mkuu mtandao upo unaweza kuangalia tu ni dola elfu 8500 kwa tani moja kwa pichi ni shilingi elfu 19.

Vile vile nimepiga simu Pemba nimeambiwa leo bei ya walanguzi wananunua pichi shilingi 12,000/=, yaani unagongewa mlango. Sasa ni nani atakayechukua karafuu zake na kupeleka Shirika la *ZSTC*. Kwa kweli na hapo kuna siri gani hasa serikali isiongeze bei, isipokuwa nina wasi wasi kwamba msitu huu wa bei ndio unaofanya watu kudumazwa na wala siamini kabisa kuwa bei ya karafuu imeshuka kiasi hiki ambacho serikali inashindwa kuongeza bei ya kilo ya karafuu.

Mhe. Spika, kwa sababu wenzangu wamezungumza mengi basi niseme tu kwamba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo namuamini sana, kwa hiyo naomba majibu ya gesi kiasi gani tumepewa, ili tumsaidie kwenda mbele na ikiwa atashindwa Mhe. Saleh Nassor Juma alisema kwamba sitaki ajivue gamba, lakini atuambie na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ikafanye utafiti huko Dar-es-Salaam na tujue tatizo nini.

Kwa hivyo, hatuwezi kujadili mapato na wala hatuwezi kuwafukuza watu kwa sababu ya parking shilingi 250/= tukiacha mabilioni ya fedha za gesi ambazo tunazo. Mhe. Spika, ni haki yetu kwenye Katiba pamoja na hata kwenye kitabu kitukufu cha *Quraan* cha Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mchana huu kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ambayo iko mbele yetu.

Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa bajeti hii, ingawa yamo mapungufu madogo madogo, lakini alikuwa mahiri na kuwasilisha vyema. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri amelipa Baraza hili hisia fulani kuwa yeye ni mzuri tena ni mtekelezaji. Lakini dhana kama hili nilipata mwalimu wangu mmoja aliniambia hisia ya mwanzo yoyote unayoipata kwa mtu, basi hisia hiyo ni mbaya, nataka Waheshimiwa Wajumbe wenzangu mnifahamu vizuri.

Kwa mfano, hisia yoyote unayoipata kwa mtu hata kama ni nzuri basi hisia hiyo ni mbaya, maana yake ni nini. Kwa hiyo, hapa kila anayesimama anamsifu mpaka na mimi mwenyewe kuwa amefanya vizuri kwenye shughuli hii.

Kwa hivyo, mwaka hadi mwaka watu wataendelea kumuona hivyo, sasa wakati atakapojeuka na kumuona vyengine, basi kwanza watu watakuwa wagumu kuamini hivi ni kweli Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo amegeuka, kwa nini kwa sababu huku nyuma ameshawagenga kuwa yeye ni mzuri.

Sasa watu watapata tabu kuamini kuwa amegeuka na tutakapoona amegeuka basi tutaona oo! Ubinadamu umempitikia. Kwa mfano, mtu leo ni Sheikh mzuri na kesho tunaambiwa ni mlevi mkubwa, kama vile Sheikh X ni hivi sasa anaanguka barabarani na wanawe wanamuokota, watu wanaomjua watakuwa wagumu kuamini kwa nini, kwa sababu ile hisia uliyoijenga mwanzo imewadumaza akili zao.

Kwa hivyo, *first impression you get is always bad*. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri amejenga hisia hiyo, basi abakie hapo tulipomuweka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze utangulize kwenye ukurasa wa 6 kuna maelezo mengi yaliyoelezwa na hatimaye ukasema kwamba Lengo la Bajeti ni Kukuza Utalii, Kuimarisha Sekta ya Elimu, Uhakika wa Chakula na Kuwajengea Wazee

Mazingira Mazuri ya Kuishi. Kwa mujibu wa maelezo ya mengi yaliyotoka huko nyuma, lakini *conclusion* yake ndio haya mambo niliyoyasema hapo juu.

Sasa ikiwa hayo ndiyo malengo basi bajeti bado ina malengo mafinyu mno. Kwa mfano, Kukuza Utalii, Kuimarisha Sekta ya Elimu na hali kadhalika Uhakika wa Chakula na haya nitatoa ufafanuzi huko mbele wakati nikiendelea na mchango wangu.

Nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 10 kuhusu ongezeko la idadi ya watu kutoka milioni 1.18 mwaka 2009 hadi kufikia milioni 1.21 mwaka 2010 na hili tumeambiwa kuwa ni ongezeko la asilimia 3.1 na hii ni idadi kubwa ya ongezeko. Mhe. Spika, kwa mawazo yangu watu tunaongezeka kupitia nyanja mbili tofauti, kwa sababu tunaoana na kuzaana na nyengine uingiaji wa watu ambao wanatoka nchi nyengine na kuingia hapa kwenye visiwa vyetu ikiwa kihalali au vyenginevyo.

Mhe. Spika, zaidi Kisiwa cha Unguja hapa Mjini kwa kweli kama ingekuwa mtu anayekula basi tungesema ameshavimbiwa, yaani *population* imekuwa kubwa mno kuliko uwezo wa mji wenyewe. Kwa kweli wengi hawana shughuli maalum za kufanya ndio maana huwa yanatokea matatizo mbali mbali hapo.

Kwa hivyo, ongezeko hili linakuja kwenye ongezeko la kipato cha Mzanzibari. Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Waziri inatuonesha kuwa mwaka 2009 wastani wa kipato cha Mzanzibari kilikuwa ni shilingi 728,000/= na imeongezeka hadi kufikia shilingi 783,370/= mwaka 2010. Kwa maana hiyo, ongezeko hili ni sawa kwa mwezi shilingi 6,656.667/= kwa mwaka 2009 na shilingi 65,780.833/= kwa mwezi kwa mwaka 2010. Mhe. Spika, hii ni sawa na shilingi 2,160/= kwa siku na huo ndio wastani wa pato la Mzanzibari.

Sasa tumtazame Mzanzibari wastani wa pato lake ni shilingi 2,000/= kwa siku moja na kuna wengine hizi hawazipati, ingawaje wako wengine wanapata zaidi ya milioni na huu ndio wastani. Kwa hivyo, tumchukulie mtu wa kawaida katika hali ya maisha ya nchi hii yalivyo wastani wake ni shilingi 2,000/= na wakati mwengine hazipati.

Mhe. Spika, miongoni mwa watu wanaoishi katika hali ya kiajabu ajabu ni sisi Wazanzibari kwamba tunatumia zaidi na wala hatupati kitu na tunaishi, yaani tunapata kidogo na tunatumia sana, sasa hiki cha ziada tunakitoa wapi, mimi mwenyewe sijui tunakitoa wapi. Kwa kweli wengi wetu tunatumia zaidi kuliko kile kipato chetu na hii ni hali ngumu tena ya hatari kuwa mtu anatumia zaidi ya anachokipata.

Mhe. Spika, tumekizungumza kilimo kuwa ni sekta moja wapo ambayo itatukwamua kwenye hali mbaya hii ya maisha yetu. Hivi sasa kilimo kinakua mwaka hadi mwaka, lakini pamoja na ukuaji wa kilimo bado hali ya chakula katika nchi yetu si nzuri.

Nadhani ni vyema nizungumzie kwetu ninakokujua watu wanategemea kulima mihogo, mpunga, ndizi. Kwa kweli kwa bahati mbaya mwanzo tulikuwa tukilima ndizi kwa wingi, lakini kutokana na hali ya ugumu wa maisha Wapemba hatuli ndizi tena na zote tunazitia kwenye meli mbovu na watu wanalala baharini zaidi ya masaa, 18 kwa ajili ya kuleta ndizi hizi kwenye kisiwa hiki cha Unguja ambako ndiko zinakotumika.

Kwa hivyo, hali ya chakula na zaidi kule ninakotoka mimi si nzuri na wala sisemi kwamba kuna njaa iliyokithiri, isipokuwa watu wanashindwa kupata angalau milo miwili kwa siku. Kwa kweli mtu anatakiwa angalau apate milo mitatu kwa siku, basi huo mmoja anaoupata ni wa kudumbukizi, yaani asubuhi anakunywa chai tupu na ile fedha anayoipata angalau aweze kupata chakula cha jioni na watoto wake.

Mhe. Spika, hii ndio hali ambayo tunaishi ingawa tunatangaza kwamba hali ya uchumi inapanda, sasa uchumi unapanda, lakini mtu wa kawaida anadidimia, yaani tunakwenda *vise versa* na mambo. Nafikiri ni vizuri uchumi unapopanda basi na hali ya maisha nayo iboreke.

Mhe. Spika, kwenye kitabu hiki takriban sekta pamoja na idara nyingi zimetajwa, lakini nilivyokipitia mimi sikuona pahala popote Sekta ya Mazingira ilipotajwa, isipokuwa mazingira imetajwa pale niliposema Kuwajengea Mazingira Mazuri Wazee ya Kuishi pale tu ndipo lilipotajwa mazingira.

Kwa kweli mazingira ni kama sekta au idara ama vyombo chengine hakikutajwa popote kwenye kitabu hiki, ingawa kwenye kitabu chengine cha kwanza mazingira yametajwa kwenye ukurasa wa 259 hadi 262 na kitabu cha pili kwenye ukurasa wa 115 hadi 119.

Pamoja na hayo Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa kwenye Baraza hili basi suala hili la mazingira alilipa kipaumbele na kilitaja kwenye ukurasa wa 27. Lakini hotuba ya bajeti kama siku-*overlook* zaidi ya pale nilipoona kuwa Kuwajengea Mazingira Mazuri Wazee ya Kuishi, basi suala hili halikutajwa sehemu nyengine yoyote, sasa sijui kwenye bajeti yake itakuja kuonekana wapi.

Mhe. Spika, takriban sote tuliosimama tunazungumzia juu ya mafuta. Kuna mfasiri fulani alikuwa akisafiri kwenye Mto Mississippi na huu ni mto wa maji baridi na walikuwa kwenye chombo, lakini baada ya kutokea dhoroba hakuja kama yuko baharini au kwenye mto, kwa hiyo alifika hapa akahisi kiu na ikawa anapiga kelele na kusema maji.

Mhe. Spika, naomba kunukuu kwa lugha iliyotumika ya Kiingereza *water, water*, basi yupo mmoja akamwambia *sink down your bucket where you are*, kwa maana zamisha ndoo yako hapo ulipo maji yapo. Sasa sisi tunasema mafuta, mafuta na yapo chini ya ardhi.

Kwa kweli suala hili tayari tumeshalifanyia uamuzi na wala hakuna haja ya kutwambia tena kama wanataka kufanya mazungumzo. Mhe. Spika, suala hili kwa sentensi yake mwenyewe kwamba hili tayari limeshafikia mahala pale na mazungumzo ambayo mimi nakubali ukafanye ni vipi, yaani ni masuala ya kitaalamu na wala sio mafuta ya Wazanzibari au laa, kwa sababu tayari mafuta ni ya Wazanzibari wenyewe ni yetu. Mhe. Spika, sisi tumeshakubali kwamba mafuta ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, uendelezo wa sentensi yako isijekuwa maelezo ya kuuza vyengine, kwa sababu hata mimi ukiniuliza nitasema ngojea, kama yapo mazungumzo mengine ni namna gani tutaweza kuyachimba na sio tunatafuta yetu au si yetu, yaani akienda kuuliza hivyo Mhe. Waziri bado atakuwa hajajiamini.

Mhe. Spika, imani yangu ni mtu mahiri, mzuri tena anajiamini, kwa hiyo sidhani kama atakwenda kuuliza kuwa ni yetu au si yetu, kwa sababu tayari anajua kuwa ni yetu na yameshapitishwa kwenye Baraza hili kuwa mafuta ni yetu Wazanzibari na wala si ya Muungano tena, yaani tumeshaachana na Muungano kwa suala hili. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu kuhusu Sekta ya Elimu. Kwa kweli hii ni sekta kubwa ambayo ni pana tena yenye matatizo makubwa sana. Lakini mimi binafsi mambo haya nataka nije niyazungumze kwa kina kwenye bajeti zao husika.

Mhe. Spika, nishati au umeme tulionao tunategemea kwa wenzetu Bara. Kutokana na hali hii tunavyokwenda inaonesha kwa kiasi fulani kwamba umeme ule bado hautoshelezi. Lakini sisi tunasema kwamba tumepata umeme wa uhakika kutoka kule. Kwa hivyo, hata kama ingelikuwa sisi basi hatuwezi kutoa msaada au kuuza kitu ambapo sisi wenyewe bado hakijatutosheleza. Kwa manaa hiyo, ndio kila mara kwa mara kuna huu mgao kwa sababu kitu chenyewe hakitoshi na sisi lazima tupate.

Mhe. Spika, ushauri wangu kama ilivyopendekezwa kwamba umeme wa kutumia nguvu za jua pamoja na upepo utumike kwa pande zote mbili za visiwa vyetu. Kwa mfano, sisi kule Pemba tunategemea umeme kutoka Tanga pamoja na kwamba leo hatuna matatizo. Lakini katika uendeshaji wa kitu uzuri wake ilikuwa tuwe na kitu cha akiba.

Mhe. Spika, leo sisi hapa kama umeme utazimwa ghafla basi Mhe. Spika utaahirisha Baraza hili, kwa sababu hatuna kitu cha akiba. Kwa kweli tumejenga tabia mpaka tumalizikiwe au tuharibikiwe ndio tufanye nini. Kwa mfano, mara kadhaa hapa tumeahirisha Baraza kutokana na uzimwaji mfupi tu wa umeme. Sasa kama tungekuwa na *generator* la akiba linaloweza kutoa huduma kwa jengo hilo, basi ingekuwa Baraza hatuahirishi.

Kwa hivyo, kama tutajenga vyanzo vyengine vya umeme na pale inapotokea upungufu kule ambako tunakotegemea, basi shughuli zetu zitaendelea kama kawaida. Kwa maana hiyo, tuache hii tabia ya kusubiri hadi tugonge ndio tuzinduke. Mhe. Spika, nadhani ni vyema tuzindukeni na tuandae kabla ya kugonga.

Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu Sekta ya Mawasiliano. Kwa kweli mawasiliano inachukua juhudi kubwa tena nyingi zaidi ya kujenga barabara Unguja na Pemba na zaidi nitakuja kuelezea wakati wa bajeti ya wizara husika. Lakini ni vizuri wizara ichague kampuni pamoja na wahandisi ambao si wa kubabaisha, yaani watu wawe na taaluma kuhusu ile shughuli yenyewe.

Kwa mfano, wakati mwengine barabara ya Mgagadu/Kiwani mwaka juzi ilifanyiwa majaribio na walikuja wataalamu sijui walitokea wapi kwa ajili ya kujenga barabara, basi iliponyesha mvua kuku walikuwa wanakufa kutokana na kunywa yale maji. Kwa bahati nzuri yule alikuwa muungwana alipoona hakufanikiwa, yaani barabara yake haikufanikiwa basi aliondoka na wala hakuendeleza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo yuko mwengine anafanya na wala hafanikiwa tena haondoki na serikali inamsifu. Lakini zaidi nitakuja kuzungumzia kwenye bajeti ya wizara husika. *(Makofi)*

Vile vile Sekta ya Afya ni muhimu ambayo ni kubwa. Kwa kweli bila ya kuwa na afya hatutokuwa na watu wa kuweza kufanyakazi na kibinaadamu mtu chochote alichonacho basi yuko tayari akitumie, kwa ajili ya kujenga afya yake tu. Kwa hivyo, tuone umuhimu wa afya pamoja na afya za watu wetu.

Kwa maana hiyo, Wizara ya Afya inahitaji kutizamwa kwa jicho la huruma sana, ili iweze angalau kukidhi asilimia 90 ya mahitaji yake. Kwa mfano, kuna

dada zetu, ndugu zetu, wake zetu wanakwenda wakati wakiwa wajawazito kwa ajili ya shughuli zao, yaani huduma muhimu za kuwahudumia huwa zinakosekana. Kwa hivyo, naomba Wizara ya Afya kupitia kwako Mhe. Spika itazamwe na bajeti hii katika fungu la huruma sana. Kwa mfano, kuna Afya ya Mama na Mtoto. Kwa kweli Wizara ya Afya inahitaji kuangaliwa kwa makini sana, ingawa mazingira hayakuzungumzwa humu. Lakini mazingira kama hatukuyapa kipaumbele basi iko siku visiwa hivi vitazama. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumekwenda sehemu mbali mbali tumeona athari za mazingira, pia namna vile zilivyoathirika ama kwa ukataji wa kuni, uchimbaji wa mchanga au vyenginevyo. Kwa hiyo, mazingira yana umuhimu mkubwa katika nchi yetu ni hii ni idara muhimu sana.

Mhe. Spika, nadhani wakati wangu umemalizika. Lakini wakati mwengine nitaomba huruma fulani, kwa sababu afya yangu ya kusema siwezi kusema kwa haraka kama watu wengine wanavyosema na ninaposema kwa haraka siwezi kufahamika, basi ndio maana ninazungumza taratibu ili niweze kufahamika. Kwa hiyo, wakati mwengine nitaomba kama ni dakika kumi basi niongezewe angalau tano, ili niweze kumaliza yake mazungumzo yangu. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha kikao kuna matangazo mawili.

Moja tunakumbushwa kwamba Mkahawa wenu hapa nyuma unafanyakazi vizuri, kama kufika nyumbani itachukuwa muda kwa kuwahi chakula cha mchana basi kinaweza kupatikana hapa hapa.

Pili na hili nilikumbushwa na Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Rashid Seif Suleiman pia naye anajua lakini hakunikumbusha, jambo hili ilikuwa tuliseme kwenye Mkutano wetu wa Pamoja wa Wawakilishi wote na sio Mkutano wa Baraza, lakini kwa kuwa nilipitikiwa na nimesahau. Kwa hivyo, naomba niitumie nafasi hii niwape hiyo taarifa pamoja na ujumbe niliotumwa.

Waheshimiwa Wajumbe, kila asubuhi na karibu kila wakati tunasikia Sauti ya Tanzania Zanzibar ikitangaza kupitia vikundi mbali mbali masuala ya kwenda Hijja. Hivi karibuni kama siku 7 nyumba Vikundi tofauti vinavyoandaa Safari ya Hijja waliitisha Kongamano ambapo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikuwa ni Mgeni Rasmi pamoja na mawaziri wengine walikuwepo kwenye mkutano huo na mimi pia nilialikwa. *(Makofi)*

Kwa kweli mkutano huo tulialikwa Wajumbe sote, lakini si wengi ambao tuliohudhuria pale. Kwa hivyo, kwa kuwa mimi mwenzenu nilikuwepo, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na baadhi ya Mawaziri, nimetumwa nikupeni salamu.

Kwanza sisi wenyewe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunashajihishwa tukumbuke umuhimu wa kwenda Hijja japo mara moja. Pili tuwashajihishe na wananchi wetu ambao ni Waislamu wenzetu wenye uwezo nao Mwenyezi Mungu akiwajaalia wapate kufanya Ibada hiyo mwaka huu pamoja na miaka mingi mbele.

Waheshimiwa Wajumbe, tuliarifiwa kwamba Viongozi wa Hijja pale Saudia Rabia wametuandalia nafasi elfu 30 kila mwaka, lakini nafasi tunazotumia labda ni elfu 3 tu. Kwa hivyo, zipo nafasi kama elfu 27 ambazo hatuzitumii. Kutokana na hali hiyo wenzetu wenye vikundi mbali mbali wanaosafirisha Mahujjaji wakaamua kufanya Kongamano na kutualika sisi Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi wa wananchi, ili tushajihike sisi pamoja na kuwashajihisha wananchi wetu tunaowawakilishi.

Naomba nivue mzigo huu ambao nilitumwa nikwambieni. Kwa hivyo, nawasilisha kwenu ujumbe huo na salamu hizo basi sisi tuwasilishe kwa wananchi tunaowawakilisha. Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kupokea salamu hizo pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, jambo jengine linalohusu Baraza hivi punde wametokea Wajumbe wengi wanaotaka kuchangia na wapo wajumbe karibu 20 ambao hawajachangia na wengi kati ya hao wamejitokeza leo hii. Kwa kweli nia na madhumuni ni kufanya majumuisho kesho jioni panapo majaaliwa na muda wetu wa kuchangia ni leo jioni na kesho wakati wa asubuhi.

Kwa hivyo, nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe, kwamba tupange points zetu vizuri nategemea karibu zote hawa tusikilize michango yao kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri. Lakini ili tumudu kuweza kuwasikiliza wote, basi itabidi sasa tupunguze muda kidogo pengine tutumie dakika 20 au hata 15, ili wote hawa tumudu kuwasikiliza kati ya leo jioni na kesho asubuhi.

Kwa hiyo, jioni ya kesho tumuachie Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya kutoa majibu ya maombi, michango, maswali na yote mengine ambayo yamezungumzwa katika kuchangia Bajeti hii ya Serikali.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa

mpaka saa 11:00 jioni)
(Saa 11.00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe Spika amenikabidhi jumla ya wajumbe kumi na saba hao ni *back bencher* hamna Mawaziri, Mawaziri wako sita kwa hivyo mtajumlisha wenyewe kupata idadi kamili, kwa hivyo tunaomba yule atakaepewa nafasi kuchangia sasa tumetoka dakika thalathini na tumeingia dakika ishirini ili hawa kumi na saba wote wapate, kesho waanze mawaziri na jioni tupitishe bajeti yetu.

Kwa hivyo nawaomba sana waheshimiwa tujali muda ili tuweze kwenda kwa mpangilio mzuri.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kupata nafasi hii jioni hii kwa kupata nafasi ya kwanza kuchangia bajeti hii ya serikali, pia nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kutuletea kioo cha maendeleo ya nchi yetu na watu wake, kwa sababu ya kuokoa muda basi mimi nitaingia moja kwa moja katika kitabu ukurasa wa kumi na nane.

Mhe. Naibu Spika, hii inahusiana na ajira rasmi hapa Waziri ametaja idadi ya waathiriwa kwa mwaka 2009 na mwaka 2010, lakini hakutaja mategemeo ya ajira katika kipindi hiki cha mwaka 2011 na wale ambao wanategemea ajira kipindi hiki cha mwaka 2011 na 2012 wako masikio wazi kusikiliza ni idadi gani ya waajiriwa mwaka huu wa 2011/ 2012 wataajiriwa, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri afafanue hili ili wananchi wetu wajenge matumaini.

Mhe. Naibu Spika, sasa naingia kwenye ukurasa wa ishirini na tisa kuhusu suala la umeme, hili ni suala nyeti sana na miongoni mwa nyenzo za maendeleo, kama tunavyoona kwamba kunakuwa na upungufu wa umeme katika visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba. Lakini nashukuru kwamba Mhe. Waziri amesema kutakuwa na ongezeko la umeme mbadala yaani umeme wa kutumia jua pamoja na upepo, lakini miongoni mwa maeneo ambayo Mhe. Waziri ameyataja ni sehemu ya Makunduchi, Matemwe na Nungwi katika kisiwa cha Unguja.

Mhe. Naibu Spika, visiwa viwili hivi vya Unguja na Pemba ni kama watoto pacha unapowavalisha nguo sare wanakuwa wanapendeza sana, pamoja na kuwa Pemba kuna umeme unaotoka Tanga lakini tukipata umeme wa ziada ni vizuri zaidi. Tunamuomba Mhe. Waziri hili aliangalie ili wananchi wa Pemba

na wao wajisikie kwamba katika mtandao huu mpya wa umeme nao wameingia.

Mhe. Spika, nikiendelea haraka haraka ukurasa wa ishirini kuhusu mishahara ya watumishi wa umeme, mimi niipongeze wizara kuangalia upya mapitio ya mishahara, mishahara hii kwa kweli inaweza kuwanufaisha wafanyakazi wetu kwa kiwango kizuri sana au inaweza ikakosa kuwanufaisha kwa kuogopa mfumko wa bei za vyakula na vitu vyengine. Nikiangalia katika uzoefu wangu hapa Zanzibar kuna mifumo mitatu ya wafanya biashara ambao huongeza biashara zao bei, kwanza ni kupanda kwa mishahara na wafanya biashara sasa hivi wanasikiliza wanaweza kuongeza bei za vyakula na huduma nyengine.

Sababu ya pili ambayo huwafanya wafanyabiashara kuongeza bei za biashara zao ni msimu wa mazao ya karafuu, na msimu wa tatu ni msimu unaokaribia sikukuu. Kwa maana hiyo Mhe. Waziri mimi namuomba pamoja na ongezeko hili ambalo litatajwa keshokutwa la mishahara basi aangalie ziada ya mfumko huu wa bei, kwani mishahara hii kama kutakuwa na mfumko wa bei kwa vyakula itakuwa haujafanya kitu kwa sababu hali itakuwa ni ile ile ngumu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi wetu wa Zanzibar mimi nahisi kwamba ili kusaidia wafanyakazi wetu na kuwaondolea kero la maisha na kuwakwamua katika umasikini, kuna mfuko wa *ZSSF* ambao umeanzishwa kwa madhumuni ya kuwakomboa wafanyakazi wetu wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mfuko huu umekuwa na wanachama wa mfuko huu hawajaufaidi isipokuwa wale ambao wamestaafu kazi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri mfuko huu uwanufaishe wafanyakazi ndani ya kipindi hiki cha kazi kwa mikopo nafuu, wafanyakazi wetu wako katika hali ngumu tunawaona kutokana na hali ngumu waliyokuwa nayo wafanyakazi wetu hawa wanashindwa hata kujiendeleza kimajengo, kujiendeleza huduma za kusomesha watoto na matibabu, wanashindwa hata kupata makaazi ya bora.

Kwa mantiki hii kwa kuwa wafanyakazi wengi wana malipo madogo yanakimu labda mlo wa chakula kimoja tu, namuomba Mhe. Waziri awape matumaini wafanyakazi wetu kuutumia mfuko huu kwa mikopo nafuu ili wajikwamue katika matatizo ambayo yamewakabili.

Mhe. Naibu Spika, jengine niende katika vipaumbele vya bajeti, ukweli vipaumbele vya bajeti vimetajwa vingi lakini kwa sababu ya kuokoa muda nataka nivitaje viwili tu na mimi kutoa mchango wangu, kwanza Afya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli afya ni miongoni mwa nyezo kubwa ya maisha ya mwanadamu katika utekelezaji wa shughuli zake za kila siku, bila ya afya binaadamu hawezi kufanya lolote na kuwa na mwelekeo wa kutosha kwa

udhaifu wa afya yake, sasa hapa nashukuru kwamba serikali imeamua kuboresha suala hili la afya.

Pamoja na kuzipandisha daraja baadhi ya hospitali zetu ikiwemo Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, namuomba Mhe. Waziri aangalie jengo la Mnazi mmoja ni jengo ambalo limejengwa miaka mingi sana wakati huo idadi ya watu ilikuwa ndogo ukilinganisha na sasa. Kwa mantiki hii nakusudia kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha aweke miundombinu madhubuti juu ya kuziboresha hospitali za Mikoa na Wilaya ili kuzipunguzia idadi kubwa ya watu wanaohitaji huduma pale katika hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja, kuziwezesha hospitali hizi za wilaya na Mikoa basi kutaipunguzia msongamano kwa kiasi kikubwa hospitali hii ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika kipaumbele cha pili ni suala zima la kuboresha elimu, katika bajeti yake Mhe. Waziri amesema ataimarisha ubora wa elimu kwa kupunguza tatizo la uhaba wa madawati, vifaa vya maabara, vifaa vya kufundishia na kumaliza madarasa yaliyoanzishwa na wananchi katika maeneo yao, mimi nashukuru sana kwa hili kwa sababu na mimi katika eneo langu limenigusa kuna madarasa ambayo yameanzishwa muda mrefu niyazungumza katika bajeti ya Wizara ya Elimu.

Lakini namuomba Mhe. Waziri wa Fedha ajue kwamba kuna uhaba mkubwa wa walimu katika maskuli yetu ya Zanzibar hasa maskuli yaliyopo vijijini, kwa mantiki hii ni kwamba katika bajeti iangalie vyema waajiriwa kuna walimu wetu wengi wameshamaliza masomo ya ualimu ngazi ya cheti na diploma hivi sasa wapo hawajaajiriwa. Kwa hivyo namuomba hili aliangalie kwa kina ili ule upungufu wa walimu nao katika maskuli uondoke kabisa, kwa sababu kuweko kwa madarasa mengi lakini kukiwa na upungufu mkubwa wa walimu itakuwa hatujaondoa tatizo lakini itakuwa tumebakia katika tatizo la muda mrefu.

Mhe. Spika, katika elimu kuna mrundikano mkubwa wa wanafunzi katika madarasa, darasa lina wanafunzi wasiopungua thamanini na kuendelea kwa hivyo kuajiriwa kwa walimu kutasaidia sana punguzo hili la idadi kubwa ya wanafunzi madarasani.

Vile vile nazungumzia kuhusu suala zima ambalo wamelizungumza baadhi ya wajumbe wenzangu hapa ingawa ulisema kwamba mada zilizokwishakuzungumzwa zisigusiwe lakini mada zote zimezungumzwa na itabidi tuzipitie hizo hizo, kuzitia nyama na sisi kuzichangia katika bajeti. Nazungumzia kuhusu habari ya uchimbaji wa mafuta.

Katika ukurasa wa arubaini na sita kuna maelezo ya ndani ya kitabu yanasema hivi naomba kunukuu.

“Mhe. Spika, katika suala la kuimarisha na kuibua vyanzo vipya vya mapato serikali inaendelea na juhudi za maandalizi ya uchimbaji wa mafuta na gesi kwa upande wa Zanzibar, kufuatia maamuzi yaliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimae kupitishwa katika Baraza lako tukufu juu ya kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika orodha ya mambo ya Muungano”.

Halafu kuna sentensi ya pili inasema naomba kunukuu:

“Serikali ya awamu ya saba itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kulipatia ufumbuzi wa pamoja wa kulitoa suala la mafuta katika orodha ya mambo ya Muungano”

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nina utata kwa sentensi ya kwanza kwa sababu Baraza la Wawakilishi la serikali ya Awamu ya sita imeshalizungumza suala hili la mafuta kwamba ni mali ya Zanzibar, lakini sentensi ya pili inazungumza kwamba serikali ya awamu ya saba itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Sasa namuomba Mhe. Waziri hili atufafanulie ili kupata uelewa tosha juu ya kauli ya awamu ya sita na hii awamu ya saba ambayo bado tunahitaji tushirikiane na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa una wachangiaji wengi watafuata badala yangu mimi nasema kwamba naunga mkono hoja na nakushukuru sana kunipa nafasi hii ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ambayo itaniwezesha kuchangia bajeti ya Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Spika, kwanza kabla ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuweka hapa leo tukiwa hai na wazima, tukiwa na busara nyingi, tukiwa na uvumilivu mkubwa.

Mhe. Spika, la pili nampongeza sana Mhe. Waziri kwa bajeti yake ambayo imekuwa na umahiri mkubwa na utaalam ambao leo karibuni kila mzungumzaji aliyekuja hapa amekuja na pongezi hizo. Mhe. Waziri nakupongeza sana na nawapongeza watendaji wako wote ambao wameshirikiana na wewe katika kutekeleza suala hili la maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi bajeti hii imenifurahisha sana na kwa sababu bajeti ambayo imeibua changamoto, lakini vile vile bajeti ambayo imetoa mikakati ya kuweza kukabili changamoto hizo, bajeti hii imebeba maeneo yote mimi

naweza kusema bajeti hii ni polisi kwa sababu imechukua nyanja zote haikubakisha kitu.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja naanza katika ukurasa wa sabiini na moja ambao unaelezea hatua ya kuimarisha usimamizi wa matumizi, hapa tumeelezewa vipi Waziri pamoja na wizara yake watashughulika katika kuhakikisha kwamba matumizi yanasimamiwa vizuri au kwa karibu, amesema kwamba atafuatilia kwa karibu misaada ya kibajeti ambayo inatarajiwa kwa mwaka ujao ili kuepusha athari za bajeti. Nafikiri mimi naungana na yeye mia chini ya mia kwa sababu bila ya bajeti hii tunaona bado tuko tegemezi bila ya bajeti hii mambo yetu yatakuwa magumu, kwa hilo namuunga mkono Mhe.Waziri.

Vile vile ametuhakikishia kwamba atasimamia au Wizara yake itasimamia vizuri ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na matumizi yake, hapa mimi nasema tuna tatizo na tatizo lipo katika makusanyo ya mapato ya ndani, tatizo kubwa ni kwamba bado hatujaweza kukusanya mapato ambayo yatatusaidia katika kukidhi mahitaji yetu, mapato tunayo lakini mapato yale yanaingia katika mifuko ya watu kumekuwa hakuna udhibiti wananufaika watu wachache, kuna wananchi ambao ni wafanyakazi, waalim, kuna madaktari ambao wako katika huduma muhimu ambazo tunazihitaji kila siku na tunahitaji huduma hizo kwa ajili ya maendeleo yetu. Lakini bado hizi taasisi zinavujisha au ofisi wenyewe tunaziachia hizi taasisi watu wachache wanasababisha kuvuja mapato hayo na matokeo yake tunaishi katika umasikini.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri chonde chonde aliangalie suala hili kwa makini na sisi Baraza la Wawakilishi tutahakikisha kwamba atutafanya nae kazi bega kwa bega, mapato yapatikane ili umasikini nchi hii uondoke wananchi wamechoka jamani tuwaonee huruma wananchi wetu, kama walivyosema wenzangu kwamba imefika hadi wengine mlo wa siku moja ni matatizo sasa kwa nini tuwaachie wengine, sasa tuna huruma gani hapa hebu tu-*balance* huruma iko kwa huyu anayekosa kabisa au huyu anayenufaika zaidi.

Mhe. Waziri amezungumzia usimamizi wa mikataba baina ya serikali na sekta binafsi hapa mara nyingi tunakwenda *wrong*, kwa sababu inapokuwa mikataba ile mibovu matokeo yake badala ya kuendelea tunaharibikiwa na tumekuwa tukifanya makosa hayo mara kwa mara, mimi Mhe. Waziri nafikiria umefika wakati sasa hivi wa kuwa na vyombo maalum na kama vipo basi havifanyi kazi tutafute chombo ambcho kitaweza kufanya kazi na ningeliomba hata wawakilishi wawemo ndani ya chombo hicho, ili kuhakikisha kwamba mikataba katika nchi hii iwe mikataba halali na mizuri kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hiki pia kuna kuimarisha utaratibu wa upatikanaji wa bajeti zetu halisi zaidi kuliko kutoka katika sekta, haya ni wazi tunamuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba hapa anapatilia nguvu.
Kipengele cha mwisho kabisa kimesema kuwe na utaratibu mzuri zaidi ya kulipa mafao ya likizo kwa watumishi wa serikali, wakati sisi tulipokuwa tunaanza kazi tulikuwa tunanufaika sana kwa mafao haya leo hii wafanyakazi wa serikali hawapati pesa zao za likizo, tunawaonea pato chao ni kidogo lakini hata hizo pesa za likizo pia hawapati. Kwa kweli tunawaonea Mhe. Waziri nakuomba uwaangalie kwa jicho la huruma wafanyakazi wa serikali walipwe maposho yao ya likizo, nafikiri na Mhe. Waziri wa Utumishi ananisikia vile vile tufanye vyovyote tuhakikishe kwamba watu hawa haki zao za msingi wanazipata. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya hapo nimefurahi sana kwa Mhe. Waziri kutuelekeza katika maeneo ambayo ameyapa kipaumbele, maeneo yenyewe ni muhimu sana katika jamii yetu kwa sababu tunayategemea yote na maeneo yenyewe leo mimi nitazungumzia maeneo mawili makubwa, haya mangine hayanihusu lakini kwa kuwa nimesikia kwamba muda hautoshi basi naomba Mhe. Naibu Spika, unipe nafasi angalau katika maeneo haya mawili niyazungumzie.

Mhe. Naibu Spika, serikali imejikita katika kuhakikisha kuwa tunapata afya bora, kwa kupata huduma ambayo itakuwa inatolewa na rasilimali watu lakini vile vile serikali itahakikisha kwamba inatupatia vifaa ili tupate huduma. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya ni wizara muhimu sana lakini imekuwa na changamoto kubwa, moja ni kwamba bajeti yake maisha inakuwa ni ndogo haitoshelezi kuna sababu nyingi, tunazaana sana haraka haraka mpaka kufikia uwezo wake kuwa mdogo, hatuwalipi mishahara vizuri wahudumu wa afya. Kuanzia kada ya daktari mpaka msafishaji lakini vile vile na vifaa pia hatuna inasikitisha wakati mwengine hata gozi unakwenda hospitali hamna.

Mhe. Waziri mimi nafikiri umeshafika wakati tunajua kwamba saa nyengine unafika wakati wizara zinakuwa hazipewi zile kasma zake ambazo inatarajia kwa vipindi, tunaomba wizara hii itizamwe sana kila ikifika wakati wa kupewa kasma yake ipewe ili itoe huduma kwa wananchi, hakuna sababu katika wizara hii tusitie dosari yoyote tunataka kupunguza vifo vya akina mama. Wenzetu nchi zilizoendelea kusikia mwanamke mzazi au mjamzito kafa kwa mwaka mzima pengine ni kesi moja tu, sisi mzazi akienda hospitali anashahadia kwamba unaweza kupona au unaweza kutangulia mbele ya haki. Hili ni tatizo tumejaribu kulipunguza lakini twende kwa kasi sasa hivi umeshafika wakati kwamba na sisi basi tuhakikishe kwamba afya ya mama na mtoto inalindwa.

Mimi sasa nataka kuzungumzia elimu nashukuru kwamba moja katika sekta ambayo imepewa kipaumbele ni elimu, tuna elimu ambayo nashukuru kwa sasa hivi watoto wetu kwa asilimia kubwa wanahamasishwa wanakwenda skuli, lakini mimi wasi wasi wangu ni ubora wa elimu yetu imekuwa ikianguka siku hadi siku tunasema tuna wanafunzi wengi wanaojiandikisha lakini bado ubora wa elimu ni changamoto kubwa kwetu sisi. Nimeona mipango ni kuhakikisha na kuongeza kiwango cha elimu katika sayansi, jografia, hisabati na katika kiingereza lakini mimi nasema hata katika Kiswahili. Kwa sababu Kiswahili ni lugha yetu lakini ikifika wakati wa mitihani watoto wetu wanafeli ukweli ndio huo kwa hivyo na Kiswahili nacho tukitie vile vile, si kwa sababu tunaweza kusema lakini tunaizungumza, lugha ya Skuli inakuwa mara nyingi maana yake panataka ufasaha ndani ya lugha hizi.

Mhe. Naibu Spika, kubwa nahisi elimu imekuwa na changamoto kwa sababu ya walimu wetu, mara nyingi tunawaacha muda mrefu bila ya kuwapa mafunzo ya elimu. Mwalimu anaweza kukaa kipindi kirefu miaka miwili, mitatu hajapata *refresher course*. Hiyo inasababisha kwa sababu elimu kila siku inakuwa na inabadilika na sisi tuwe na tabia hiyo.

Mhe. Waziri nakuomba Wizara ya Elimu uione au taifa haliwezi kuwa bora. Taifa haliwezi kuendelea bila ya kuwa na elimu. Tunahitaji wataalamu Wazanzibari, tunaingia katika soko la Afrika Mashariki. Tunataka watoto wetu wawe *competitive*, waweze kuingia kutafuta kazi katika soko hili. Leo tunanyanyaswa hapa hapa kwetu wanakataliwa, wanakwenda katika mashirika mbali mbali, kwa sababu pengine hajui kujielezea kwa kiingereza. Hii ni aibu!

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kusema kwamba humu katika Bajeti hii ni pahala padogo sana pamezungumzia elimu kwa walemavu. Elimu kwa walemavu ni muhimu. Tuna walemavu ambao wanao uwezo wa kusoma na kufanya kazi na kuwa raia ambao wataweza kusaidia katika maendeleo yetu. Lakini bado hatuwatizami kwa jicho hilo.

Mhe. Waziri naomba katika masuala yote ya elimu lakini tusiwaache mkono walemavu, wana kila aina ya haki katika nchi hii.

Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Spika, suala la huduma za maji limekuwa ni kero kwa nchi nzima. Tumeshazungumza sana, watu wengi wamezungumza lakini na mimi naona bora nitie baraka zangu kidogo. Maji ni tatizo, namjua Mhe. Waziri wa Maji atafanya vizuri. Nashukuru kwamba yeye ndiye aliyepewa wizara hii, namuamini kwamba atafanya vizuri. Safari hii hebu tuhakikishe malengo yetu yamefikia, ili watu waseme kwamba sasa kweli tuna serikali.

Mhe. Naibu Spika, hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa imewapa matumaini wananchi wote wa Zanzibar. Tusiwatoe katika matumaini hayo, maji ni msingi. Wanawake sisi tunapata tabu sana kwa sababu hakuna maji. Muda wetu wa kukaa jikoni na kufanya shughuli za nyumbani zinazidi, mababa mtatukimbia! Badala ya kukaa jikoni inabidi atoke akachote maji mbali, akafanye shughuli zote mbali. Tunamuomba waziri Wizara ya Maji uipatie fedha za kutosha kwa wakati ili kuhakikisha kwamba maji wananchi wanapata.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Naamini kwamba bajeti hii utekelezaji wake utakuwa ni mzuri. Namuombea dua Mhe. Waziri wa Uchumi na Fedha Mungu amjaalie kijana wetu afanikishe azma yake na Mungu aijialie serikali hii ifanikishe azma yake. Mungu atujaalie amani na utulivu na upendo nchini mwetu.

Baada ya hapo napenda kuchukua nafasi hii kusema kuwa naunga mkono bajeti hii asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi hii kuichangia bajeti hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia neema ya uhai na uzima tukawa wakati huu tunakutana hapa na kujadili bajeti hii ambayo inaongozwa na Alhaj mtarajiwa Shekh Omar Yussuf Mzee, kwa baraka za Mwenyezi Mungu zitakuwa tena.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wote waliompongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutuonesha kwamba Zanzibar tunao watu wenye uwezo ambao wanaweza kututoa hapa tulipo na tukaelekea kwenye maendeleo. Nadhani ni muda mrefu sana Zanzibar tulikuwa na kiu ya kupata Waziri wa Fedha mwenye uwezo kama tulivyonaye leo Mhe. Omar Yussuf.

Mhe. Naibu Spika, nilibahati kule Bungeni muda mfupi sana mwaka jana na najua jinsi gani uwezo wa Mhe. Omar ulivyokuwa ukisaidia katika Bunge kuwasaidia ndugu zetu wa Bara wanaongoza Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kuwapa muelekeo na kuonesha kwamba kumbe Wazanzibar nao vile vile wanaweza, kwa hivyo nampongeza sana kwa hilo.

Baada ya kumpongeza naomba niseme na mimi kwamba naiunga mkono bajeti hii ambayo ameiwasilisha, nikitambua kwamba yapo mapungufu ambayo yapo nje ya Mhe. Waziri wa Fedha kuweza kuyakamilisha. Tungependa sana tukawa na bajeti ambayo ingekidhi mahitaji yetu yote. Lakini kwa sababu ya hali halisi ya uchumi wan chi yetu ilivyo hivi sasa, nadhani kwa hali ilivyo hivi sasa amejitahidi kadiri ya uwezo wake na bila shaka na mawazo tunayompa hapa atayazingatia ili tuweze kuifanya iwe nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kupongeza katika suala zima la vipa umbele sita ambavyo vimewekwa na bajeti hii. Kama nilivyosema tungependa sote kila sekta ikawa na nafasi kubwa. Lakini unapokuwa na kidogo unakubidi uchague, wanasema kupanga ni kuchagua. Kwa hivyo tunafurahi kwamba yametafutwa maeneo haya ambayo ni afya, elimu, maji, kilimo, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, na utafiti.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nilikuwa na maoni na baadhi ya masuala na baadaye nitatoa mapendekezo yangu. Katika masuala kidogo nimepata wasi wasi katika ukurasa wa 11 hotuba ya bajeti palipozungumziwa viwanda na mchango wake katika uchumi wan chi.

Tumeambiwa kwamba ukuaji wa sekta hiyo umeshuka kutoka asilimia 3.4 hadi asilimia 1.9 mwaka jana. Lakini hapo hapo ikaelezwa kwamba mchango wa sekta hii katika uchumi umefikia asilimia 12.6. Mimi hili lilikuwa linanipa wasi wasi, hasa nikiangalia aina ya viwanda tunavyovizungumzia hapa katika kitabu hiki cha kwanza cha mapitio ya hali ya uchumi, ambapo katika ukurasa wa 171 hadi 173 viwanda ninavyoviona hapa ni vile vinavyotengeneza mikate ya boflo na vile vinavyotengeneza bangili kule mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli napata wasi wasi kwamba kweli viwanda kama hivi vinaweza kweli kuambiwa kwamba vinachangia uchumi wa nchi kwa asilimia 12. Nilikuwa nataka niridhishwe kama kweli takwimu hizi ni sahihi na kweli uchumi wetu unachangia asilimia 12 na viwanda hivi ambavyo tumevitaja. Pamoja na kwamba kweli Wazanzibari wengi nikiwemo mimi na Mhe. Mansour tunaipenda sana mikate ya boflo lakini sikuwahi kuamini kwamba inachangia kiwango hiki kikubwa sana cha uchumi kama tulivyoelezwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, pia ningeomba vile vile maelezo katika ukurasa wa 12 hadi wa 13 unazungumziwa kupungua kwa uwekezaji katika nchi. Imesemwa hapa kwamba idadi ya miradi iliyothibitishwa kutekelezwa katika mwaka 2010 na thamani ya dola za Marekani 110. 34 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 270.92 milioni kwa mwaka 2009 sawa na upungufu wa asilimia 59.2.

Huku ni kushuka kukubwa sana Mhe. Naibu Spika, kwa uwekezaji katika nchi. Zaidi hapa nimeomba maelezo kwa sababu nikiiangalia hotuba ya bajeti haisemi sababu gani ilizopelekea kupungua kwa uwekezaji huo. Kumetajwa tu hapa kwenye ukurasa uliofuata kwamba upungufu huo wa uwekezaji umetokana zaidi katika maeneo zaidi ya usafiri na mawasiliano, huduma za fedha, ujenzi na ukodishwaji majumba ya kisasa. Lakini nini sababu

zilizopelekea kushuka kwa kasi hii ya ajabu ya hadi ya upungufu wa asilimia 59.2 ningependa kusaidiwa Mhe. Naibu Spika.

Eneo jengine ambalo ningeliomba maelezo ni ukurasa wa 16 unaohusu kushuka kwa uagiziaji wa bidhaa. Tumeelezwa kwamba kumepanda kwa *capital goods*. Kuna uongezekaji wa *intermidiate goods.* Lakini kuna kushuka kwa *consumer goods* yaani bidhaa za matumizi ya kawaida. Sasa kwa uchumi kama wetu ambao tumeambiwa tangu jana katika mjadala kwamba unategemea pia biashara. Kuanguka kwa uwagiziaji wa *consumer goods* kunaashiria vile vile watu wetu kukosa ajira.

Kwa sababu wengi wanashiriki katika biashara hizi za mikononi za reja reja za kuchukua hapa na wakapeleka katika maeneo mengine kwa hivyo tulikuwa tunaomba kusaidiwa. Je, ni sababu zipi na kama ni dudu hili la *TRA* tuelezwe ili wakati wa kulifungasha virago tulifungashe kwa haraka zaidi kuliko hivi ambavyo tulivyokuwa tukifikiria baadhi ya wajumbe wako.

Mhe. Naibu Spika, sasa nikiondoka katika maeneo ambayo nilikuwa naomba maelezo pia nataka kuzungumzia machache kuhusu baadhi ya haya mambo ambayo tumeyataja humu kama vipa umbele. Kwanza ni suala zima la sekta ya kilimo ambayo imepewa umuhimu. Tumeambiwa kilimo hapa kina maana pana kwa maana ya kilimo mifugo na uvuvi. Tulielezwa juzi katika semina kwamba hakuna nchi ambayo imeendelea kiuchumi kwa kutegemea kilimo.

Nchi zote zilizoendelea kiuchumi zimetegemea viwanda. Tuliambiwa kwamba pamoja na hayo sekta hii kubwa ya kilimo na sekta zake ndogo tatu, kwa maana ya kilimo, uvuvi na mifugo inatoa msingi wa hayo maendeleo ya viwanda katika nchi. Kwa maana ya kuzalisha bidhaa zinakuwa *process* baadaye na ndio zikawa msingi wa hivyo viwanda kuanzishwa katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, wasi wasi wangu ambao naomba rafiki yangu Mhe. Waziri akija atusaidie ni kwamba bajeti yake imewekeza huku na nimesema mwanzo naelewa kwa sababu tuna vyanzo vichache vya mapato kwa hivyo hivi tulivyonavyo hatuna budi kuwekeza hapo. Lakini nilitegemea kupata unafuu fulani kwa kuwashajihisha wawekezaji ambao wangetaka kuwekeza katika viwanda ambavyo vinahudumia au vitakuwa vinatumia bidhaa zinazotokana na sekta hizi ndogo tatu zinazotokana na sekta kuu ya kilimo.

Yenye mwenyewe alikuwa Naibu wa Fedha katika Serikali ya Muungano waliwahi kutoa vivutio maalum kwa mfano wanaoagiza matrekta, wanaotaka kuleta mashine za kutengeneza maziwa, siagi na bidhaa nyengine zinazotokana na mifugo, wanaotaka kusindika samaki. Kulikuwa na vivutuo fulani vya

kuteremsha kodi katika mashine kama hizi, bidhaa kama hizi ili kuvutia uwekezaji katika viwanda vinavyo *support* sekta hizi tatu.

Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoambiwa sekta hizi peke yake tukizitegemea haziwezi kuifanya nchi yetu ikaendelea kiuchumi bila ya kuwa na viwanda zinavyoambatana navyo. Sijui kwa kwa nini hakuliona hili au ndio kwa sababu amebinywa sana kwamba asiongeze kodi kwa hivyo hakuweza kupata nafuu pa kupunguza kodi. Ningeliomba hilo nalo pia tuweze kusaidiwa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la mapato ya nchi. Katika hili kumezungumzwa humu mapato ya ndani na mapato ya nje. Katika mapato ya ndani tunamshukuru kwa hilo. Ametwambia Waziri kwamba hakusudii kuongeza kodi yoyote na kwa hili nampongeza sana kwa kuwafikiria wananchi wetu. Si jambo rahisi hasa ukizingatia kwamba hivi sasa nchi nyingi zipo katika msukosuko wa kiuchumi, kukwepa kuongeza kodi si jambo rahisi. Lakini Zanzibar imeweza chini ya Mhe. Waziri hili linatutia moyo na nampongeza.

Lakini tuliambiwa kwamba hatuongezi kodi lengo sio tu kupanua ule wigo wa walipa kodi lakini pia ni kwenda chini zaidi kuhakikisha kwamba mapato hayavuji. Katika eneo hili nataka kumwambia waziri aliangalie sana suala zima la misamaha ya kodi. Tunashukuru katika hotuba yake ametueleza hapa kwamba katika mwaka jana amesaidia sana kupunguza na tumeona jinsi gani serikali imeongeza mapato. Lakini bado kuna maeneo ambayo yanatumiwa vibaya sana katika eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, zipo taarifa kwamba kuna baadhi ya wawekezaji hapa wamekuwa wakiomba misamaha ya kodi hasa katika biashara za mahoteli, wana hoteli Zanzibar lakini pia wana hoteli Dar-es-Salaam. Wanatumia misamaha ya kodi ya Zanzibar kuingiza bidhaa zaidi ya mahitaji ya mahoteli zao na baadae bidhaa hizi zinasafirishwa kupelekwa Bara, kuanzia vifaa vya mahitaji ya mahoteli vya ndani, magari na mambo mengine kama hayo. Tunaamini kwamba watendaji wengine wanayajua haya lakini pengine wanashirikiana na wanaokwepa kodi hizi kwa kuwapa misamaha ya Zanzibar kwenda kunufaisha uchumi wa Bara, ambao ukirudi nyuma haumnufaishi sana mwananchi wa Zanzibar. Nilikuwa naomba maeneo haya ayatizame.

Lakini sio eneo hilo tu la misamaha ya kodi pia tukiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetaja mianya mingi inayotumika kupotea mapato ya serikali. Kuna matumizi mabaya yasiyozingatia kanuni za fedha. Sina haja ya kumpeleka mbali Mhe. Waziri akiingalia ripoti hii ya Mkaguzi kwa mwaka 2008/2009 katika muhutasari tu uliokuwepo mwanzo

pale, unatajwa. Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, matumizi yasiyokuwa na vielelezo vya uthibitisho ni Tanzania shilingi mia moja thalathini na nane milioni, hamsini na tatu elfu mia mbili na saba na dola za Kimarekani 209.

Mhe. Naibu Spika, kwa nchi masikini kama yetu ni fedha nyingi kama itatumika hazina uthibitisho. Lakini utakuta kuna malipo yasiyokuwa na stakabadhi mia moja na tatu milioni, laki mbili tisini na nne elfu mia tano sabini na moja. Kuna malipo yasiyo na mikataba shilingi mia nne kumi na tatu milioni laki sita arubaini na nne elfu na tisini na saba.

Sasa nasema Mhe. Naibu Spika, kwamba inaonekana ipo mianya ambayo inatumika kupoteza fedha nyingi ambazo pengine tungeweza kuzinusuru na zikaenda kwenye shughuli nyengine ambazo zinaonekana kuna nakisi kama ilivyo hivi sasa. Nilikuwa naomba hizi ripoti zifanyiwe kazi, mapendekezo yanayotolewa humu, yanayotolewa na *PAC*, yawe yanafanyiwa kazi ili kudhibiti mianya hii na uvujaji wa mapato yaingie katika nchi yetu.

Nikitoka hapo kuna suala zima la ruzuku. Kuna mashirika haya ya serikali yamekuwa yakipewa ruzuku na yakipewa misamaha lakini yamekuwa hayaingizi na yanashindwa kujiendesha kibiashara. Namshukuru Mhe. Waziri tuliwahi kumsikia katika vyombo vya habari akiwapa onyo alipokutana nao, kuyaambia kwamba yasipojiendesha kubiashara atayafunga. Vile vile akawambia hakuna misamaha ya kodi kwa sababu yanafanya biashara yalipe kodi.

Nilikuwa naomba tamko lake hilo alilolitoa liambatane na vitendo. Tufike pahala Baraza la Wawakilishi liache kuthibitisha au kuidhinisha matumizi yanayokwenda ku *support* mashirika ambayo yanaitia hasa serikali badala ya kuiingizia faida. wenzetu wamefanya hivyo na sisi naomba tuendelee hapo.

Mhe. Naibu Spika, tumesema kwamba tunahitaji kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ili kufidia hizi nakisi tunazoziona. Tumeona katika bajeti yetu ya maendeleo Zanzibar inategemewa ichangie mapato ndani ya silimia 10, asilimia 90 inategemewa itoke kwa washirika wa maendeleo. Lakini hata bajeti ya matumizi ya kawaida pia ina nakisi ya takriban bilioni 13. Hapa ndipo tunapokuja katika masuala yanayohusu mapato ambayo ni haki ya Zanzibar lakini tunashindwa kuyatumia.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hii ametaja suala la karafuu. Ametwambia kwamba bei yake imepanda lakini ukiangalia kama dola 30 katika Soko la Dunia. Lakini Mhe. Hija alisema kwamba ukiangalia katika mtandao unakuta bei ya karafuu ya Zanzibar kwa tani ni kama dola 8500 sawa sawa na bei ya Indonesia. Bei nzuri zaidi inayotajwa mle ni ya India ya dola 11,000 kwa tani.

Ingawa sisi tunaamini kwamba karafuu za Zanzibar ndio karafuu *best* katika dunia, unakuwa unastaajabu.

Mimi nilibahatika katika kazi hizi zetu za kamati, tulipata kujua hapa kwamba serikali imepeleka wataalamu kwenda kuangalia suala zima la jinsi gani nchi zinafaidika na mfumo unaoitwa *Branding*. Yaani suala zima la kudhibiti uuzaji wa bidhaa yako ambayo ni aina ya pekee kama ilivyo karafuu ya Zanzibar.

Ililetwa kampuni ya Kimarekani inaitwa *Lightyears IP* kuja kufanya utafiti. Walichokigundua ni kwamba kilo moja ya karafuu ya Zanzibar wakati mkulima anauza kwa dola 2.34 wastan. Serikali inasafirisha nje kwa kumuuzia yule anakuja kununua kwake kwa wastani wa dola 6.06, huyu *importer* anaenunua kutoka kwetu yeye anauza kwa kilo moja ya karafuu ya Zanzibar dola 106.93 na huyu baadaye anapokwenda kuiuza kwa yule *retailer* anayekwenda kuiuza katika *world market* anauza kwa dola 178.21 kwa kilo moja ya karafuu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hizi ni fedha ambazo zingepaswa angalau nusu yake, hatusemi zote kwa sababu najua kwamba kuna magharama katika usarifu mazao haya, usafirisha, bima. Lakini tungefika pahala Zanzibar ikapata angalau dola 50 ya Kimarekani kwa Kilo na serikali ikapata nusu ya hizo na mkulima akapata nusu ya hizo, tungekuwa hatuuzungumzii umasikini Zanzibar.

Hicho naona ni kianzio kimoja cha mapato ambacho serikali inapaswa ikitizame kwa umakini kama wenzetu wa Ethiopia wameweza kahawa yao na sasa wanafaidika wakulima na serikali na nchi yao na sisi tufike pahala tufaidike na karafuu zetu badala ya kwenda kuwanufaisha watu wengine wanaonyonya jasho la wakulima wa karafuu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, wanaotunyonya jasho letu sio tu wanaokuja kuchukua karafuu zetu, hata ndugu zetu tunaowaita wa damu katika kutukwamisha katika suala zima la uchimbaji wa mafuta na wao hao wanatuzuia tusipige hatua za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chake hichi Waziri amesema kwamba Serikali inaendeleza hatua ya kuliondoa suala hili kwa mazungumzo na Serikali ya Muungano. Mimi nasema suala la mazungumzo limeshamalizika. Baraza hili tuliambiwa lilipitisha maamuzi juu ya kuliondoa suala la mafuta katika orodha ya mambo ya Muungano. Lakini hapo hapo paliamuliwa kwamba baadaye Zanzibar iunde mamlaka yake ya kusimamia kutoa leseni kwa kampuni zinazotaka kutafuta na kuchimba mafuta Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba tukingoja Serikali ya Muungano ichukue hatua ya kupeleka marekebisho ya Katiba ambayo ni ya mstari mmoja tu. Kwa sababu marekebisho ya Katiba ni kusema tu katika hii nyongeza ya kwanza yenye mambo ya muungano useme tu pale kwamba kifungu namba 15 kinafutwa, ndiyo marekebisho yenyewe yanayohitajika hayo. Lakini mpaka hii leo tunapigwa danadana tu.
Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nadhani sasa tusiingoje Serikali ya Muungano. Nadhani tuitake seriakli ya Zanzibar ipeleke rasimu ya marekebisho ya Katiba ya Muungano ndani ya mwaka huu wa Fedha. Si haramu, si kwamba katika Muungano huu siku zote marekebisho lazima yatoke upande wa Bara tu Zanzibar iwe haina haki. Na ikipeleka marekebisho iwe matokeo yake Rais wa Zanzibar anaambiwa ajiuzulu. Si lazima hivyo.

Mhe. Naibu Spika, haya ndio mawazo ya Wazanzibar. Tupeleke mapendekezo ya rasimu ya kurekebisha Katiba ya Muungano na ikiwa haikupitishwa ndani ya mwaka huu wa fedha, Serikali ya Zanzibar ijiundie mamlaka yake ya mafuta, izikaribishe kampuni za mafuta zije ziombe leseni Zanzibar, mafuta yachimbwe.

Mhe. Naibu Spika, watu walikuwa wanauliza hapa kama mafuta haya yapo? Mafuta yapo. Kampuni ambayo imeomba leseni ya kitalu Nam. 8 – 12 katika vitalu 12 vya Tanzania ni kampuni ya SHELI. Makampuni mengine yote yamegombania vitalu vyengine huku. Kampuni ya SHELI ambayo kwa hivi sasa inamilikiwa na Uingereza na Uholanzi ndio kampuni ya pili kwa ukubwa duniani katita utafiti na uwezo wa kuchimba mafuta. Hawa hawawezi wakang'ang'ania hapa isipokuwa wanajua kuwa mafuta yapo.

Lakini pia karibuni katika jarida la *Economic* linaloheshimiwa sana ulimwenguni na nimekuja na *photocopy* hapa. Ripoti inaonesha kwamba sasa utaalamu wa kuchimba mafuta umeendelea hasa katika bahari kuu, kwamba ukiweka satalaiti huna haja ya kwenda kuchimba na kujua kima chake yaliyokuwepo. Haiwezekana Kampuni ya SHELI ikawa haina utaalamu kama huo. Mimi naamini inao na imetambua kwamba mafuta haya yapo.

Tuliwahi kuambiwa na Rais wa kwanza wa Tanzania kwamba tusiwe tunao uchumi ukawa tunaukalia. Sasa namuomba Mhe. Omar badala ya kulalamika sana huu uchumi alioukalia auondoshe utufaidishe Zanzibar.

Napendekeza kwamba hatua zichukuliwe kupeleka mapendekezo haya. Ikiwa kutakuwa na ukaidi upande wa Bara Zanzibar i-*act on it on* ituletee sheria hapa ya kupitisha mamlaka, tukaribishe kampuni hizi na zitakuja Mhe. Naibu Spika, uchumi huu ufaidishe Zanzibar na watu wake.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nishukuru kupata fursa hii kuweza kuchangia bajeti hii ya mwaka 2011/2012. Pia kwa dhati kabisa na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wetu wa Fedha kwa namna alivyoiandaa bajeti kwa kushirikiana na wetendaji wake. Kila anayesimama hapa anamwaga sifa kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu amemjaalia. Hii yote inatokana na umahiri wa Mhe. Waziri wetu. Sisi wengine tunamfahamu vya kutosha. Mimi ni mwanafunzi wake wa siasa tangu mwaka 2000.

Mhe. Naibu Spika, mengi yameongelewa, lakini na sisi kama wajumbe tuna haja yakukazia kazia nati kwa yale ambayo wenzetu wameacha baadhi ya mapungufu. Mimi naomba nichangie maeneo kama matato. Eneo la kwanza ukurasa wa 71 katika suala zima la hatua ya kuimarisha mapato, katika suala la kutokupangisha kodi.

Mhe. Naibu Spika, suala la kutokupandisha kodi ni suala zuri, Mhe. Waziri ameliangalia kwa upeo sana pia ni suala ambalo imani ya wananchi walio wengi wameanza kujenga matarajio yaliyokuwa mazuri kuona kwamba safari hii hali ya wananchi katika kutafuta rizki huenda ikawa ni ya kuridhisha.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuelezea hali halisi ya kutokupandisha kodi, bado kuna haja namshauri Mhe. Waziri aangalie kwa uhalisia uliokuwa mzuri namna ya kuandaa mikakati ya kudhibiti baadhi ya wafanyabiashara wasiyoitakia mema nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi yanapozuka mambo kama haya ya kutokupandisha kodi, kuongeza mishahara basi wafanyabiashara huna wana mtindo wa kuongeza bei za biashara zao pasipo kuwaonea huruma wananchi wetu. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri akaangalia jinsi ya kuandaa mikakati au kuunda chombo ambacho kitasimamia kodi za biashara ndogo ndogo za wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba biashara yetu ni huria, lakini bado haja ya mikakati kwa wafanyabiashara inahitajika.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya pili ambayo naomba kuchangia ni ukurasa huo wa 71 katika suala zima la ukusanyaji wa mapato. Mhe. Naibu Spika, wengi wanazungumza na ndivyo hali ilivyo kwamba Zanzibar sio masikini. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ina vyanzo vingi vya mapato, pamoja na kuwa hatukutajiwa hivyo vyanzo vya mapato ni vya aina gani ambavyo serikali inakusudia kuvipa kipaumbele. Lakini ni ukweli vyanzo viko vingi na kama tutakuwa tuko imara basi nina imani kwamba mapato yataboreka zaidi, na

imani yangu kwa Mhe. Waziri tuliyekuwa naye basi awamu hii mambo yatabadilika.

Mhe. Naibu Spika, katika hili nataka nielezee angalau maeneo mawili tu ambayo yana upungufu wa ukusanyaji wa kodi katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, ukusanyaji wa mapato kwa mfano *airport* katika suala zima la uingiaji wa wageni. Mhe. Naibu Spika, taaswira ya wageni wanaoingia na kile ambacho utaelezewa katika maandiko basi unakuta tofauti, pia katika suala zima *visa* ni kwamba taswira ya hali halisi ya hapo huipati. Mhe. Naibu Spika, kama utakwenda kuyataka ndani zaidi basi utaoneshwa wageni walioingia ni 500, lakini uchangiaji hukuti katika hali hiyo, na katika vyombo vyetu vya ukusanyaji wa mapato *Income tax, ZRB* na *TRA* hawa watu wamekuwa wajanja sana. Kwa hivyo, tunaiomba serikali itafute njia mbadala ya kuangalia *format* nzuri katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, mapato yanakwenda kukusanywa kwa mfanyabiashara anaulizwa tukuandikiye kiasi gani, unamkuta mfanyabiashara kwa mfano anatakiwa alipe kodi ya shilingi arubaini milioni, hivyo anaulizwa kiasi gani tuandike. Mtu anasema andikeni milioni ishirini na tano mtachukua nyie. Mhe. Naibu Spika, kuna haja katika kuliangalia hili Mhe. Waziri akaona njia mbadala ya ukusanyaji wa mapato katika taasisi zetu. Mhe. Naibu Spika, hapa wenzangu walisema Waheshimiwa Mawaziri wasitembee sana, lakini mimi naona kuna haya ya Mhe. Waziri wa Fedha akajaribu kuzunguka duniani kuangalia ni jinsi gani wenzetu wanavyotumia utaratibu wa kukusanya kodi.

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kutafuta baadhi document za nchi moja ambayo nimetembelea nimeona jinsi wenzetu wanavyokusanya kodi zao. Mhe. Naibu Spika, kila unachokinunua basi unakuta mtiririko wa kodi umesimama katika aina moja tu, yaani ni chombo kimoja tu ndicho kinachokusanya kodi. Mhe. Naibu Spika, humo unaandikiwa kila kitu kama kuna serikali za mitaa asilimia yake kwa unacho kinunua inawekwa, kama kuna ZRB asilimia yake unachokinunua kinawekwa.

Lakini mkusanyaji inakuwa ni taasisi moja ndio inayosimamia mambo hayo kwa sababu, hii inatupelekea kwamba kuweka vyombo vingi vya ukusanyaji wa mapato ndio inapelekea kuleta hiyo mianya ya ufisadi. Mhe. Naibu Spika, ufisadi katika nchi umekuwa mwingi na kwa hili tuko tayari kumsaidia Mhe. Waziri kwani mambo yako nje nje na nina imani Mhe. Waziri atakubali kusaidiwa michango, na katika hili tuko tayari kulisimamia.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hali hii bado na serikali yetu iandae mikakati ya kuunda sheria zilizokuwa madhubuti, wengine wamesema hapa kwamba viongozi waandikiwe mali zao ili kumjua kila kiongozi ana miliki nini. Mhe.

Naibu Spika, hata hao maafisa wetu watendaji hawa ndio wakorofi zaidi na ndio wanaotutoa imani, siku mbili tu mtu anaajiriwa *ZRB* utamkuta na gari kuliko hata ya Rais.

Haya mambo yanatia unyonge, ukiangalia mshahara wake, kipato chake, ukianza kufanya tathmini mlo wake, matibabu, simu na umeme basi unakuta hazitoshelezi hata kununua gari ya toyota kwa mwaka mmoja. Lakini mwaka mmoja mtu ana magari matano au sita wananchi waliokuwa wengi wako masikini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi katika hili na Mwenyezi Mungu inshaallah atamsaidia na sisi tuko nyuma yake kumsaidia katika hili.

Mhe. Naibu Spika, jambo la tatu ambalo wengi wameliogelea ni suala la mafuta. Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 46 tumeelezewa kuhusu suala la mafuta, mheshimiwa ukitaja suala la mafuta huko nje basi wananchi wetu wanatamani kutumeza. Kwani matarajio yao ni kuona sisi tunawafikisha wapi pale ambapo ule umasikini utawaondokea. Mhe. Naibu Spika, kila nchi ina tegemezi yake na mengi ambayo tulikuwa tunategemea sasa hivi hayapo. Mhe. Naibu Spika, hapa tunalotegemea ni mafuta imekuwa vikwazo ni vingi, maelezo mengi hivyo tatizo ni nini?

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki kwenda ndani zaidi lakini naelezea kwa udogo wangu sana kwa kulishukuru Baraza lilopita la Wawakilishi kwa kazi kubwa, kwa umahiri mkubwa kwa kuweza kulifanya suala hili kuliondosha katika masuala ya Muungano. Mhe. Naibu Spika, mimi pia msimamo wangu uko hapo hapo kwamba ile hatua ambayo ilianza kufikiwa hebu tupewe maelezo tumefikia wapi. Kuna mambo hapa wenzetu waliyaandaa kuhusu suala la sera ya nishati, suala la utekelezaji wa mshauri elekezi, suala la utafiti. Hivyo, tunaanzisha mambo lakini baadae hatujui tumefika wapi na wananchi wanahitaji kujua wapi masuala haya yamefika na wapi yamekwama.

Mhe. Naibu Spika, naliomba suala hili liharakishwe kwani tunaumia ndio sisi tunaopiga kelele na nasema tutapiga kelele sana kwa hili, watu watakufa sana, hali zitakuwa ngumu sana kama kuna vitu ambavyo tumeviona viko karibu na vinaweza kutusaidia kama hatukuwa na uharaka wa kuweza kuvifanyia kazi ili viweze kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu amesema haya na mimi nataka kusema hayo hayo kwamba uchumi tunao lakini tunaukalia. Mhe. Naibu Spika, na hatari yenyewe ni kwamba hatukuukalia sawa sawa tumeukalia upande mmoja, mimi naomba tukaze buti katika hili ni imani yangu kwamba hakuna kisichozungumzika. Mhe. Naibu Spika, wenzetu wanashaurika,

wenzetu wanazungumzika na nina imani kwamba kwa hili watatusikiliza, lakini wakati tunasubiri mazungumzo basi kazi zianze.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimalizie kwa sababu naona unaniangalia muda namalizia katika masuala ya kipaumbele, nataka nimshukuru Mhe. Waziri kwa vipaumbele sita alivyovieleza kwa kweli kila mtu amekuwa na matarajio na wananchi wetu wengi wamejenga matumaini katika hili. Lakini pamoja na kuweka vipaumbele hivi bado na mimi kwa upande wangu namuomba Mhe. Waziri suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi tulipe kipaumbele cha pekee. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tutakapoiwezesha wizara hii nina imani kwamba wananchi walio wengi watanufaika na kupata ajira zilokuwa sio rasmi na kuipunguzia serikali ajira.

Mhe. Naibu Spika, sisemi hivi kwa sababu Mhe. Haroun Ali Suleiman alikuwa ni mwalimu wangu mwaka 1985 pale Haile Selasie, mimi nazungumza hili kwa kuangalia mustakbali wa nchi yetu katika suala zima au ukwasi uliotupata katika suala zima la ajira. Mhe. Naibu Spika, ajira imekuwa ngumu serikalini lakini tuna njia ambazo ni mbadala na Mhe. Rais ameiona hii wizara akaianzisha, basi nimuombe Mhe. Waziri hii taasisi ya uwezeshaji kiuchumi ipewe kipaumbele cha pekee.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nasema kuna mengi vipaumbele ni vizuri, niseme tu kwa sababu muda unatukimbia na kuna wenzangu ambao wanahitaji kutoa michango yao. Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba naunga mkono bajeti hii sio kwa asilimia mia moja, bali ni kwa asilimia zote hata kama itakuwa mia tano mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika bajeti ya mara hii ya Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, napenda niseme kwamba tusisahau kuwa mfumo mpya duniani ambao uchumi wa dunia unaelekeza kuwa ni kitu kimoja. Kwa hivyo, kama ni hivyo mfumo wetu wa dunia utakuwa ni kitu kimoja basi mabadiliko ni ya lazima, ni lazima mabadiliko yapatikane ya mfumo mpya wa uchumi duniani. Kwa hivyo, kutokana na mabadiliko haya umezifanya nchi zetu za Afrika Mashariki kuwa nazo zipate mfumo wa aina hiyo. Nataka nimshukuru Waziri wa Fedha kuweza kwenda sambamba na mfumo wa dunia kuwa kitu kimoja, na nitatoa mifano ambayo na yeye ni sahihi katika bajeti yake hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo hazina budi nchi zetu za Afrika au sisi wenyewe Wazanzibari kwamba lazima ziangalie upya mambo yafuatayo. Kwanza

namshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kuzingatia mipango yetu kwa sababu hatuwezi kwenda bila ya mipango. Kwa hivyo, katika kitabu chake ameweza kutandika mipango rasmi jinsi gani tutakwenda na bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo lilofikiriwa ni suala zima la sera yetu, kwa hivyo, na sera iko wazi kabisa inaelekeza katika mfumo mzima wa bajeti. Pia tunahitaji katika mpango mpya wa mfumo mmoja wa dunia ni lazima mikakati iandaliwe na mikakati bila shaka ndio inaelekeza *strategies* hizi ni lazima ziwepo. Kwa hivyo, katika mfumo wetu wa bajeti ya mara hii haya yamekuwepo, mipango tunayo, sera tunazo na mikakati tunayo vile vile.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ni muhimu sana ni suala zima la usimamizi pamoja na yote haya ni lazima tuhakikishe kwamba usimamizi umekuwa mzuri na uwajibikaji ndani yake umekuwa wa ukamilifu kabisa. Kwa kweli bajeti hii ya mara hii imetoa taswira nzuri, imetoa tafsiri nzima iko wazi kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri pamoja na kuandaa haya kimfumo wa kidunia ni sawa lakini tutaangalia hali tunavyokwenda hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na yote hayo ya kukuwa tunaambiwa katika bajeti hii kwamba uchumi umekuwa, lakini tuangalie katika kukuwa katika uchumi wetu hakuna uchumi utakaokuwa hauna tofauti. Kwa hivyo, uchumi wote utakaokuwepo utakuwa na tofauti ya kipato miongoni mwa wananchi wetu tulionao. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba watakuwepo wale ambao wenye uwezo na wale wenye kipato, ambao kipato hiki tunasema ni kipato cha chini kabisa. Kwa hivyo, tutakuwa nao watu wenye uwezo tabaka la watu wenye uwezo na vile vile tutakuwa na tabaka la watu ambao hali zao ziko chini sana.

Mhe. Naibu Spika, wale wenye kipato cha chini maisha yao siku zote yanakuwa duni siku hadi siku. Kwa hivyo, hii ndio tunasema kama hali ni hii ndio tunasema kwamba lengo kubwa la kukuza uchumi ni kupunguza umasikini, hali ndio hiyo kwamba imejengeka katika taifa letu wale wenye uwezo ambao wanamudu kufanya mambo yao na wale ambao waliokuwa hawana uwezo hali yao ni duni.

Mhe. Naibu Spika, tuchukue mfano ambao mtu hali yake ni duni tujaalie mwanamke ambaye yuko peke yake, pengine hana familia nyengine isipokuwa yeye na watoto wake. Hivyo, hana mpango wa kupata maisha ya binafsi ila atafute biashara ndogo ndogo ende akachukue kilo mbili za unga ende akafanye maandazi ili ale na watoto wake. Mhe. Naibu Spika, hebu nifikirie kilo mbili hizi za unga na pengine ana watoto watano nyumbani kwake anategemea apate kiasi gani kuweza kuwalisha, wapate nguo, wapate madawa na shughuli zote za nyumbani.

Kwa hivyo, hilo ndio linalokuwa tabaka ambalo ni la chini, hili ni suala ambalo namtupia Mhe. Waziri alielewe kwamba pamoja na yote ya kutengeneza hali ya uchumi, lakini taifa liko katika hali mbaya. Je, yeye kama ni Waziri na masuala yangu ameyasikia kwa wananchi kama hawa ambao hali ni duni na maisha ni magumu katika kuendeleza maisha yao ya kila siku, je, atawasaidia kiasi gani au kundi hili ameliona, ameligundua? Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tuna haja ya kuwafikiria wale ambao hali zao ni duni je, bajeti hii imewafikiria watu hao au haikuwafikiria?
Mhe. Naibu Spika, sasa niingie katika sekta ya kilimo ambayo katika bajeti hii sekta hii ya kilimo imetoa vipaumbele vyake na sote tumeviona. Lakini kubwa katika sekta hii ya kilimo ni suala zima la umwagiliaji maji kwa sababu zamani tulikuwa tunalima chakula chetu kwa kutegemea mvua, lakini kwa hali zozote imebainika kwamba kwa kutegemea mvua hatuwezi tukapata mafanikio.

Kwa hivyo, maamuzi makubwa yamekuja katika suala zima la umwagiliaji Mhe. Waziri amejitahidi kuelezea kwamba tutaweka mbegu za mpunga zilizo bora, zenye mapato makubwa pia zinazoweza kustahamili wadudu, mbolea pamoja na madawa ya kuulia magugu pamoja na kuweka matrekta ya kwa ajili ya kulimia mabonde hayo. Lakini tunaulizana sasa pamoja na kuwa serikali inasema imeweka kilimo kipewe nafasi ya juu kabisa ambayo tangu hapo zamani tunasema katika kuendeleza uchumi wa nchi hii tumesikia mambo mbali mbali mpaka tumefikia kilimo leo.

Kwa sababu zamani tulianza kwenye karafuu, tukatoka kwenye karafuu tukaingia kwenye utalii, tukatoka kwenye utalii haidhuru utalii ndio unaleta mapato makubwa ya nchi hii lakini pia tukasema mwanzo iende kwenye kilimo. Lakini na hicho kilimo chenyewe kwa ushahidi kamili unaonesha kwamba bado ukulima wetu ni kumfaidia mtu mmoja mmoja na lengo letu sio la kumfaidia mtu mmoja mmoja, lengo letu ni kutoa manufaa ya chakula au mavuno yatakayovunwa kwa kuweza kusafirisha nchi za nje. Je, Mhe. Waziri hapa amejiandaa kiasi gani kwamba tunajua na wana kubalia kwamba mavuno yanayopatikana ni ya faida ya mtu kwa chakulia chake, lakini bado mavuno yakuweza tukauza nje bado hayajapatikana. Mhe. Naibu Spika, hii ndio dhamira ya kwamba tukauze nje ili tupunguze kuagizia michele, bado hilo halijatendeka.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona kwa mawazo yangu waziri katika kuandaa suala zima la kilimo ilikuwa aangalie kisiwa cha Unguja na aangalie kisiwa cha Pemba haiwezekani kwa kilimo hicho hicho cha mpunga kinaweza kikastahamili kwa mambo yote. Lakini angelikwenda akaangalia kwa mfano tuchukue hapa Unguja kuna maeneo mengi ambayo yakuweza kufanya umwagiliaji wa maji. Lakini kuna maeneo mengi vile vile hayana uwezo huu wa kuweza kumwagilia maji na yote haya yatategemea hayo mabonde ambayo

yanaweza kuzalisha chakula kwa wingi tukashiba sisi tuliomo humu ndani na tukaweza kusafirisha.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naona jambo moja ambalo hakuweza kulizingatia angeliangalia *geographical* baina ya kisiwa cha Pemba na Unguja. Mhe. Naibu Spika, hali ya Pemba kuanzia Kusini kwenda Kaskazini ni mabonde na milima na mvua zake huwa ni nyingi hicho ndio kilimo cha mpunga. Lakini ukitoka Kusini mpaka Kaskazini ya Magharibi kuna Kusini na Kaskazini ya Mashariki ambako huko kwa kilimo cha mpunga hakiwezi kufanyika. Kwa hivyo, je Mhe. Waziri ameangalia suala hilo la ardhi tuliyonayo kwamba hizo ardhi nyengine haziwezi kulima mpunga. Je, hapa waziri amejiandaa kiasi gani kuhakikisha kwamba hao watu wa Mashariki ambao ukanda wao ni wa mawe je watu hawa amewaandalia kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii haikutoa taswira hiyo, taswira ya Unguja tambarare ambayo ni sehemu ya mawe haiwezekani kwa kilimo cha mpunga, na taswira hii hii kwa Pemba kwa sehemu ya ukanda kuanzia Kaskazini mpaka Kusini upande wa Mashariki suala hilo la kilimo cha mpunga hakiwezekani. Je, na sisi tunataka tushibe halafu tuuze hivyo inawezekana?

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema hapa amekosea kitu kimoja kwamba hakuweza kuwafikiria watu wenye tambarare za nchi za mawe kwamba hapa tuweke makulima tu, tusiweke njia ya kilimo maalum kwamba kama kuna mbaazi, kuna choroko, kuna mahindi, kuna mtama hakuna katika bajeti hii haijaeleza kwamba tutafikiria hayo. Kwa hivyo, hilo ni changamoto kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme vile vile haikuanisha kwamba katika kilimo hiki tutakachokifanya kiwe ni kilimo chetu rasmi mara hii kulikuwa na hujuma za wadudu wengi sana katika kilimo cha mpunga, wananchi walikuwa na wanahangaika kutafuta madawa ya kuulia wadudu. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba chakula kiko tayari, wadudu wameshaanza kuhudumu chakula hakukuwa na maelezo yoyote katika Wizara ya Kilimo ila kuvamiwa wawakilishi na wabunge watoe dawa kwa ajili ya wadudu kwa kuwauwa, tutawamaliza watu wote, sio rahisi mheshimiwa.

Kwa hivyo, waziri hapa hajafikiria hasa mikakati yakuona kilimo kikapeleka na taathira zake inawezekana jua, inawezekana mvua nyingi, inawezekana upepo ukapukusa maua, inawezekana wadudu wakahujumu mpunga. Hilo mbona halijafikiriwa ni kulima tu hakuna matokeo ambayo athari zitaweza kuathiri kilimo, hivyo hayo yote hayakupewa kipaumbele na kama yalipewa basi hakuna huduma ambazo zinatolewa kwenye masuala haya. Kwa hivyo, hapa ningemshauri Mhe. Waziri katika suala zima la kilimo aliangalie vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ningelimwambia Mhe. Waziri si kilimo tu, kilimo yote ni jumla ya kilimo lakini hata matunda, hata *spices* zote hizo zinaingia katika kilimo haya mbona hayakufikiriwa. Mhe. Naibu Spika, bado fedha ya Zanzibar tunasema Zanzibar hakuna mzunguko mzuri wa fedha, tunapata mishahara leo, tunapata hapa tunauza kila kitu asubuhi tunaifunga kago tunapeleka nje. Mhe. Naibu Spika, pesa ya Zanzibar haina mzunguko kwa sababu hatuzalishi ndani, fedha yetu tuwe nayo mkononi tupeleke nje tukanunue halafu tulete ndani na sisi tunasema tunataka fedha izunguke Zanzibar, fedha haizunguki. Kwa hivyo, bado kuna hali ngumu ya kuhakikisha kwamba katika kuzalisha chakula pamoja na matunda na shughuli nyengine za kilimo zifanywe na wananchi. Hiyo ni mikakati ya Wizara ya Kilimo na hiyo katika bajeti yake hatukuiona imeelemea upande mmoja imeipuuza upande wa pili, bado fedha zitakuwa hazina mzunguko wa Zanzibar kwa sababu bado fedha tunaipeleka nje kununua vitu vyengine.

Mhe. Naibu Spika, tuje katika suala la afya kwa kweli tumepewa vipaumbele vya afya vipo huduma nzuri, madawa tunaambiwa tutaletewa, vifaa vya hospitali tutaletewa, lakini nasema haya ni mazungumzo ya kila siku. Hizi huduma na madawa bado unapokwenda hospitali unaambiwa madawa hamna inabidi ndio maana tukapata hizi *pharmacy* tunakwenda tunanunua humo. Je, kama madawa yapo ya kutosha hizi *pharmacy* zingeweza kufanya kazi?.

Kwa hivyo, hali hii bado tuna mapungufu makubwa ya dawa, vifaa vya hospitali hali ambayo inajitokeza sasa hivi niseme kwamba idadi ya watu Zanzibar imeongezeka, na kama idadi ya watu Zanzibar imeongezeka basi hatuna budi na hospitali zetu ambazo tulizozijenga kwa miaka mingi ni lazima papatikane tofauti. Kwa sababu haiwezekani jengo lile lile, nyumba vile vile kama chumba kinachukua watu kumi miaka mitano iliyopita, haiwezekani chumba kile kile baada ya miaka 20 au 30 ikachukua idadi ya wale watu 10 itabidi watu wengine walale nje.

Kwa hivyo, hapa ni lazima waziri afikirie katika kuyafanya mazingira ya hospitali yawe bora zaidi kwa kuongeza majengo ambayo majengo haya yataweza kutoa huduma kwa wananchi kutokana na idadi ya watu waliomo Zanzibar hatuwezi kuwa na majengo yale yale na tukasema majengo haya yaendelee kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo, suala la kusema tunapandisha daraja kwamba hospitali hii sasa hivi imekuwa ya Wilaya maana yake itasaidia nini wakati makaazi ni yale yale, madawa pana mapungufu na mambo mengi yamo mapungufu. Kwa hivyo, nafikiri hapa Mhe. Waziri angalie sana kwenye masuala ya majengo na kuongezeka kwa idadi ya watu.

Mhe. Naibu Spika, jengine niseme tu kwamba katika suala zima la serikali kuwanufaisha wananchi katika kutoa huduma. Mhe. Naibu Spika, nasema huduma za maji safi ni sawa lakini bado Zanzibar Mjini Magharibi kuna matatizo ya maji. Mhe. Naibu Spika, kelele zimekuwa za muda mrefu lakini bado hapa kati kati ya Jiji la Zanzibar matatizo ya maji yapo na yakipatikana maji basi ni saa tano za usiku.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana hapa kuna mambo ya hitilafu ama itakuwa kuna uchakavu wa mabomba au bado kuna maeneo mabomba hayajatiwa na maji hayapelekwi na hao waliowekwa huko kusimamia suala hili wanangoja watutese mpaka saa tano za usiku ndio watu wapewe maji, hilo sio jambo la busara. Mhe. Naibu Spika, inatakiwa tufanye jambo la kiubinadamu kwamba serikali imefanya jitihada maji yatolewe na mapema.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine kulikuwa na mikopo ya benki linasema suala hili la mikopo ya mabenki wizara iendelee kukopa katika mabenki isikope huko vichochoroni kwenye makampuni na mashirika. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tukianza kukopa huko vichochoroni kwenye mashirika na watu binafsi tunaipa mzigo serikali kwa sababu *interest* ya kule na *interest* ya mabenki itakuwa ni tofauti. Tunaipa mzigo mkubwa sana serikali na interest ya benki na *interest* ya mabenki itakuwa ni tofauti, tunaipa mzigo mkubwa sana serikali na *interest* zao ni tofauti au huku kuna habari gani kuwa lazima tuelekee huko kwani benki hazipo, naona Unguja tuna benki nyingi tu. Kwa hivyo, tuendelee kukopa katika banki kuliko kuendelea kukopa katika sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la misaada ya bajeti ambayo ni ile ya 4.5 *percentage.* Hii inasema kuna bilioni hizi zilizotajwa kiasi shilingi 30.28 bilioni ambazo kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Waziri tunakwambia kwamba mgao huu wa **milioni**30.28 hauelezi uhalali wa fedha zote. Kwa hivyo, hapa sisi tunasema hatujaridhika na hii 4.5%, nenda, fanya, panga, pangua, lakini suala hili la 4.5% tunataka maelezo ya kutosha bado hatujaridhika nalo linatupa wasi wasi.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la vipaumbele vya elimu kwenye suala la madawati, maabara, vifaa, ujenzi wa madarasa, hapa yameelezwa vya kutosha lakini tangu miaka ya nyuma maelezo haya yanakuwa hivi hivi Mhe. Waziri, bado kuna mapungufu makubwa ya madawati, vifaa vya sayansi, walimu, kuna mambo kemkem ya mapungufu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hayasemwi sana tu, lakini huko kuna siri kubwa sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri haya masuala baada ya kuyatengeneza hebu nyinyi wenyewe piteni hii fedha mliyoitoa ni hakika kwamba mmeitoa kwenye Wizara ya Elimu au wizara ya Afya imefanya kazi vya kutosha, au tunapeleka fedha mgao huu unakwenda

badala ya kuhudumia jambo fulani watu wanageuza wanafanya huduma nyengine. Kwa hivyo, haya mapungufu yaliyopo yaweze kurekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la *Zanzibar Free Port*, tunahitaji Zanzibar bandari huru tuwe nayo, tuwape nafasi. Mimi nataka niseme kitu kimoja nimwambie Mhe. Waziri, kwa mfano tulinganishe vitu viwili, tuchukue Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo na Maliasili hizi ni mbili. Tumchukue mwekezaji tumuuliwe hii ni Wizara ya Kilimo na hii ni Wizara ya Biashara tunataka wewe uwe mwekezaji wetu mkubwa utakwenda upande gani? Utakwenda kwenye kilimo au kwenye biashara?atasema siendi kwenye kilimo nitakwenda kwenye biashara. Kwa nini asema atakwenda kwenye biashara? Anajua fedha yake akiipeleka kwenye kilimo kama mwekezaji anajua fedha ile itakwenda itaangamia hairudi.

Sasa kwa hivyo, ataingia katika biashara. Kwa ufupi ni kusema kwamba, mazingira ya Zanzibar ni mazingira ya kibiashara na watu wote wanaelemea kwenye biashara, kama hali ya Unguja ni suala zima la kibiashara basi tuwekeni *free port* sio maeneo huru ya Micheweni au ya Fumba haya yatatusaidia nini, ukame ulioko Micheweni, hali ya maisha magumu kweli hiyo, maeneo huyu?

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nataka nizungumzie suala zima la mafuta na gesi asilia. Suala la mafuta linatukereketa na roho, hii ni rasilimali ya Wazanzibari, tunaumia. Kuna nyaraka za kihistoria zinazozungumzia asili na inasema mafuta ni ya Wazanzibari na mafuta yatachimbwa na wenyewe Wazanzibari hakuna mtu mwengine yeyote atakayeingilia. Hili ni suala muhimu, sasa mimi nastaajabu kitu tumezungumza kipindi kilichopita, tumekubaliana, sera ya mafuta iko tayari, vijana tumeshawapeleka kwenda kusoma, kuna lipi tena tukashauri tunamshauri nani?

Nasema mafuta tuchimbe wenyewe Wazanzibari hii ni rasilimali yetu, ni hidaya yetu hii, hii hidaya Mwenyezi Mungu katupa au mnataka tunyang'anywe, tunangoja tunyang'anywe wanayataka hao, tukilala watatunyang'anya kweli, watatafuta vipengele tu vya kutunyang'anya. Tunasema Wazanzibari kwa nini serikali mpaka leo inashindwa kuileta tena hoja hii tukaizungumza tangu tulipozungumza kipindi cha mwaka 2005 mpaka leo haijaletwa tena maana yake nini? Si kunyang'anywa huko, huko ni kunyang'anywa wanatafuta vipengele watunyang'anye na sisi hatunyang'anyiki wala hatudanganyiki hata siku moja.

Kwa hivyo, nasema suala la mafuta ni yetu wenyewe na hatua tuliyokwishapiga ni kubwa na namshukuru aliyekuwa Mhe. Waziri wa wizara inayohusiana na mambo ya mafuta, Mhe. Mansour alifanya kazi kubwa sana, alituelimisha vya

kutosha, akatupa mikakati na maelekezo mazuri na Baraza la Mapinduzi lilikubali hasa likatuletea waraka, tukaujadili waraka ule tukakubaliana nao hakuna masuala tena, hakuna mjadala katika suala la mafuta, mafuta ni yetu Wazanzibari. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Konde na mimi nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Subeti Khamis Faki: nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba hii ya bajeti iliyoko mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi namshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea bajeti hii katika kipindi ambacho wananchi wetu wa Zanzibar wote wana matarajio makubwa kuhusu bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nianze katika eneo la uvuvi. Nasema sasa wakati umefika, kwa sababu huwezi kufuga mali ardhini au baharini, mali ukiifuga ardhini aidha italiwa na ardhi na mali ukiifuga baharini basi inaweza ikayayuka na maji. Kwa nini nikasema hivyo Mheshimiwa? Kwa sababu sisi hapa Zanzibar tuna rasilimali nyingi sana na sisi kila kukicha tunasema nchi yetu ni masikini, lakini mimi nataka kusema kwamba huu umasikini na sisi wenyewe tunauchangia. Kwa nini niseme kwamba wenyewe tunauchangia?

Mhe. Naibu Spika, bajeti iliyopita tulizungumza kuhusu suala la uvuvi wa bahari kuu na mara hii tumelirudia tena suala hili, hivi tunasubiri nini kusema kweli. Katika bajeti yetu hii Mhe. Waziri anatuambia alitoa leseni ambazo zilitolewa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, lakini leseni zile zilizotolewa zilitolewa kwa wageni ambao kuwa wao ndio waliovua bahari kuu, hivi wavuvi wageni ikiwa watavua ndio tutafaidika sisi au faida yetu sisi ni kutoa leseni watu wakatuibia? Hivi hizi leseni tunazozitoa ili watu wavue samaki wenye wakajifaidishe kwenye nchi zao ndio sisi tunatosheka?

Mhe. Naibu Spika, wakati umefika serikali ifanye kila jitihada, kila linalowezekana ili sasa wananchi wetu wafaidike na rasilimali zilizo katika nchi yao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wakati umefika sasa wananchi wa Zanzibar wafaidike na uvuvi wa bahari kuu, fanyeni kila jitihada serikali ni mama, serikali ni baba, linaloharibika lolote kwa nchi inaangaliwa serikali.

Wananchi wanajua serikali yao ina uwezo kwa sababu unapopewa uwezo wa akili, fikira, kila aina Mwenyezi Mungu amekupa mwanadamu, kwa hivyo, sisi pamoja na umasikini wetu tulionao hebu tubembelezeni watu wenye uwezo waje wawekeze, tukipata meli mbili au tatu tu hapa wananchi wa Zanzibar wakiingia kwenye meli zile wakienda kuvua watafaidika. Kwa hivyo, sasa wakati umefika Mhe. Waziri tusifuge samaki baharini.

Kipindi kilichopita hapa nilisema kwamba samaki wanacheka tu baharini mkanicheka, mkasema kuna samaki wanaocheka? Ndio wanacheka kwa sababu hawavuliwi wamo baharini wametulia tu. Kwa hivyo, wakati umefika sasa wale samaki kuwafanyia kazi wakafaidisha nchi yetu.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ni suala la kilimo, mwenzangu amezungumza hapa kwamba serikali ina nia nzuri kabisa ya kuanzisha kilimo ambacho kitakuwa na manufaa kwa nchi yetu na kutusaidia. Lakini kama alivyosema mwenzangu kisiwe kilimo cha kufaidisha mtu mmoja mmoja. Kwa sababu kilimo cha kufaidisha mto mmoja mmoja hatutaona tija yake, kuwa mtu anakwenda kulima akapata mpunga wa kula siku mbili bado. Kwa hivyo, serikali kama kweli imepania kufufua au kunyanyua kilimo basi ianzishe kilimo cha ukweli iwe ni kilimo ambacho kitakuwa kinatufaidisha kwa Zanzibar nzima.

Halafu namuomba Mhe. Waziri isiwe ni kilimo cha mpunga tu, mtu wa Micheweni hana bonde la mpunga, kibonde kilichopo pale watu anakwenda waking'ang'aniana, koo kumi zina eka moja wananyang'anyiana, huwezi kusema hawa wanalima mpunga. Kwa hivyo, je, hawa wenzetu walioko kama kule Micheweni, Kizimkazi, Nungwi na kwengineko, Mhe. Waziri umewaandalia maandalizi gani. Kwa sababu sio watakaolima mpunga tu kuna wananchi wengine hawana maeneo ya kulima mpunga. Kwa hivyo, serikali imewaandalia maandalizi gani na hawa nao ni wananchi wa Zanzibar. Mhe. Waziri na wao uwapangie mipango kabambe ili wananchi wa Zanzibar wote waweze kufaidika na wafaidike na rasilimali za nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la kuimarisha Muungano. Mhe. Naibu Spika, suala hili nalo kwa kweli linataka kuandaliwa. Mhe. Waziri naomba suala hili nalo aliangalie kwa kina kabisa. Kwa sababu wenzangu wamezungumza, lakini na mimi kwa vile linanikereketa nitazungumza.

Kuna suala la fedha za wahisani ambazo zinasaidia zinazokuja kwa ajili ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Waziri Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliyopitishwa juzi ni 13 trilioni, sasa fedha hizi ukiziangalia kuna fedha ambazo ni mapato ya ndani yanayotoka kwenye Serikali ya Muungano na kuna fedha zinazokuja kama ni misaada, hizi ni zetu pamoja si zao peke yao. Kwa sababu Tanzania ikiambiwa na sisi Zanzibar tumo kwa hivyo, hizi fedha ni zetu sisi pamoja na wao, sasa kama ni zetu pamoja asilimia hamsini ya bajeti ni fedha zinazotoka kwa wahisani kutoka nje zinazosaidia Tanzania msaada wa kibajeti.

Sasa trilioni 13 hizi zilizotolewa ukizigawa hizi basi kama tirilioni nane ni fedha ambazo zimekuja kwa ajili ya kusaidiwa Tanzania. Sasa je, sisi tumesaidiwa hizi shilingi 30 bilioni hivi hizi fedha zikigawiwa huo muda zinaogawiwa wa ile 4.5 hizi ukizigawa kweli tunazopewa sisi ni sawa sawa na hizo fedha ambazo tunatakiwa tupewe? Kwa hivyo, wenzetu wanatufanyia ujanja, hapa pana ujanja.

Mhe. Waziri tunakutaka uangalie kwa kina wenzetu bwana ni wajanja mno tumeshachoka kufanyiwa ujanja, wenzetu wanatufanyia ujanja. Mhe. Waziri tunataka hizi fedha mzichunguze kwa kina kabisa tuangalie haki yetu Zanzibar ni ipi, kwa sababu wenzetu wanatupaka mafuta kwa nyuma ya chupa, wanatupaka nyuma ya chupa tunaona vizuri Mheshimiwa tumeshachoka.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ninalotaka kuzungumza ni hili hili suala la kuimarisha Muungano. Nyumba tunakotoka tulikuwa na mgogoro wa kuwa Zanzibar si nchi, tukaja hapa tukakaa kitako tukarekebisha katiba ya kuwa Zanzibar ni nchi, sasa hivi kuna suala la Afrika Mashariki. Suala la Afrika Mashariki kwa nini Zanzibar isiingie kama ni nchi tuingie kwa mwavuli wa Muungano kwa nini.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba na hili uliangalie, tunaingia Afrika Mashariki kwa mgongo wa Serikali ya Muungano tayari suala lile la mgogoro hakuji kero ya Muungano pale, kutakuja na zogo la Muungano huku nyuma. Kwa sababu tukishaingia tayari moja kwa moja Zanzibar itakuwa pale pale kuwa si nchi tutawaambia vipi watu hata wakubali na sisi tumeingia kwa mwamvuli wa Muungano.

Rwanda imeingia wenyewe, Uganda imeingia wenyewe, Kenya inaingia yenyewe, Tanzania pia kwa nini sisi tuingie kwa *umbrella?* Kwa nini sisi Zanzibar wakati ni nchi tusiingie wenyewe pale? Mheshimiwa ‘ujiti na macho, nchi na hoho’. Wallahi tutakuja kutimiza miaka 10 tunapapatua, hapa nawaomba mpaangalie kwa kina kabisa, tunaingia kwenye shimo Zanzibar inamalizika hapa Afrika Mashariki kuingia kwa mwavuli wa Muungano tunamalizika, Zanzibar itakuwa kweli si nchi na moja kwa moja itakuwa si nchi tunakuja kupapatua miaka nenda miaka rudi na bado haijatoka.

Tunaomba Mhe. Waziri na hili nalo mliangalie katika masuala ya kuimarisha Muungano mlione kama ni moja la kuimarisha, Muungano wetu ni sawa sawa upo kwa nini sasa wakati umefika kuna jambo gani lenye uzito wa kuwa wenzetu wale wa Tanganyika wasiwe na Serikali ya Tanganyika na sisi tukawanayo ya Zanzibar halafu tukawa na ya Muungano tukafanya kazi kwa pamoja kwa nini, kuna uzito gani jamani.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni suala la nishati, hili nalo ni suala linalotuumiza. Leo tumeshakuwa tunaungiwa tena umeme wa *NCC*, asubuhi nimezungumza na hivi sasa nazungumza. Tuna mradi huu wa *NCC* wa umeme ambao tutachukua *megawaltt* 100 kupeleka hapa. Sasa wasi wasi wangu nilionao tulikuwa na *megawaltt* 50, leo umeme wa kugaiwa tunapata kwa mgao, bahari nzuri baada ya kupata matatizo yale ya umeme rafiki yangu kupitia serikali yetu na jenerali wetu aliyekuwepo tukapata majenereta 32, lakini hivi sasa majenereta yale hayakidhi haja kwa sababu ya kwamba tuna matatizo ya mafuta, hatuna mafuta ya kuendeshea jenereta kwa hivyo, umeme unakwenda kwa mgao.
Sasa leo *megawaltt* 50 tuna mgao, haya hizi *megawaltt* zinazoundwa 100 wao wenyewe kule sasa hivi hauwatoshi umeme, bado nasema kuna haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujitatua na suala la kupata umeme mbadala katika nchi yetu basi ndio suala zima kwisha.

Mhe. Naibu Spika, kufundua tandu ukamfunika nge ni mashaka, tandu anauma na ana ushingo, nge kazidi. Kwa hivyo, tunafunua tandu tunafunika nge tunamwambia tandu tutafune, umeme huu bado halijawa suluhisho la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Waziri suluhisho ni kupata umeme mbadala katika nchi yetu, tujipinde, tujifanye vipi, twende, turudi, lakini suluhisho tufanye kila inavyowezekana tupate umeme mbadala katika nchi yetu.

Jamani mimi asubuhi nilisema maneno yangu nimetoa kama wazee wa kale walivyokuwa wakiseme kutoa maneno ni elimu, jamani mtumaini cha ndugu anakufa masikini, wewe hutaki kujituma leo unasikia ndugu yangu ana mali na mimi nitakuja kupata, bora jitume ndugu yako akifa ana watoto ndio watakaorithi mali ile, hurithi wewe mali ya ndugu yako wanarithi watoto wake. Kwa hivyo, na sisi tujipindeni kila hali tupate umeme wetu Zanzibar, umeme huu wa kutamania kule wenyewe kila siku wanatuongezea madeni, madeni haya yanaongezwa kila siku.

Leo Mhe. Naibu Waziri anatuambia kwamba walikaa kitako, sisi tumeshafuatilia Ngelege alitukimbia kule, tulimfuata alitukimbia katika kamati yetu kipindi kilichopita tulipokwenda kwa suala hili, tangu kipindi cha miaka mitano iliyopita. Tulikwenda sisi kumfuata Ngeleje alitukimbia. Sasa Mhe. Waziri Mkuu alisema suala hili la deni hakusikilizwa na Rais mwenyewe hakusikilizwa hivi sisi tutakusanya kero za Muungano mpaka lini? Zitakuwa ngapi kero hizi? Kila linalokuja tunalizungumza ni kero la Muungano jamani sasa tena tusiwe na kero la Muungano tena liwe na zogo la Muungano, mambo mengine tuyatanye sisi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni suala la elimu. Kama walivyozungumza wenzangu kwamba kuna vipaumbele vya kuimarisha elimu, lakini na mambo

mengine yanatia aibu katika nchi yetu, ingawa masuala hayo nataka nije niyazungumze katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini nayatoa kidogo. Mambo mengine yanatia aibu tunawadumaza watoto wetu katika elimu itakuwa hawafahamu. Leo Mhe. Waziri kwa mfano nitoe mfano wa skuli yangu ya Micheweni, kuna madarasa 12 watoto wanaokaa kwenye viti ni madarasa manne tu, yaliyobakia yote wanakaa chini, jamani hebu Mheshimiwa tujitahidini kidogo.

Mhe. Naibu Spika, namalizia hapa naunga mkono bajeti ahsante sana.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi magharibi haya kuchangia kidogo katika mwelekeo wa uchumi wa nchi yetu au Makadirio na Mapato ya nchi yetu.

Kwanza ningependa kushukuru kupata fursa hii kwa mara ya mwanzo katika maisha yangu na mimi kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Wananchi wa nchi hii. Ama Mhe. Waziri wewe utanisamehe, kwa sababu Waswahili wanasema, "mno dhara" naona hongera zimeshakuwa nyingi kwako.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, nataka nigusie kuhusu suala la karafuu, nafanya hivi ingawa Mhe. Ismail Jussa suala hili kalipitia kusini na kaskazi, lakini na mimi kidogo inabidi nichangie kwa sababu sehemu ninayotoka ndio sehemu kuu inayozalisha hizo tani 2000 zilizobakia za karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kuna kero zinazoitwa za Muungano na wenzangu wameshazitaja kwa wingi ikiwemo mafuta. Ama hili zao la karafuu limekuwa ni kero baina ya serikali na wananchi, hiki kidogo kilichobakia hivi sasa imekuwa ni kama keki ambayo kila mmoja anaiwania, serikali wanaitaka na wananchi wanaitaka wao. Katika suala hili nafikiri serikali bado haijaangalia kwa kina, tukiangalia rikodi tunakuta kwamba tulikuwa tuna sifa nzuri sana Zanzibar kwa kuzalisha karafuu bora na kwa wingi. Lakini hivi sasa sifa ile imeondoka tumebakia na tani 2000. Labda lawama kubwa tuwatupie wenzetu walikabidhiwa kazi hii Shirika la *ZSTC* ambao wao walikuwa ni wanunuaji wakubwa.

Mhe. Naibu Spika, shirika hili naweza kusema kwamba limetuweka pabaya, limetufikisha katika muda ambao karafuu yetu sijui huko ulimwenguni ina bei gani. Hivi sasa naweza kusema kuwa shirika halina uwazi katika bei ya karafuu. Nikisoma vitabu vyetu nakuta kwamba labda kwa kilo moja inauzwa kwa dola 3.591, ukipiga mahesabu unaweza kukuta labda ni shilingi elfu saba au nane hivi, wakati huko nje tunasikia kuwa karafuu ina bei au tukiangalia *internet* tunaikuta kuwa ina bei kubwa. Sasa sijui hapa pana uwazi gani.

Lakini la kushangaza zaidi kwamba hata hizi tani 2000 zilizobakia na wao wanazitaka. Kinachotokea sasa katika kung'ang'ania tani hizi ni kwamba wananchi wetu wengi wanaingia hasara na hasara wanayoipata wengi wanakufa kwa kupigwa risasi aidha na askari wa kuzuia magendo KMKM au wanazama baharini kwa kukimbia askari hao hao. Sasa ningeiomba serikali kwanza katika suala hili ikatafuta ufumbuzi na mimi hapo baadaye nitapendekeza baada ya kumaliza kuelezea suala moja na jengine.

Mhe. Naibu Spika, katika hii robo iliyobakia ambayo wananchi wanakwenda kuipeleka katika njia wanayoipata, mimi ningependa kumfahamisha Mhe. Waziri kwamba wananchi wamenufaika pakubwa sana na wengi waliyojiingiza katika biashara ya magendo utawaona hivi sasa tayari wao wameshaondokana na umasikini hawakusubiri serikali kuwasaidia kuondokana na umasikini. Leo watu hawa wameweza kujenga majumba, wameweza kuimarisha biashara, wamenunua magari, kwa hivyo hii keki iliyobakia imekuwa ni tamu sana, naweza kusema kwamba itakuwa ni kazi kubwa kwa serikali kwa hivi sasa kusema kwamba tunataka kuzuia magendo, sijui watazuia kwa njia gani kwa sababu na huyo anayetaka kuzuia magendo sijui Mhe. Waziri anayehusika na mishahara kawawekea mkoba wa kiasi gani, lakini na wao pia wanashawishika katika biashara hii. Kwa hivyo, hivi sasa kuna ugumu mkubwa.

Sasa ili kuondokana na matatizo hayo ya watu kufariki, wengine kuondoka katika nchi hii, kwa sababu ukituhumiwa kwamba unapeleka karafuu ya magendo basi inabidi uondoke wengine wamehama, wamekimbia familia zao, kungetafutwa *alternative* nyengine.

Serikali ina nia nzuri na imesema kwamba inataka kufanya *reform* ya shirika hili, si vibaya kufanya na wafanye, lakini wakimalizia utafiti wao na wakagundua kwamba labda tumegundua moja, mbili, tatu, basi wangeangalia na uwezekano mwengine. Je, hakuna uwezekano mwengine hivi sasa wa kusema kwamba hili zao tunaliondosha katika mkono wetu na tunalipeleka katika mkono mwengine? Baadaye ndio wakafikia suluhu. Kufanya hiyo *reform* ya Shirika la *ZSTC* itakuwa kama ni kufufua maiti. Kwa sababu wao wameondoka kutoka tani 12,000 mpaka wamefikia tani 2000, hii ni aibu, kama ni mgonjwa unamwita *nearly dead* huyu ameshafariki anahitaji apelekwe *ICU*. Sasa unafanya *restriction reform* ya nini tena.

Mhe. Naibu Spika, njia pekee nafikiri hivi sasa labda serikali ingetizama uwezekano mwengine, hivyo tukawaruhusu tukatoa leseni sisi kuwapa wananchi kuuza karafuu sisi wenyewe tukakusanya *export tax* kutokana na mauzaji yale ya karafuu je serikali isingefaidika? Kwa hivyo, mimi nashauri hapa kwamba serikali iangalie uwezekano, lakini zao hili la karafuu lisibakie

mikononi tena kwani hawa sina imani nao kwamba wanaweza wakaliendesha suala hili.

Labda ikiwa kama serikali inahofia kwamba wafanyakazi wake watafanya *redundance* serikali haitokuwa na pesa basi wangechukua hati fungate wakenda wakakopa katika mabenki au kwa watu binafsi huko. Lakini hili shirika halikuwa *statistics* kwamba wao wazalishe karafuu tu na waendelee kununua karafuu. Hii ni *Zanzibar State Trading Corporation* wanaweza wakaendelea mpaka biashara nyengine.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa biashara ya mwani imeshamiri na imekua kiasi kwamba imechukua nafasi ya biashara ya karafuu. Au wakaendesha biashara za michele na sukari pengine tungefaidika zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika suala la elimu. Mhe. Naibu Spika, serikali imejipanga na imeweka mikakati mizuri na hii ni moja tuliyoiweka vipaumbele. Mhe. Naibu Spika, serikali imejipanga naona zaidi katika sekta ya vikalio. Ukiwepo skuli ukiweka A na B, A inakuwa na *grade* kubwa na B *grade* ndogo, nayo ni njia moja ya kupanua sekta ya elimu.

Lakini hapa ninachotaka kukisema ni kwamba hivi sasa ukipiga mahesabu ya skuli ambazo tunazo tuna skuli karibu 690 tukiongezea na hizo ambazo tunataka kuzijenga itafikia skuli 700. Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa niliyoipata kutoka Baraza lako tukufu ni kwamba serikali ina mpango wa kuwaajiri walimu 800, kwa hesabu ya haraka haraka utakuta kila skuli itapata labda mwalimu mmoja na nusu.

Sasa hii naiona bado haijatiliwa umuhimu wa ziada. Hivyo kweli mwalimu mmoja kwa kila skuli ataweza kukidhi ule upungufu ambao tunao. Ili tuendelee na hii ndio nuru basi sekta hii ingeangaliwa zaidi. Sambamba na hilo sielewi kwamba mfuko wa Mhe. Haji Omar Kheir ukoje, lakini pia walimu lazima wapewe motisha ya hali ya juu. Katika watu ambao *physical and mental* wanafanya kazi ni hawa, wao saa 24 tofauti na mimi nikirudi hapa natupa mkoba napumzika.

Kwa hivyo, kama ni kuangalia basi waangaliwe ili sekta yetu ikue. Bila ya hayo hiyo *industrial revolution* ambayo tunatarajia kuifanya itakuwa tunajitaabisha.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika hilo serikali imejipanga kuwasomesha walimu lugha ya Kiingereza. Kama sikosei miaka ya 1900 mwisho wa miaka ile mimi sikuwepo katika nchi hii lakini niliwaona walimu wa lugha ya Kiingereza

waliokuja Uingereza kufundishwa lugha ya Kiingereza, ili walimu wale warudi katika nchi hii na waje wasaidie kuleta maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, walimu wale bado wengine wapo hai na wanajiweza. Sasa ningeshauri serikali kwamba watafutwe na wao waingizwe katika mfumo huu ambao unataka kuanzishwa wa lugha ya Kiingereza wakachangia na wao japo katika mfumo wa *partime.*

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niseme kwamba ukitaka kusoma lugha usikae pale ambapo haizungumzwi. Labda kama ni serikali ina nia nzuri kabisa basi ingeandaa programu nzuri ya kuwapeleka walimu hawa ambao imekusudia kuwaleta kuja kusomesha lugha ya Kiingereza katika zile nchi ambazo zinazungumza lugha ya Kiingereza. Hapo itakuwa tumefanya juhudi ya makusudi na itakuwa ile nia yetu ya kusema kwamba leo tuna walimu wa Kiingereza itapatikana.

Mhe. Naibu Spika, natoa mfano wangu mimi mwenyewe binafsi. Mhe. Naibu Spika, mimi nilibahatika kusoma mambo ya lugha na hivi sasa namshukuru Mwenyezi Mungu naelewa lugha nne. Lugha ya mwanzo niliyoisoma hapa ilikuwa ni lugha ya Kiarabu na nilichukua miaka minne lakini uwezo wangu ulikuwa ni mdogo. Lakini nilipokwenda katika nchi ambayo inazungumza lugha ile ya Kiarabu nilichukua muda mfupi sana na muda wa mwaka mmoja nikawa na mimi ni mtaalam wa lugha ya Kiarabu.

Sambamba na hilo naelewa na lugha ya Kiingereza, pia nilipata fursa ya kutembelea nchini Uingereza kwa hiyo nikajifunza lugha hiyo ya Kiingereza kwa muda mfupi. Kwa hiyo, naiomba serikali hawa ambao wameandaliwa kwa ajili ya kuja kusoma lugha ya Kiingereza basi wakapelekwa katika nchi ambazo zinazungumza lugha ya Kiingereza. Si hivyo, itakuwa ni kupoteza muda.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kidogo sasa katika sekta ya afya. Mhe. Naibu Spika, sekta ya afya nayo imewekwa katika kipaumbele na ni sekta muhimu kwa sababu hatutoweza kuja katika Baraza wala hatutoweza kwenda katika shughuli zetu za kusomesha au kukusanya kodi bila ya kuwa na afya. Katika kipengele hichi cha afya kidogo tu mimi nilikuwa na wasi wasi nimeona *figure* hapa ambayo imenikanganya.

Mhe. Naibu Spika, katika makisio ya vifo vya watoto na wajawazito wametengewa shilingi milioni 328 wakati Kitengo cha Ukimwi wametengewa shilingi bilioni 4.01. Hii Mhe. Naibu Spika, naiona ni *figure* kubwa. Licha ya kuwa wahisani ndio watakaochangia pakubwa katika sekta hii ya Ukimwi lakini pia hata mchango wa serikali hapa ni mkubwa zaidi kulikoni ule mchango ambao umeelekezwa katika vifo vya mama wajawazito na watoto.

Kwa hivyo, naiomba serikali hili iliangalie tukiangalia njia zile za kufikia mtu ambaye anapata maradhi ya Ukimwi na mtu ambaye anakufa kwa sababu uzazi ni njia ambazo ukenda kidini utakuta labda hawa walikuwa na sababu ya kusaidiwa zaidi kuliko hawa ambao wameipeleka mikono yao Waarabu wanasema *"Walaa tulku aydiakum illa ltakhaluqa".* Usiipeleke mikono yako katika maangamizi. Naomba nisieleweke vyengine.

Mhe. Naibu Spika, sitaki nichukue muda sana nakwenda kidogo sasa katika sekta ya nishati. Mhe. Naibu Spika, wajumbe wako wengi wameizungumzia sekta hii lakini na mimi nataka nizungumzie. Sekta hii bado naona kwamba haijapewa umuhimu wa pekee, tukitilia maanani kwamba hayo mapinduzi yote ya kilimo, mapinduzi ya elimu, mapinduzi ya viwanda tutakayoyafanya bila ya kuwa na nishati hii hayatofikiwa.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunataka kuwekeza katika kupitisha mkonge ambao utaleta umeme lakini tumesahau kwamba tabia nchi hivi sasa imebadilika. Huko ambako unazalishwa huu umeme kuna mabadiliko makubwa sana ya tabia nchi na matokeo tunayaona. Hakuna aliyekuwa katika mitaa yetu hapati mgao wa umeme, sasa huu umeme hauna *guarantee* na sisi tunataka kuleta mapinduzi ya kilimo. Sasa tutayafikiaje mapinduzi hayo ya kilimo bila ya kuwa na umeme.

Mhe. Naibu Spika, mapinduzi ya kilimo yataletwa zaidi na kilimo cha umwagiliaji ambacho kitahitaji zaidi umeme. Sasa mimi ningeiomba serikali kama imekusudia kweli kutatua tatizo hili basi ingekwenda sambamba. Leo tunatafuta umeme mbadala na huku tunaendelea kuzika mitambo yetu ili kuondoa kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, sitaki nichukue muda wako naomba tu na mimi niseme kwamba hotuba ni nzuri japo hatujaichangia vya kutosha, lakini kwa vile na mimi naogopa nisije nikaitisha uchaguzi mwengine basi naunga mkono hoja.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache niliyonayo. Mhe. Naibu Spika, pili nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake kwa utaalam mzuri wa kuichambua bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukisikia tu kama uchumi wa nchi umekua au pato la taifa limekua, lakini uchumi huo au pato la taifa ukuaji wake hauna tafsiri maana yake watu wetu wa chini waliokuwa hali zao ni za chini hauendani nao. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri katika hili ukuaji wa uchumi huo uendane

na matakwa na hali za wananchi wetu wa chini wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, ombi langu kwa Mhe. Waziri kwamba ukuaji huo uendane na watu wa Zanzibar wa hali za chini kabisa waliokuwa hawana mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niipongeze serikali kwa kutoa vipaumbele katika nyanja nyingi. Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 34 ibara ya 57 mpaka 59 imezungumzia kipaumbele cha elimu. Mhe. Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, kila mwananchi wa nchi hii anatakiwa apate elimu. Serikali ina nia nzuri na imetangaza mengi kuhusu elimu. Lakini nataka nimuombe Mhe. Waziri katika kulikuza hili la elimu, elimu ina vipengele vingi na ina mipangilio mingi. Elimu inaanza katika ngazi za chini kuanzia maandalizi, msingi mpaka sekondari.

Mhe. Naibu Spika, kuna wenzetu wa hali za chini wanyonge vikwazo vya kulipia ada ya elimu wanaweza wakashindwa kuchangia kwa sababu kuchangia elimu ni mtihani. Kuna watu ni wanyonge hali zao ni za chini kimaisha, mzazi ana watoto wake watano na wote hao wanasoma na wanategemea kulipiwa na wazazi wao.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa hapakuwekwa kipengele cha kuondoa malipo ya elimu na wakati huo huo michango hiyo ya elimu inapishana haiku sawa. Namuomba Mhe. Waziri atufafanulie atuwekee wazi michango hii ya elimu kuanzia msingi mpaka sekondari iendane iwe ni asilimia ile ile, kama haikuwezekana kuondoshwa kabisa basi iwe angalau na mfuko mmoja.

Mhe. Naibu Spika, mwanafunzi anayetoka skuli ya maandalizi kuingia darasa la kwanza anachajiwa shilingi elfu saba mpaka elfu nane, aliyekuwa hakupitia maandalizi pengine anachajiwa shilingi elfu tisa na kuendelea. Skuli za sekondari kidato cha kwanza hadi cha nne anaanzia shilingi elfu saba mpaka elfu kumi na inatofautiana baina ya skuli hii na skuli nyengine. Kwa hiyo, Mhe. Waziri katika hilo naomba aliangalie sana kwa sababu wananchi wetu wana hali ngumu za maisha na elimu ni lazima kwa kila Mzanzibari. Sasa Mhe. Waziri awahurumie na awatazame kwa jicho la huruma wale wananchi wanyonge na wao waliokuwa wana haja ya kupata elimu.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye suala la kipaumbele cha afya ni muhimu kwa kila mwanadamu. Serikali kwa nia safi imetoa kipaumbele kwa afya na naipongeza kwa kuamua kujenga vituo vya afya vingi tu Unguja na Pemba. Lakini naiomba serikali kupitia wizara husika vituo vya afya hivi vinavyotaka kujengwa imani yetu Wazanzibari hasa wanawake kwa sababu wanawake ndio tunaopata tabu kubwa kwenye mambo ya uzazi, wanawake wajawazito na watoto wachanga, basi tunaomba sana tupatiwe tiba ya uhakika na iliyokuwa haina michango.

Mhe. Naibu Spika, enzi za miaka ya nyuma Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alitangaza afya bure, elimu bure, lakini bahati mbaya sasa hivi kila kitu kinalipiwa. Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wanapata tabu, wananchi wetu wana maisha magumu kupindukia, naiomba serikali iwasaidie sana wanawake kwani kumsaidia mwanamke ni kuisaidia jamii. Unapomsaidia mwanamke katika nyanja yoyote ile kuanzia kilimo, afya na elimu basi tayari unaisaidia jamii kwa sababu mwanamke ni mlezi, mzazi, matatizo yote ya kidunia yeye ndio yanayomfika mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kitu kimoja katika Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC)* wenzangu wengi wamelisemea suala la karafuu. Mhe. Naibu Spika, karafuu ni uchumi wetu na ni uti wa mgongo wa maisha yetu na ni zao letu kubwa la karafuu ndio tunalolitegemea Wazanzibari. Lakini cha kusikitisha zaidi asilimia kubwa ya mikarafuu imekufa haiulizwi, karafuu zinakosa bei na hizo zinazopatikana zinasafirishwa magendo kila anayekuja hapa analalamika. Kwa hivyo, naishauri serikali kupitia *ZSTC* au Wizara ya Kilimo na Maliasili nayo isimamie utunzaji wa mikarafuu, sio *ZSTC* iwe ni wanunuzi tu wa karafuu, itunze mikarafuu kwa sababu ndio mali yetu.

Mhe. Naibu Spika, haileti taswira nzuri kuwa mikarafuu au zao la karafuu kuanzia hizo enzi za kisultani karafuu zinachumwa zinakaushwa kwa jua tu baadae zinauzwa kwenye magunia yale yale. Kwa azma hii tuliyonayo kwa uchumi ulivyoshuka ipo haja ya serikali kutafuta utaratibu mwengine wa kuzikausha karafuu au kutafuta viwanda vya kuzisarifu karafuu hizo ili tuongeze pato letu la taifa. Kwa sababu wakati wa mvua karafuu huwa zinaharibika au zinaoza na ndio zao letu kuu tunalolitegemea hapa visiwani.

Mhe. Naibu Spika, nataka niishukuru serikali na kuipongeza kwa kutupatia umeme wa uhakika kisiwani Pemba lakini naomba nishauri mambo mawili. Katika kupata umeme huu wa uhakika na matumizi yake naomba uungwaji wa umeme katika kisiwa cha Pemba yale malipo yapunguzwe ili tupate kutumia vizuri rasilimali yetu hii ya umeme.

Mhe. Naibu Spika, pili tufanye mbinu mbadala ya kutafuta umeme wetu wenyewe wa uhakika aidha kupitia njia ya upepo au jua. Mhe. Naibu Spika, hilo linawezekana ni kutafuta tu utafiti na sisi tukapata kuendelea katika shughuli zetu. Kila siku tusitegemee tu cha kugaiwa au kukopeshwa tukategemea wahisani.

Mhe. Naibu Spika, naipongeza serikali kwa kutoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo. Lakini kilimo kimezungumzwa sana asilimia kubwa ya wakulima wa mpunga na mboga mboga ni wanawake. Wanawake wanalima sana mboga

mboga, wanalima mpunga, masoko yanakuwa ni tatizo kwao. Halafu wakati huo huo mpunga wanalima lakini hawana wataalam. Kwa hiyo, naiomba serikali iwatafutie wataalam wa kulima ili wapewe maelekezo mbolea, kutafuta dawa na nini tatizo.

Kwa sababu mara hii ninavyosema Mhe. Naibu Spika, asilimia kubwa ya wakulima wa Wilaya yangu ya Wete wamepata hasara kubwa. Kwa hiyo, ipo haja Mhe. Waziri kwenda kuwatembelea na kuwapa pole jinsi walivyopata hasara ya kilimo hichi cha mpunga. Nguvu zao nyingi zimepotea, pesa zimepotea lakini kipato kimekimbia kabisa, mipunga imeiva kabla haijafumua.
Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwenye suala la maji. Maji ni uhai na suala la maji ni tatizo na litaendelea kuwa tatizo, sijui tatizo liko wapi. Kwa sababu Mhe. Waziri wetu hapa anazungumzia kila siku patachimbwa visima vingapi lakini bado suala la maji limekuwa tatizo. Mhe. Naibu Spika, binadamu ukikosa maji unakuwa na matatizo mengi, uchafu hauadimiki, nchi yetu yote inanuka kwa kukosa maji, uchafu mtupu haieleweki kila unapopita. Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri suala la maji litiliwe mkazo.

Mhe. Naibu Spika, naipongeza sana serikali kwa kutoa kipaumbele cha elimu na kusema kwamba itajenga skuli 15 Unguja na Pemba. Lakini katika kujenga skuli hizo isiwe ni mabanda tu, mabanda hayo yawe na walimu wazuri, walimu ya sayansi, hisabati ambapo haya ndio masomo magumu kufahamika. Watoto wetu wanapata tabu kwa hiyo wanatakiwa wapatiwe mafunzo mazuri ili waelimike na waje watusaidie baaadae.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache katika bajeti hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa jitihada yake kubwa aliyoifanya alipokopa, alipogaiwa lakini alimradi kufanikisha bajeti hii kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, bajeti imeshachangiwa sana michango mizuri tu kutoka kwa wajumbe. Kwa hiyo, hatuna haja ya kurudia yale kwa yale kupoteza muda. Mimi nasema wajumbe wote wanaochangia yote wanayoyachangia nayaunga mkono na bajeti naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya mwaka 2011/2012. Mhe. Naibu Spika,

kwanza nichukue fursa hii ya kumpongeza kaka yangu, shemeji yangu, Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa kuweza kuandaa bajeti nzuri ambayo imeleta matumaini kwa wananchi wetu wa Zanzibar katika mwaka huu 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wetu mpendwa Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein kwa kuweza kumuamini na kumchagua waziri wetu huyu kwa kumpa kazi hii ambayo sote waheshimiwa tumekuwa na imani nae na tuna imani kubwa kwamba mambo haya yatakuwa mazuri katika kipindi hichi cha bajeti hii ya 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niende katika suala la kilimo. Mhe. Naibu Spika, suala la kilimo Mhe. Waziri amelieleza katika ukurasa wa 22 hadi 24. Kwa kweli ni matumaini makubwa ambayo tuko nayo waheshimiwa pamoja na wananchi wa Zanzibar kupitia kilimo kwa sababu kilimo ndio uti wa mgongo kwa kila mwananchi wa Zanzibar.

Kwa sababu kilimo Mhe. Naibu Spika, ndio tegemezi la wananchi wetu kwa asilimia 90 kama alivyosema Mhe. Waziri katika hotuba yake kwamba wananchi wa Zanzibar wanategemea kilimo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha na kutekeleza yale ambayo yameelezwa katika bajeti hii. Kwa sababu suala la kilimo wakulima wetu wanahitaji msukumo mkubwa katika kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu. Wakulima wetu wanahitaji pembejeo, wakulima wetu wanahitaji mabadiliko ya nyenzo za kulima kwa sababu wakulima wetu huko mashambani wamezoea ukulima ule wa kizamani kwa kutumia vijembe kongoroka. Mhe. Naibu Spika, nadhani tubadilike tuachane na vijembe kongoroka serikali ijitahidi kuleta mabadiliko kununua zana za kisasa ili kuondokana na kilimo tegemezi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa nije katika utalii. Mhe. Naibu Spika, serikali yetu inategemea pato kupitia utalii baada ya zao letu la karafuu kurudi nyuma katika kutegemea kupata mapato katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ningemuuliza tu Mhe. Waziri kupitia suala hili la utalii tumejipanga vipi katika soko hasa hili la Afrika ya Mashariki ambalo waheshimiwa wengi wamelizungumza. Serikali ya Zanzibar imejipanga vipi kupata fursa ya kutumia katika soko hili la Afrika ya Mashariki ili kuongeza utalii wetu.

Halikadhalika Mhe. Naibu Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri wenzetu Tanzania Bara wanahamasishwa sana katika soko la ndani, yaani utalii wa ndani. Sijui Mhe. Waziri amejipanga vipi kushajihisha wananchi ili kuweza

kuwekeza katika utalii wa ndani. Hili linaweza kutusaidia kwa sababu duniani kunatokea mabadiliko mbali mbali, sasa hili soko la ndani katika kushajihisha wananchi kutumia utalii wa ndani ningeomba wizara husika ya mambo ya utalii iweze kushajihisha wananchi kuweza kuwekeza katika suala hili la soko la ndani.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya soko la ndani lakini kuna maeneo ambayo yanahitajika kufanyiwa msukumo zaidi hasa katika nchi kama vile China, India, Nchi za Kiarabu pamoja na Uturuki ili kuweza kuhamasisha na kujipanga kuwekeza katika nchi hizo ambazo tusitegemee tu nchi za Ulaya au Marekani na nchi nyengine. Hivi tumejipanga vipi kuwahamasisha hawa au kutangaza nchi yetu katika nchi hizo. Ningeomba Mhe. Waziri kufanya kazi za ziada au kutueleza ile mipango ambayo inafanya kushajihisha watalii kutoka nchi hizo.

Mhe. Naibu Spika, katika utalii kuna upungufu sana au kuna uvujaji wa mapato. Mhe. Naibu Spika, mimi nafahamu sana mambo ya utalii, wawekezaji wetu wanatumia ujanja na mipango mbali mbali kuweza kupoteza mapato. Wageni wengi wanaokuja kutoka nchi za nje kupitia uwanja wa ndege wengine wanakuja kwa bandarini mapato mengi yanapotea. Kwa hivyo, sijui Mhe. Waziri atatueleza vipi mikakati ambayo inafanywa ili kuweza kuyazuia yale mapato tunayoyapata katika sehemu hizi za watalii wanaopitia uwanja wa ndege pamoja na bandarini.

Mhe. Spika, utalii unaweza kutuongezea mapato lakini pia tuangalie mambo mengine ya nchi yetu ilivyo. Mhe. Naibu Spika, watalii watakapokuja hapa wana imani kwamba Zanzibar ni nchi ambayo ni salama na amani na hilo tunamshukuru Mwenyezi Mungu usalama na amani upo. Lakini hali ya usafi wa nchi yetu na hili limeshasemewa sana, ukweli hali ya usafi hasa katika jiji letu la Zanzibar mji haufai, sasa watalii wanapokuja wanaona hiyo Zanzibar tunayoisikia hali yake ni hii. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba anazungumza na Baraza la Manispaa kuweza kuweka mji wetu safi, mji wetu unanuka sio watalii wanakuja Darajani wanakuta hali sio nzuri.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea nachukua fursa hii pia kuipongeza Wizara jana nimeona katika vyombo vya habari kuna ulinzi shirikishi ambao wamehusisha wawekezaji wa mambo ya utalii. Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuweza kufanya suala kama lile

Baada ya hapo nakuja kwenye suala la maji. Mhe. Naibu Spika, suala la maji limezungumzwa na waheshimiwa wengi, kilio kimekuwa kikubwa juu ya suala la maji, hatuwezi kuleta maendeleo kama hakuna maji.

Mhe. Naibu Spika, nazungumzia katika Jimbo langu la Rahaleo. Pale Rahaleo raha ni leo lakini sasa Mhe. Naibu Spika, raha ile haipo sasa, raha imepotea ya Rahaleo, maji hakuna. Mhe. Spika, maji ambayo yanakwenda Mji Mkongwe, maji yanakwenda Kikwajuni basi maji lazima yapite Rahaleo. Lakini wananchi wa Rahaleo maji hawapati. Kwa hivyo, ningeomba awezeshwe Mhe. Waziri wetu wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili kuondoa tatizo la maji katika mji wetu wa Zanzibar. Suala hili Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelizungumza, tunamuomba kwa sababu hatuwezi kutatua matatizo ya maji kama waziri wetu hajawezeshwa.
Kwa hivyo, serikali ijitahidi kuweza kumuwezesha na hiyo miradi ambayo ipo basi itekelezwe, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukizungumza, lakini utekelezaji umekuwa mchache. Mafundi wetu wale ambao wanashughulika na mambo ya maji, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hivyo, naomba waziri awezeshwe, halafu waziri aweze kuhakikisha kwamba utekelezaji unapatikana.

Mhe. Naibu Spika, nije katika nyanja ya habari ni sehemu moja muhimu sana ya kueneza hata huo utalii, kwa sababu bila ya kutumia hitengo vya habari na kuutangaza utalii, basi utalii hauwezi kutusaidia. Kwa hivyo, ningemuomba waziri kuweza kutumia kila hali ili kujitangaza na kuitangaza nchi yetu katika nchi mbali mbali kwa kupitia wizara hiyo ya habari ili kuitangaza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nije katika sekta ya biashara. Mhe. Naibu Spika, sekta ya biashara ni sekta muhimu sana. Mimi nashukuru na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kumchagua mtu ambaye anahusiana na mambo ya biashara. Lakini Mhe. Naibu Spika, suala la biashara wananchi wetu wanalia, ukija katika suala la viwango vya vyakula na viwango vya vitu mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, wananchi wanasikitika sana na kulia sana, viwango vya vyakula vimekuwa vibaya sana.

Ukija kwenye mchele hayo mapembe kwa kweli ni kitu cha kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika. Unaweza kwenda sokoni pale kama Darajani ukanunua mchele wa basmati, lakini unapofika nyumbani Mhe. Spika, basi utapigwa nao wa uso, kwa sababu hauliki.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu ni maskini wanakula basmati skukuu hadi skukuu, lakini Mhe. Naibu Spika, hali ya viwango vya vyakula ni vibovu. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri hili suala la viwango basi liangaliwe zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hata katika viwango vya vitu vya majumbani pamoja na magari. Juzi mimi nilikwenda kununua *spare* ya gari yangu kwenye duka moja maarufu, lakini baada ya kununua *spare* ile na kuipeleka kwa fundi

nikaambiwa hii *spare fake.* Niliporudi kwa vile ni mheshimiwa ndio akaanza kuniomba mheshimiwa samahani, tumekuuzia hatukujua kama iko hivi na hivi. Kwa hivyo, haya mambo yapo Mhe. Naibu Spika.

Halikadhalika Mhe. Naibu Spika, kama wiki moja nyuma nilikwenda kununua jiko la kupikia, siwezi kulitaja duka gani, lakini nilikwenda kununua. Mhe. Naibu Spika, kufika nyumbani jiko lile haliwaki, yaani halifanyikazi, tatizo ni viwango. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tuangalie sana suala la viwango.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, kwa sababu waheshimiwa wengi wamezungumza. Nitakuwa sina fadhila kwa wana michezo wenzangu. Mhe. Naibu Spika, mimi nawashukuru sana wana michezo wa Zanzibar wananipenda na mimi nawapenda, bila ya kuzungumza michezo hapa sina la kuwaambia wana michezo wenzangu.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii haikuzungumzia suala la michezo na kuendeleza michezo. Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri chonde chonde wana michezo Zanzibar ni wengi, kwa hivyo bajeti hii iwaangalie wana michezo, kuinua hali ya viwanja. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika kitabu cha bajeti hii kwenye kitabu cha pili kile kinaeleza mambo ya michezo. Kwa kweli serikali bado haijawekeza katika sekta ya michezo.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aangalie sana sekta ya michezo, kwa sababu haya yote tunayoyafanya, yaani ukishapata chakula kizuri, ukishapata maendeleo mazuri, halafu jioni unataka kwenda kuburudika ukae kidogo uangalie mpira. Sasa mpira hamna. Kwa hivyo, bila ya kuyatizama haya na kuitilia mkazo serikali basi michezo itakufa, michezo inaitangaza nchi. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa jicho la huruma kuhusu wana michezo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema haya, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Rahaleo, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Ashura Shariff Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi hii, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Subhanahu Wataallah aliyetujaalia uhai akatuwezesha kuwa katika Baraza lako hili tukufu tukijadili maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia sina budi nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi wakati wa jioni hii. Mhe. Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mhe. Waziri

kwa jinsi alivyoandaa bajeti hii na kutufikishia hapa mezani na hadi usomaji wake pia.

Mhe. Naibu Spika, kupanga ni kuchagua. Mhe. Waziri ametuchagulia mambo ambayo yana maslahi na taifa letu. Naamini kwamba kuumiza kwake kichwa na kutumia muda wake pamoja na wataalamu wake hii ni kwa nia nzuri ya kuwatendea haki Wazanzibari na kuwafikisha katika maendeleo endelevu kwenye kipindi cha mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, kusema kweli Mhe. Waziri wakati alipokuwa anaisoma bajeti hii katika Baraza lako tukufu, nilikuwa nakumbuka sana ile hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar alipoisoma katika Baraza lako tukufu wakati wa ufunguzi wa mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameyaangalia kwa kina yale ambayo Mhe. Rais aliyagusa katika Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa hili kwa miaka mitano. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walikuwa shahidi kupongeza hotuba ile na kusema ndio dira ya maendeleo na ndio mstari aliyopita Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendele.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia katika kitabu hiki kwenye sehemu ya vipaumbele, Mhe. Waziri yale yote ambayo ameyasogeza ni muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, nikianza katika vipaumbele ambavyo Mhe. Waziri amevitaja hapa kwenye ukurasa wa 73 alipoigusa afya ya jamii, naomba hapa niweze kueleweshwa. Namuambia Mhe. Waziri afya ya wananchi wa Zanzibar ni muhimu. Pia azingatie na kuona kwamba wanawake wa Zanzibar wanahitaji afya, waendane sambamba na mradi ambao ulianzishwa mwaka 2010/2011 wa kupunguza vifo vya mama na watoto.

Mhe. Naibu Spika, hili nalisema kwa sababu sisi wanawake wa Zanzibar tunategemea sana bajeti yake kutugusa kwa asilimia mia na sio kutugusa kwa maneno tu, bali utekelezaji wake ndio utakao wakwamua wanawake hawa na kuweza kufikia maendeleo na ile dhana ya kupunguza vifo vya mama na watoto kuondoka kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nikigusa katika sekta hii hii ya afya niangalie katika hospitali ya Rufaa ya Mnazo Mmoja, hospitali ambayo ni tegemezi kubwa ya wananchi wa Unguja pamoja na Pemba, ambao mara nyengine hupewa rufaa kutoka Pemba kuja Unguja.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa nasema katika hospitali hii sehemu ya ICU ni mtihani. Mimi binafsi yangu nimekwenda na nimepata maelezo ya kutosha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika bajeti hii

atuhakikishie kumthibitishia Waziri wa Afya kwamba sasa tutaondokana na hii hali ilivyo hivi sasa, kuwa mgonjwa akipelekwa basi ni ajabu, maana yakitokea ya kutokea basi anapelekewa mkono kama yuko nyumbani. Mitungi ya gesi ya *oxygen* haipatikani.

Mhe. Naibu Spika, kama afya inayotakiwa ni hiyo, kina mama huwa wajawazito na wakati mwengine hupata vifafa vya mimba na kusababisha kupelekwa pale kwa ajili ya kupata *oxygen* hiyo. Je, Mhe. Waziri hali ikitokea hivyo, haya ambayo tumeyaandaa itakuwaje. Namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie sana kwa kina, katika fungu la Wizara ya Afya alipeleke jicho la huruma na kuona kwamba haki hii inatendeka na kufanyiwa juhudi na kuonekana kwamba sehemu hii inatia matumaini.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mengine ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja. Katika hotuba yake alisema kwamba atatoa kipaumbele cha kununua vifaa pamoja na dawa muhimu za hospitali. Siku hizi Mhe. Naibu Spika, unapokwenda pale na kuandikiwa dawa, basi utakazozipata ni zile za bei nafuu sana na zile ambazo mwananchi wa kawaida hana uwezo wa kuzimudu basi anatakiwa kuzinunua.

Mhe. Naibu Spika, ningependa Mhe. Waziri katika mtiririko wake wote ambapo ameonesha imani ya kutosha juu ya kuwatendea wema na kuwafikisha Wazanzibari katika hali ambayo tunaitarajia basi lionekane hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuna mchango hapa unatokea wakati wa kwenda kujifungua mama mjamzito anatozwa Shs.40,000/-. Ningeomba kwa kupitia Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hili alione ili haki itendeke basi wanawake hawa wasitozwe chochote, ili waweze kula matunda ya serikali yao, kwani hawa wanawake ambao katika taifa hili ni wa kutegemewa sana, kwa sababu ndio wazalishaji wakubwa, ndio walezi na ndio watetezi wa haki. Kama mtaangalia hata kwenye shughuli za kisiasa za kufanikisha kwake basi ni kuwepo kwa wanawake katika taifa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja katika kilimo cha kisasa, kilimo ambacho kwa ile hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar yeye alisema anataka kuleta mapinduzi ya kilimo hapa kwetu Zanzibar, ili kuwabadilishia hali Wazanzibari waondokane na kilimo cha kijembe kongoroka na waweze kufikia kilimo cha kisasa kabisa ambacho kina pembejeo, kina mabwana shamba, utaalamu na kuweza kuwafikisha kuzalisha chakula chao na pia kuweza kuzalisha kwa ajili ya akiba na kuweza kuuza nje.

Mhe. Naibu Spika, narudi tena kwenye masikitiko yangu. Dhana hii ambayo Mhe. Waziri umeigusa kwa kweli ni dhana muhimu sana na inakubalika.

Nasema tumeipokea, lakini mheshimiwa hii dhana haitaki kuwa ya muda mfupi yaani ya mpango wa mwaka mmoja, inataka kuwa endelevu. Uanzishwaji wake naamini kuwa utakuwa wa pole pole lakini unataka uwe endelevu, pia uwe unafikiria kwamba wazalishaji wakubwa na wana vikundi wakubwa kwa hapa kwetu Zanzibar ni wanawake. Wanawake wanahitaji sana mchango huu na wamepatwa na hamu kubwa ya kutaka kusikia bajeti hii baada ya kusomwa kuona kuna mabadiliko ya kuletewa kilimo cha kisasa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niingie katika ukurasa wa 69 ambao umegusa utafiti na maendeleo. Mhe. Naibu Spika, nimefurahi mno ulipogusia kwamba umeunda tafiti kwa kila kitengo katika mawizara ya serikali kwa ajili ya utafiti. Lakini hili mimi ningelipendekeza kwake Mhe. Waziri kuwa na taasisi moja tu hapa kwetu Zanzibar ambayo itashughulikia suala la utafiti, ili tuone mipango yetu ya kimaendeleo na sera inatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, pia ningemshauri Mhe. Waziri hapa kuviwezesha vyuo vikuu vilivyomo ndani kuweza kufanya tafiti zetu. Suala hili naomba liwemo katika utaratibu huo kwa vile na sisi hapa Zanzibar tumeanzisha vyuo vikuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mengi ni mazuri, yanapendeza mno na nasema wengi wamechangia na wengi wameyagusa mengi. Lakini niguse kidogo katika ukurasa wa 10 kwenye kifungu cha 13, nimeona hapa Mhe. Waziri umelitaja pato la taifa kwa mtu binafsi.

Mhe Naibu Spika, nimeona hapa Mhe. Waziri umetaja pato la mwananchi wa kawaida katika mwaka 2010 kwa dola za Kimarekani 561 ambazo kwa pesa zetu za Kitanzania ni Shs. 783,370/= ambazo kwa wastani wa dola 1.6 yaani pato la mwananchi wa kawaida, ambazo ni sawa na TShs. 2,340/=. Hapa Mhe. Waziri nimeshtuka kidogo. Kilichonifanya nishtuke ni nini, ni kusema kwamba mwananchi wa kawaida hapa kwetu Zanzibar anaweza akazichuma Shs. 2,340/= pengine na mwengine akashindwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, najiuliza kuwa tuna nia ya kuimarisha afya, lakini mlo hautimii kwa Wazanzibari. Shs. 2,340/= hata mkate wa asubuhi mtu na wanawe watano hamudu, sisi wanawake kwetu imekuwa ni mzigo mkubwa na balaa, tunaambulia matalaka, tunaendelea kuishi katika maisha ya kuzurura. Hivyo basi imekuwa kwetu ni mzigo mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametaja ongezeko la fedha kwamba mwananchi wa kawaida pato lake limeongezeka. Lakini sote ni mashahidi kwamba Shs.2,340/= huwezi kumudu mlo wa mara tatu kwa siku uwe peke yako basi huwezi kushiba, je mtu ambaye ana watoto sita au saba na ana familia na ana wazazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuliona hili ningeomba nimshauri Mhe. Waziri aliangalie kwa kina na alitazame kwa moyo wa huruma kabisa. Aangalie yeye mwenyewe haiwezekani kuondosha ushuru wa hizi bidhaa za mchele, unga wa ngano pamoja na sukari ili tuwaondolee mzigo wananchi wetu wa Zanzibar ili wakaweza kumudu maisha. Mambo yale ya mapato yakatozwa ushuru zaidi katika mambo ya anasa ili mulo watu wakaweza kuumudu wote.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba ngoja ngoja inaumiza matumbo, nikiwa na maana kwamba Zanzibar ni kisiwa kilichojaaliwa kuwa na neema kubwa, ile kuwa kisiwa tu peke yake basi ni neema. Kisiwa hiki kimezungukwa na bahari.

Mhe. Naibu Spika, baada ya michango ya muda mrefu na ufuatiliaji wangu wa vipindi vya Baraza wakati mimi nilikuwa nje niliwahi kusikia kwamba kumeibuliwa utaratibu mpya wa rasilimali mpya hapa kwetu visiwani, ambao utatuondolea kero na umasikini na vitu vyote ambavyo vimetukabili kwa wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulisema hili kwa sauti pana na kwa niaba ya wanawake wa Zanzibar wote kuwa tunataka rasilimali yetu ya mafuta na gesi ichimbwe mara moja, ili kutuondolea kero na adha iliyotushika hapa kwetu Zanzibar.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Naibu Spika, niseme misingi miwili au mitatu ambayo ningemkumbusha Mhe. Waziri kuweza kuitumia kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti yake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe malizia.

Mhe. Ashura Shariff Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Nasema kwamba maadili ya kazi ni msingi wa maendeleo ya watu. Misingi ya kujiongoza basi tujifanye wenyewe tunaweza kujiongoza. Uwajibikaji katika taifa hili umewekwa nyuma ya mgongo, kila mmoja hatimizi majukumu yake, tunaomba uwajibikaji.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo pia niseme kwamba kila jambo lifanywe kwa wakati. Wakati sasa umefika na mafuta tunasema ya chimbwe

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda umemaliza, malizia.

Mhe. Ashura Shariff Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Kaskazini B, naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru kwa michango tuliyotoa tangu asubuhi mpaka hivi jioni, nawashukuru wote waliopata nafasi. Naomba niseme mambo mawili kabla hatujaahirisha kikao chetu. Katika orodha ya wachangiaji tumebakiwa na waheshimiwa *backbencher* watatu. Wa kwamza Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Ussi Jecha Simai na Mhe. Rufai Said Rufai. Hapo hapo tuna mawaziri tisa wanataka kesho watie baraka kwenye bajeti ya serikali.

Kwa hivyo, nashauri kwamba kesho baada ya maswali na majibu tutaanza na *backbenchers* hao kwa dakika kumi kumi, halafu tuwape Waheshimiwa Mawaziri, ili jioni tumpe nafasi Mhe. Waziri aje kutupa majumuisho na kupitisha bajeti kuu ya serikali. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kesho kazi ndogo ndogo zote tuziache, tuhudhurie kwa wingi ili kupitisha bajeti yetu ya serikali.

Baada ya hayo naahirisha kikao mpaka kesho tarehe 22/06/2011 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 22 June,2011 saa 3:00 asubuhi)